ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.

13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.

25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Saba - Tarehe 08 Juni, 2015

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka 2015/2016. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka 2015/2016. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 62

Taa za Barabarani kwa Mchina Mombasa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kuweka miundombinu ya kuongezea vyombo vya usafiri barabarani katika makutano ya barabara ya Mombasa kwa Mchina. Hata hivyo, kumekuwa na usumbufu kwa madereva kuchelewa kuvuka kwa sababu ya uwepo wa vituo vya daladala kwa kila upande wa barabara hiyo, vikiwa masafa mafupi tu baada ya kuvuka taa hizo.

a) Kwa nini vituo vile vya daladala visisogezwe mbele kidogo ili kutoa nafasi pana ya madereva wengine kuvuka pale taa zinaporuhusu.

b) Kwa kuwa madereva wengi hawajazoea taa zile ambazo zipo tofauti kidogo muelekeo wake, kwa nini kwa kipindi hiki wasiwepo askari wa barabarani kusaidia muongozo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni swali lake nambari 62 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:

Mhe. Mwenyekiti, Serikali kwa juhudi inazozichukua kuimarisha miundombinu, aidha ningependa kufahamisha kwamba hivi sasa gari za daladala zinaposimama hapana kituo rasmi cha daladala kwa sehemu zote za barabara, isipokuwa kinachofanyika ni gari za daladala kushindwa kusimama kwenye kituo rasmi kwa tamaa ya abiria na kuamua kusimama chini ya mpindo kitendo ambacho ni kosa kwa mujibu wa sheria ya usalama barabarani.

Serikali tutahakikisha kwamba mambo haya yanachukuliwa hatua kwa kushirikiana na wenzetu wa Jeshi la Polisi.

a) Mhe. Mwenyekiti, kituo rasmi cha daladala kutoka Kiembesamaki kuelekea Amani kipo mwisho wa nyumba ya marehemu Mzee Kassim Ali mkabala na kituo cha kuuzia umeme, ambapo pamejengwa sehemu ya kusimamisha gari *bay* na kituo cha daladala kutoka Mwanakwerekwe kuelekea Kiembesamaki kipo mwishoni mwa jengo la ghorofa mkabala na klabu ya BOT ambapo pamejengwa *bay.*

b) Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa taa za kuongozea magari zilizowekwa katika maeneo hayo zipo kwa ajili ya majaribio ili kuona mapungufu yaliyokuwepo ili yapatiwe ufumbuzi. Lakini hata hivyo upo mpango maalum wa kutoa mafunzo kwa watumiaji wote wa barabara wanaotumia makutano ya barabara mara baada ya kuondoa kasoro za mapungufu yaliyojitokeza katika taa hizo.

Hata hivyo madereva wote wa magari wanapaswa kujua sheria za barabara kama ulivyo wajibu wao.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla ya hapo nichukue fursa hii kumpa pole Mhe. Naibu Waziri kwa safari ya Michamvi siku mbili mfululizo na machofu aliyokuwa nayo nimuulize maswali mawili madogo sana ya nyongeza.

Je, ni lini hatua za haraka zitachukuliwa ili madereva wa daladala wasimame karibu na sehemu hizo na huu wimbo mtaumaliza lini kama nyinyi ni dhamana ikiwa Waziri na Naibu Waziri kujenga vituo vya daladala mkaiga kama

mnavyotembea huko duniani ili kuondosha matatizo ya wananchi, mkizingatia Serikali ni wananchi na wananchi ndio Serikali.

Mataa mliyoyaweka hivi karibuni madereva wengi hawajapata elimu ya kutosha, je, lini mtafanya semina hiyo kama mliyofanya jana ili madereva wapate kufahamu umuhimu wa kutumia taa zile.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, la kwanza nimepokea ile pole lakini mimi kwenda kwetu sistahiki kupewa pole nadhani ni wajibu wangu kwenda kusalimia wazee wangu, kwani wamenilea wamenikuza na wao wana haki ya kula matunda yao.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kituo cha daladala hatua za haraka ni madereva kusimamia taratibu na sheria zao za uendeshaji wa magari nchini, sisi wajibu wetu Serikali, yeyote atakayetenda kinyume na sheria za nchi wajibu wetu ni kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kumshtaki, kumfikisha mahkamani ili haki iweze kutendeka. Kama Serikali wajibu wetu ni kutengeneza miundombinu ya wananchi ili waweze kupata huduma. Maeneo hayo tayari kuna eneo maalum la *bay* ambapo kutokusimamisha gari katika eneo lililokusudiwa ni kutenda kinyume na utaratibu wa sheria, na sisi kama Serikali tutamkamata na kumfikisha mahkamani.

(b) Mhe. Mwenyekiti, unaposema madereva tuwape semina barabara ile haina watu maalum wanaoitumia maana yake madereva wote wa Zanzibar wana haki ya kutumia barabara ile na kuona mataa yale. Wajibu wa dereva ni kujifunza na kuhitimu sheria za usalama barabarani. Imani yangu kwamba madereva wote wa Zanzibar hasa kwa utaratibu wetu, huwezi ukapata leseni ya kuendesha gari kama hujahitimu mitihani inayostahiki, ule wa nadharia pamoja na ule wa vitendo. Suala hili la taa nalo pia limezingatiwa. Unapohitimu matumizi ya barabara maana yake umehitimu pamoja na matumizi ya mataa barabarani yanayokuongoza badala ya kuwepo mtu anayekuongoza.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika majibu yake amesema kwamba haiwezekani kuwapa mafunzo madereva wote lakini katika majibu yake (b) amesema kwamba upo mpango maalum wa kutoa mafunzo kwa watumiaji wote wa barabara wanaotumia makutano hayo ya barabara mara tu ya kuondoa kasoro za mapungufu. Je, hao watakaopata mafunzo ni madereva wa aina gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, taa zile zinatumia *solar*, taa zile zimewekwa kwa majaribio anaposimama *traffic* pale katikati kwa ajili ya kusaidia kuongoza sambamba na ule mwenendo wa zile taa ndio mafunzo yenyewe yaliyokusudiwa. Alichokiuliza Mhe. Jaku aliuliza semina

ya watumiaji wa barabara kwa maeneo yale. Kwa hivyo tunaposema mafunzo kwa maana kwamba yule *traffic* anaposimama anakuelekeza ukiona mshare huu maana yake wewe upite huku, kwa sababu taa zilizokuwepo zina *bullet.*

Bullet moja inaongoza kushoto, *bullet* ya katikati ndio inaongoza katikati, watu wengi kinachowachanganya *bullet* ya kushoto inapowaka wao wanategemea kwamba ndio wanyooshe barabara. Wakati *bullet* ya kushoto haina *arrow* inapowaka *bullet* ya kushoto inakuongoza wewe upinde kushoto na ile ya katikati ndio inayokuongoza wewe uongoze njia kuelekea Mwanakwerekwe.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Naibu Waziri mjukuu wangu hapo Mhe. Issa Gavu naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa zile taa zilizopo pale *round about* kakiri zinatumia *solar* jambo ambalo siku za mawingu makubwa kama haya masika yaliyopita, taa zile zilikuwa zikitubabaisha sana kwa sababu ya kukosekana mwangaza wa jua, kwa hivyo zilikuwa wakati mwengine hazioneshi kutokana na muangaza ulikuwa hafifu au ulikuwa haupatikani sana siku za mvua. Je, ni lini Mhe.Waziri mtaunganisha taa hizi zinazotumia *solar* za pale na hata hizi za mjini maeneo yanayoongoza magari ni lini maeneo yale angalau mtayaunganisha na *grid* ya taifa ya umeme ili kusudi ziweze kuwa hazitupi shida kwa zile siku za dharura tu za masika.

(b) Kwa kuwa umekiri kwamba kutoka Mombasa hadi Kwerekwe ni kile kituo kilichopo mkabala na nyumba ya Mzee Kassim Ali pale ndio kituo pekee cha dalala ambapo hakitoshi kama ambavyo kituo hiki kilichopo karibu na Kisiwandui ambapo kinaleta usumbufu sana kile cha Mombasa kule na hata hapa Kisiwandui, yaani daladala zimekuwa kero sana. Na kwa kuwa madereva wanalipa kodi, wanalipa kodi za *road license,* je, ni lini Serikali itaamua kujenga *car parking* nzuri kwa ajili ya daladala hapa mjini na maeneo ya vijijini, kusudi isitoe usumbufu hususan siku hizi za wagombea kutaka kuingia pale kwenda kuona kaburi la marehemu Mzee Amani Karume pale Kisiwandui, kupata tabu sana katika kwenda kunadi azma yao!

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ningetegemea ile juzi kwenye semina Mhe. Nassor angekuwepo haya maswali asingeuliza. Maana tumepata nafasi nzuri ya kuyazungumza haya, kutoa kasoro, kutoa maoni na pengine alikuwa na mawazo mazuri zaidi tungeweza kuyachukua sisi Serikali kwa ajili ya kwenda kuyafanyia kazi. Lakini kwa kuwa bahati mbaya hakuwepo sina budi kumjibu na ni wajibu wangu kumjibu.

(a) Taa zile zimewekwa baada ya kufanywa uchambuzi mfupi wa kujiridhisha kwamba kwa mujibu wa hali ya nchi yetu kwa maana kwamba ile

climate bado matumizi ya *solar* yanaweza yakawa *annually* bila ya kuleta athari zozote. Tunatambua kwamba ziko siku jua letu linakuwa hafifu na sehemu kubwa inakuwa inachukuliwa na mawingu ama mvua, lakini bado haiathiri uwezekano wa mwanga kuweza kutunzwa na kuweza kuzalisha umeme utakaopelekea upatikanaji au mwangaza wa taa katika taa zile.

Lakini suala la kuweka akiba ya kuunganisha na *grid* sisi tunalichukua, lakini *study* yetu inaridhisha kabisa kwamba uwezekano wa *solar* ni mkubwa na wala hauna tatizo *annually.*

Swali la pili la maegesho, sisi Serikali tayari tumeanza kulifanyia kazi suala hili la maegesho na miongoni mwa mambo ambayo yatahitaji mabadiliko makubwa sana katika mji wetu ni suala hili la maegesho. Linahitaji mabadiliko katika matumizi, linahitaji mabadiliko katika mfumo wa usafiri nchini kwetu. Hatuwezi tukawa tuna maegesho mamoja halafu kuweza kuwa-*accommodate* watu wanaofuata huduma katika mji wa Unguja. Lazima tuwe tuna maegesho yasiyopungua mawili kwa kuona kwamba tuwe tuna vituo, kuwe kuna kituo cha kwanza magari yanafika yanasimama, kituo cha pili watu waweze kuondoka na *Taxi* na gari nyengine kwa ajili ya kufuata huduma katika mji wa Zanzibar.

Kwa hivyo kukwambia lini Serikali tutaamua, Serikali tayari tumeshaamua kinachotukwaza sasa hivi ni utekelezaji wake ambao unahitaji fedha. Mara tutakapopata fedha tutaamua na pahali gani kituo kitakuwepo sote tutakuwa mashahidi tutakwenda kukishuhudia kwa ajili ya kupata huduma zitakazotolewa katika maeneo hayo.

Nam. 23

Kubaguliwa kwa Nambari za Watahiniwa wa Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Ahsante sana kabla ya swali langu kujibiwa, ni kweli kwamba nilishindwa kuhudhuria mapema ile Semina kwa sababu ya kwenda kumpokea mgombea wangu wa Urais Mhe. Seif Shariff Hamad nilimpokea juzi *airport*, na nikasababisha kuchelewa. Lakini baada ya dibaji hiyo kabla ya swali langu kujibiwa naomba marekebisho madogo yafanywe.

Baraza la Mitihani la Tanzania (*NEC*) wanapowatathmini watahiniwa wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano huanza na herufi "S" kwa wale *School Candidates* na herufi "P" kwa ajili ya wale *Private Candidates* na halafu zikifuatia nambari zao za mitihani na baadae hufuatia nambari ya kituo cha mitihani na

nambari ya mtahiniwa, kwa hivyo mtahiniwa kutoka Tanzania Bara na anayetahiniwa kutoka Zanzibar sio rahisi kuwatambua pale mitihani inaposahihishwa (*marking*).

Na kwa kuwa Baraza la Mitihani la Zanzibar nambari zake za mitihani huanzia "Z" kwa watahiniwa kutoka Kisiwa cha Unguja na "P" kwa watahiniwa kutoka Pemba jambo linalowatafautisha watahiniwa kutoka Pemba na watahiniwa kutoka Unguja jambo ambalo sio zuri.

Je, ni sababu gani zilizopelekea nambari za watahiniwa kutoka Zanzibar ziweze kubaguliwa hivyo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Saleh Nassor Juma wa Jimbo la Wawi swali lake nambari 23 kama ifuatavyo:-

Kwanza Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa utaratibu wa Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa namba za utambulisho wa vituo vya mitihani vya kidato cha nne na kidato cha sita ambapo vituo vya watahiniwa wa Skuli huanzia na herufi ya "S" ikimaanisha *School Candidate* na kwa watahiniwa wa kujitegemea huanza na herufi ya "P" ikimaanisha *Private Candidate.*

Kwa upande wa Baraza la Mitihani la Zanzibar kwa miaka mingi utambulisho wa vituo vya kufanyiwa mitihani umekuwa ukitumia herufi ya "Z" kwa kumaanisha vituo vya mitihani vya Skuli ya Unguja na herufi "P" kwa vituo vya mitihani vya Skuli ya Pemba. Hata hivyo katika kikao cha nane cha Bodi ya Baraza la Mitihani Zanzibar kilichofanyika tarehe 30/9/2014 kilipitisha maamuzi ya kubadilisha mfumo wa utambulisho wa vituo vya mitihani na kuanzia mitihani itakayofanyika mwaka 2015 utaratibu mpya wa utambulisho wa vituo utakuwa kama hivi ifuatavyo:-

a) Vituo vya mitihani vya Sekondari vitaanza na ZS.7/ na kufuatiwa na nambari ya mtahiniwa.

b) Vituo vya mitihani vya Skuli ya Msingi vitaanza na ZP.7/ na kufuatiwa na nambari ya mtahiniwa.

c) Herufi Z inamaanisha Zanzibar, S - *Secondary* na P - *Primary* na 7 nambari ya kituo. Utambulisho wa vituo na nambari za watahiniwa vinatosheleza rasmi kwa skuli zote za msingi. Sekondari zitakazofanyika mitihani kwa mwaka 2015 kwa barua yenye kumbukumbu ya No.

BMZ/MT/69/Vol. 15.118 ya tarehe 27/01/2015 iliyozitaka skuli zisajiliwe kwa kufanya mitihani na kupewa nambari mpya. Tarehe ya mwisho ya usajili itakuwa ni tarehe13/03/2015. Utaratibu huo unaondoa utambulisho wa vituo vya mitihani kwa kumaanisha sehemu wanazoishi watahiniwa wa Unguja na Pemba.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa niipongeze serikali kwa kuweza kufanya marekebisho hayo.

(a) Kwa kuwa Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba kwa kipindi kirefu hiki mlichokuwa mnatumia "Z" kwa watahiniwa kutoka Unguja na "P" kwa watahiniwa kutoka Pemba, je, hamuoni kwamba ilikuwa mnawabagua Wazanzibari kwamba Zanzibar ni Muungano baina ya Unguja na Pemba, leo mnaitumia Zanzibar kwa Unguja tu.

b) Kwa kuwa mlikuwa mna-*identify* kwamba hawa wanatoka Pemba hawa kutoka Unguja kwa kutumia hiyo hiyo *sign,* je, hamuoni kwamba ilikuwa *possibility* ya kuwakandamiza watahiniwa wa upande mmoja ilikuwa kubwa katika kipindi chote hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakiri inawezekana ilikuwa tumefanya kosa na ndio maana Bodi ya Baraza la Mitihani Zanzibar baada ya muda mrefu ambao ilikuwa ikitumika ikaamua sasa kubadilisha. Lakini ambacho nataka kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi ni kwamba hakukuwa na ukandamizaji kati ya Unguja na Pemba, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, wanaosainisha mitihani hii ni Wazanzibari wanatoka pande mbili za Zanzibar kati ya Unguja na Pemba, kwa hivyo sifikiriii kama kutakuwa kuna upendeleo wowote katika usainishaji, kama inaweza ikawa sehemu moja inakandamizwa. Na huu utaratibu kama ulivyosema ni wa zamani, kwa hivyo tukichukulia zamani mpaka hii leo 2015 ingekuwa hakuna Mpemba aliyesoma wala hakuna Muunguja ambaye kasoma.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza baada ya kupata majibu mazuri na ya kuridhisha ambayo nayapongeza ya Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi suala langu ni kwamba siku zote kama kuna utaratibu unaendelea na ukahitaji kufanyiwa mabadiliko ya aina yoyote yale, maana ni kuwa utaratibu ule ulikuwa una tatizo. Mheshimiwa amesema kama ingelikuwa kuna matatizo hayo ambayo muuliza swali ameyauliza ingelikuwa hakuna Muunguja wala Mpemba aliyesoma. Maswali yangu mawili;

a) Kwanza ni sababu zipi za kimsingi na kuonekana kulikuwa na kosa gani mpaka kikakaa kikao hiki cha nane na kuleta marekebisho hayo ya usajili wa watahiniwa.

b) Kuna njia yoyote ya kumfanya mtu aliyesoma na akapasi ikawa wote hawapasi kwa sababu ya utaratibu huu uliowekwa kutokana na maneno ya Mhe. Naibu Waziri kwamba asingelikuwepo hata mmoja aliyekuwa amesoma.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, katika jibu langu mama ambalo nilitoa hapa nilikiri kama wizara imeliona hilo tatizo, kwa sababu tatizo ambalo limejitokeza linamaanisha au linaonesha wazi kwamba mwanafunzi huyu kituo chake kiko Pemba kwa kuanzia herufi ya "P", na mwanafunzi huyu kituo chake kiko Unguja kwa kuanzia herufi ya "Z" ndio maana tukaona wizara, na bodi ikaona hakuna haja ya kuonesha kama mwanafunzi huyu anatoka Unguja au anatoka Pemba tukaona tuweke *serial number* sasa za "ZP" na "ZS".

Kwa hivyo, niliainisha kwanza hapa kama tuliona tatizo lipo, lakini nilichosema mimi kama hakukuwa na upendeleo ni kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, watoto wanafaulu kutoka Unguja na Pemba, na nilisema kama walimu ambao wanasainisha wanatoka Unguja na Pemba. Kwa hivyo, hapo hapawezi kusimama upendeleo, na ndio nikatoa mfano kwamba ndio maana wanafunzi wetu wanapasi kutoka sehemu zote za Zanzibar. Nakushukuru Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu ya ufasaha. Mhe. Naibu Waziri mimi nataka sijui nikusaidie ama nikuokoe katika hoja nitakayouliza maana yake leo ukizingatia una bajeti yako hii hoja wajumbe wasije wakaichangia.

Suala la msingi la Mhe. Saleh linahusu mitihani, lakini hivi sasa Mhe. Naibu Waziri kuna kilio kikubwa cha wasimamizi wa mitihani haki yao ya stahiki hamjawapa mpaka leo. Kama ni kweli kuna msemo unasema *mpe mtu haki yake kabla jasho halijakauka*, si kuwavunja moyo walimu wetu hivi ukizingatia kazi ngumu wanayoifanya, ni lini mtawapa stahiki zao hizo ili Wajumbe wasije wakachangia hoja hii, hii hoja inaweza ikaleta mjadala kidogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama tuna deni la wasimamizi wa mitihani karibu milioni 133,000,000 ambazo bado hatujawalipa. Lakini mheshimiwa ambalo nataka niwaeleze Baraza lako Tukufu ni kwamba Baraza la Mitihani halina vyanzo vya mapato linatarajia

sana bajeti kutoka serikalini, na bajeti ambayo waliyoiomba ilimalizika kutokana na gharama za mitihani kupanda Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, mpaka hivi sasa tumewasiliana na Wizara ya Fedha wametaka tuhaulishe vifungu vyetu ili deni hilo liweze kulipika. Ninalotaka kuahidi Mhe. Mwenyekiti, kama deni hilo tutalipa kabla ya kumaliza bajeti hii kwa utaratibu huu ambao tumejipangia.

Nam. 34

Kuondoshwa kwa Wafanyabiashara

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Hivi karibuni Waziri wa Ardhi amefanya kikao na wafanyabiashara wa Nyumba ya Treni iliyopo Darajani na kuwapa muda wa mwezi mmoja tu waondoke ili kupisha ujenzi huo.

a) Je, jengo hilo linajengwa na nani na litagharimu kiasi gani.

b) Hivi karibuni kumeanzishwa Shirika la Nyumba Zanzibar. Je, hao ndio wataanza kazi hiyo hapa au tumeanzisha Shirika la Nyumba kwa mdomo bila ya utekelezaji.

c) Tangu kuanzishwa kwa Shirika hili kuna angalau nyumba moja tu waliyojenga au kukarabati.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati amefanya kikao na wapangaji na wamiliki wa Nyumba ya Treni iliyopo hapo Darajani na kuwapa muda wa mwezi mmoja kuhama jengo hilo lakini bado hawakutekeleza agizo hilo.

Muda huo wa mwezi mmoja ulikuwa ni muda wa ziada na ulitolewa katika kikao cha mwisho kilichofanyika tarehe 14/02/2015.

Pia ifahamike kuwa wapangaji wa Nyumba ya Treni kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa wamesimamishwa kulipa kodi ya jengo hilo, kwa hiyo ilibidi watekeleze agizo la serikali.

Mhe. Mwenyekiti, jengo la treni matengenezo yake yatasimamiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) gharama itakubalika baada ya kukaa *ZSSF* na Mamlala ya Mji Mkongwe.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa hivi karibuni (Oktoba, 2014) kumepitishwa Barazani Sheria ya Uanzishaji wa Shirika la Nyumba Zanzibar na hatua iliyofanyika ni kwamba sheria hiyo tayari imeshatiwa saini na Mhe. Rais, kinachosubiriwa sasa hivi ni Mhe. Rais kumteua Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo pamoja na Mwenyekiti wa Bodi. Ujenzi wa jengo la treni kama nilivyoeleza hapo juu utafanywa na *ZSSF* kwa makubaliano maalum na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Nyumba halijajenga nyumba hata moja lakini Shirika hilo litapotangazwa na litapoanza shughuli zake basi lina nia ya kufanya hivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu ya kusikitisha sana ya Mhe. Naibu Waziri na ya kuvunja moyo katika chombo chako hiki. Hivi juzi hapa niliuliza swali la banda la hospitali ya Mnazi Mmoja kwa watu wanaokwenda pale kuangalia wagonjwa wao ili wapate pahala pa kupumzikia, sehemu ndogo ambayo Mhe. Spika alikuwa ni Mwenyekiti yeye akaninyima haki ya msingi, na hili suala ilikuwa halitaki hata tenda kwa mujibu mimi nilikuwa ni Mjumbe.

Leo hii vigezo gani vimetumika kwenda kupewa *ZSSF* bila ya kutangaza tenda na ukiangalia *ZSSF* ni Shirika, hatuoni kauli zetu humu ni kupotosha wananchi ikiwa jengo kama lile la watu kwenda kusubiri wagonjwa wao lilitaka tenda, leo tenda gani iliyofuatwa hapa ukizingatia hizi pesa *ZSSF* ni mali za wananchi. Je, lini itatangazwa tenda au ndio ishaamuliwa tu kupewa *ZSSF*.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi.

Kwanza ningependa ieleweke kwamba *ZSSF* ni chombo cha umma kwa maana ni chombo cha serikali, na bado jengo lile linatakiwa kufanyiwa ukarabati litaendelea kuwa mali ya serikali. Kinachofanyika pale ni makubaliano maalum kati ya serikali na *ZSSF* ili jengo lile liweze kufanyiwa ukaratibu kwa mujibu wa mahitaji yanayohitajika na kwa mujibu wa taratibu za Mji Mkongwe. Kwa hiyo, jengo

litakalofanywa pale litakuwa ni jengo litakalotoa haiba ya kisasa lakini lenye kutimiza masharti yote yanayohitajika ya Mji Mkongwe. Hivyo, serikali imechukua hatua hizo kwa kuhakikisha kwamba ili baadae wale ambao wamo mle warudi tena kuendelea kufanya shughuli zao katika jengo lile. Na halikutaka liuzwe kwa sababu lingeuzwa ingekuwa tatizo kwa baadhi ya wale wafanyabiashara ambao leo wamo ndani, kesho wasingepata fursa hiyo.

Kwa hiyo, serikali imechukua utaratibu huo makusudi kutokana na upungufu wa kifedha wa serikali, na kwa sababu *ZSSF* ina uwezo wa fedha, kwa hivyo ndio ilikuwa ufanyike uamuzi huo wa serikali na ziliitwa taasisi nyingi za kifedha, lakini zile taasisi zilizokubali masharti ya serikali ni *ZSSF*, na kwa sasa utaratibu unaendelea ili jengo lile lijengwe na halitotumika utaratibu mwengine wowote wa tenda kwa sababu serikali haina nia ya kuuza jengo na lina nia ya kulikarabati liondoshee hasara ambayo ingeweza kutokea kwa wale wanaokaa ndani, maana litakapoanguka litaleta hasara kubwa sana kwa wale wafanyabiashara waliomo mule.

Na inajulikana wazi wangeuziwa wafanyabiashara binafsi wangewaondosha wale wenzao ambao wamekaa muda mrefu wakifanya shughuli za kibiashara, na baadhi yao tayari wameuziwa jengo lile. Kwa hiyo, utaratibu unaofanyika serikali ni halali na mzuri kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kutoa ufafanuzi mzuri kuhusu ukarabati wa jengo lile maarufu Jengo la Treni pale Darajani.

a) Swali langu la nyongeza lipo hapa, ni kwamba Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua kwamba serikali kupitia *ZSSF* wanakusudia kulikarabati jengo lile kwa muda gani.

b) Kwa gharama ya kiasi gani. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kama nilivyosema ujenzi ule nia na dhamira ya serikali sio tu kulikarabati kwa ajili ya kulirudisha katika hali iliyo bora zaidi, lakini pia liweze kutoa haiba nzuri kwa matarajio ya serikali kwamba eneo lile la Darajani lote ina nia ya kuliimarisha na kuendeleza majengo ambayo yataleta haiba ya Mji wa Zanzibar na iwe mfano wa ujenzi katika Mji wetu wa Zanzibar. Kwa hiyo, ilichukua muda katika kulifanyia matayarisho yote kukamilisha hilo. Lakini sasa ramani zake ziko tayari, michoro yote imekamilika na wakati wowote kuanzia sasa shughuli za ujenzi zitaanza kwa kuwa tumeshakubaliana uzuri na *ZSSF*, kuna baadhi ya mambo kidogo ya kitaalamu yakamilike ili ujenzi uanze.

Kuhusu suala la gharama kwa sababu bado shughuli nyengine zinaendelea siwezi kwa sasa kutoa ni gharama kiasi gani zitatumika. Lakini muda usio mrefu gharama zote zitajulikana na tutaweza kuliarifu Baraza lako Tukufu. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa jengo lile la treni muna wafanyabiashara wengi wanaofanya kazi katika jumba lile na wanaokaa kwenye jumba lile. Na kwa kuwa serikali azma yake ni kulifanyia marekebisho jengo lile ili liwe na haiba nzuri. Je, namuuliza Mhe. Waziri wale wafanyakazi waliomo, je, baada ya kumaliza matengenezo watarudishwa wale wale au serikali itawapa watu wengine.

Pili, Mhe. Waziri ni kwamba baada ya kuanzishwa Shirika la Nyumba Zanzibar tunaona wenzetu wa Tanzania Bara wana Shirika la Nyumba la Taifa lakini majumba yote ya Shirika la Nyumba yamepigwa muhuri unapopita unajua jumba hili ni la Shirika la Nyumba.

Je, ni lini serikali yetu itaona kuainisha aidha kwa alama yoyote ile ya kuona kama hizi nyumba ni za Shirika la Nyumba ili tuweze kuzijua nyumba zote kama hizi ni nyumba za Shirika la Nyumba. Na je, ni lini wataanzisha kujenga majumba ya mkopo nafuu ili kuwakodisha wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni nia na dhamira ya serikali kwamba wale wapangaji waliomo baada ya kufanyiwa ukarabati wapewe nafasi ya kwanza kukodishwa katika eneo lile. Kwa vyovyote itakavyokuwa, kwa kuwa gharama zitatumika kutakuwa na tofauti ndogo ya kodi, lakini naamini itakidhi haja na wale wote ambao leo wamekodishwa pale watafurahia kiwango hicho cha kodi, naamini pia watapendelea kurudi pale.

Kwa hivyo, kipaumbele cha kwanza wale wote walioko pale ni uamuzi wa serikali watafikiriwa wao kukodishwa upya. Lakini kama nilivyosema kuna baadhi mule wameuziwa rasmi na serikali katika maeneo ya jumba lile. Kwa hiyo, pia kutakuwa na mazungumzo maalum kati ya wananchi hao na serikali ili nao waweze kuelewa gharama zitakazotumika katika ukarabati huo.

Kuhusu suala la (b) kuwa na alama maalum ya Shirika la Nyumba la Zanzibar, kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri katika swali la msingi alieleza hapa kwamba matayarisho ya kuanzishwa shirika yanaendelea vizuri na si muda mrefu atateuliwa Mkurugenzi Mkuu wa kuendesha shirika hilo.

Kwa hiyo, mara shughuli zote zitakapokamilika za kitaasisi juu ya shirika hilo hapana shaka yoyote kutakuwa na alama maalum za shirika hilo katika nyumba hizo ili ziweze kueleweka, na serikali ina utaratibu maalum wa kukabidhi nyumba zake kwa shirika hilo, ili ziweze kuendeshwa vizuri, ziweze kutunzwa vizuri na ziweze kufanyiwa ukarabati ili wale wananchi wanaokaa humo wawe wanaishi kwa salama na furaha na zizidi kutoa tija ili shirika hilo liweze kujiendesha kibiashara na kuweza kujenga nyumba nyengine, ndio maana swali lake la (c) linaloonesha kwamba kuna utaratibu wa kujenga nyumba zenye kodi nafuu ndio nia na dhamira ya shirika hilo pamoja na serikali kwa jumla, ili kujenga nyumba zile za *low costs,* wananchi wetu waweze kuwa na makaazi bora ya kisasa.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2015/16 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

(*Majadiliano yanaendelea)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea na majadiliano yetu kuna taarifa mbili; ya kwanza inahusu yale maswali na majibu ya siku ya Ijumaa katika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anataka kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo yalikuwa yamejitokeza juzi.

Jengine kwa niaba ya Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa siku yetu ya leo tumepata wageni ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo. Wageni hao wanatoka katika Chama cha Ushirika cha Vijana Wasomi Zanzibar (*ZYMUMC*), jumla yao ni tisa wanaongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Imamu Mtumwa Vuai naomba asimame aonekane.

Katibu wao Bi Salama Mkadam Haji naomba nyote msimame muonekane kabisa. *(Makofi)*

(Hapa wageni walisimama ili kuonekana)

Mhe. Mwenyekiti: Haya kaeni, hawa ndio wageni wetu kwa siku ya leo. Baada ya maelezo hayo sasa tumkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili atusaidie huo ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi wa ziada juu ya majibu ya Swali Nam. 66 lililoulizwa hapa Baraza la Wawakilishi kufuatia majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati aliyoyatoa asubuhi ya tarehe 5/6/2015.

Mhe. Mwenyekiti, sote tutakumbuka kwamba Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati iliwasilisha majibu ya swali Nam. 66 ambalo liliulizwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusu ununuzi wa majenereta 32 ya Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*), swali ambalo lilijibiwa kwa ufanisi mkubwa na Mhe. Naibu Waziri wa wizara hiyo siku ya Ijumaa, tarehe 5/6/2015 ndani ya ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, yaliulizwa maswali mengine ya nyongeza na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na baadae Mhe. Mohammed Mbwana Hamad kuhusu hatma ya majenereta hayo. Kwa bahati Mhe. Naibu Waziri alijibu kwamba tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa agizo rasmi kwamba majenereta hayo yauzwe kwa maslahi ya umma ili itafute njia nyengine ya kuweza kuweka vyombo vya dharura ambavyo vitaweza kutusaidia.

Aidha, Mhe. Naibu Waziri aliongeza kwamba, wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umeme tayari wameshatoa tangazo na wamewahi kujitokeza wateja na kwenda kuangalia baadae hawakurudi tena.

Mhe. Mwenyekiti, hali halisi ni kama ifuatavyo. Ni kweli imebainika kuwa uendeshaji wa majenereta hayo una gharama ya pesa nyingi ambapo *unit* moja itagharimu shilingi 600 ikiwa ni ongezeko la shilingi 278 kwa *unit* moja kulingana na gharama za *unit* moja zinazouzwa sasa kwa mtumiaji wa umeme ambayo ni shilingi 222. Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya kulitafakari kwa kina suala hili imeamua kwamba, majenereta hayo yasiuzwe wala kukodishwa hadi pale serikali itakapokaa pamoja na Washirika wa Maendeleo kujadiliana namna bora ya kuyaendesha majenereta hayo. Kama ilivyokubaliwa katika mkataba wa ununuzi wa majenereta wa tarehe 10 Machi, 2010 *Article* ya 3 ya kifungu cha kwanza, Washirika hao wa Maendeleo ni Serikali ya Norway, Serikali ya Sweden na Serikali ya Uingereza ambao wote kwa pamoja walichangia dola 11,500,000 sawa na asilimia 88.46 ya gharama zake, ambapo SMZ ilichangia dola za Kimarekani 1,500,000 sawa na asilimia 11.53 ya gharama hizo.

Kwa hiyo, kwa sasa serikali haina nia ya kuyauza wala kuyakodisha mpaka pale ambapo tumekaa na Washirika wa Maendeleo kwa namna moja au nyengine ndipo uamuzi rasmi wa serikali utatolewa.

Naomba kuwasilisha, nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutoa taarifa ya serikali. Lakini utaratibu wa kiti je, taarifa hii inajadiliwa? Kama inajadiliwa tuweze kupewa nafasi ya kuweza kujadili. Kwa sababu kuna vitu ambavyo vimetofautiana hapa, serikali imesema haiuzwi mpaka wakae washirika, lakini Naibu Waziri alipokuwa akizungumza alisema na *tender* ishatoka na kila kitu. Naomba Mheshimiwa utusaidie kiti chako.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe Mwakilishi wa Jimbo la Kitope niliposimama hapa nilisema kwamba ni taarifa ya serikali juu ya maswali na majibu yaliyotokezea siku ya Ijumaa, serikali imekuja kutoa maelezo ya ziada juu ya swali lililokuwa limeulizwa na Waheshimiwa Wajumbe, maswali aghalabu yake huwa hayaulizwi wala kuchangiwa, huu ni ufafanuzi zaidi juu ya maswali ambayo yalikuwa yameulizwa siku ya Ijumaa hakuna mjadala katika swali hili.

Naomba tuendelee na tumpishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati inayohusika aje kusoma taarifa. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kusoma hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio, Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, siha na nguvu zilizoweza kutufikisha hapa Barazani na tukaweza kufanya shughuli zetu kama tulivyopanga, hatuna budi kusema *Alhamdulillah*.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani zangu za dhati pia zije kwako wewe kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuwasilisha Hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambayo hivi punde Mhe. Waziri wa Elimu na mafunzo ya Amali amewasilisha mbele ya baraza lako hotuba ya wizara yake.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe.Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Ali Juma Shamuhuna, vile vile nimshukuru Mhe. Naibu

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Zahra Ali Hamad; Katibu Mkuu, manaibu wake, Afisa Mdhamini, Wakurugenzi pamoja na watendaji wengine wote kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati wakati wote tulipokuwa tukifanya kazi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, natumia fursa hii adhimu kuipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Fedha kwa kuamua kufanya mageuzi ya bajeti ikiwa ni sehemu ya mageuzi ya utawala na udhibiti wa fedha za umma.

Mhe. Mwenyekiti, sitakuwa nimetenda haki iwapo nitaendelea na hotuba hii bila ya kutoa shukurani za pekee kwa Wajumbe wa Kamati yangu, ambao tumeshirikiana kwa umoja wetu kuyapitia na kuyachambua makadirio haya ya bajeti, nawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kutambua mchango wao mkubwa kwenye Kamati hadi kufanikisha kazi hii, naomba sasa niwataje kwa majina wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hassan Hamad Omar	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Farida Amour Mohamed	Mjumbe
4.	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjuumbe
5.	Mhe. Abdi Mosi Kombo	Mjumbe
6.	Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
7.	Mhe. Mohamed Mbwana Hamad	Mjumbe

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kuwataja Makatibu wetu wa Kamati ambao huwa tunashirikiana nao katika kazi zetu na wamekuwa wakitusaidia kwa karibu katika kufanikisha kazi hizo.

1. Ndg.Asha Said Mohamed; na
2. Ndg Abubakar Mahmoud Iddi

Mhe. Mwenyekiti, naomba ieleweke kwamba, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha106 (e) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2012. Majukumu ya Kamati yameelezewa katika kanuni ya 112 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi ambapo miongoni mwa majukumu yake ya msingi ni pamoja na kuchambua mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi wangu huo, napenda sasa nitoe maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kama ifuatavyo**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipofanya uchambuzi wa bajeti kupitia wizara hii, imebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kutumia programu kuu sita (6) ambazo ni:

1. Programu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi
2. Programu ya Elimu ya Sekondari
3. Programu ya Elimu ya Juu
4. Programu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali
5. Programu ya Ubora wa Elimu; na
6. Programu ya Uongozi wa Elimu

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ina jukumu kubwa hasa katika lengo zima la maendeleo ya nchi yetu, kwani ndio wizara inayohusika na utoaji wa taaluma kwa wananchi wetu na hatimae kupata wataalamu, viongozi, wajasiriamali, wafanyabiashara na wengineo ambao ujuzi wao ni tunu kwa nchi yetu**.**

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza wizara hii kwa bidii wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yake ya kutuandalia wataalamu wa fani mbali mbali muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu, hasa ukizingatia tunaishi katika karne ya mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaamini kwamba malengo hayo yatafikiwa iwapo fedha kutoka serikalini zitapatikana kama zitakavyoidhinishwa na Wajumbe wako na kuingizwa kwa wakati.

PROGRAMU YA ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

Mhe. Mwenyekiti, ubora wa taifa lolote duniani, unajengeka kutokana na mfumo na ubora wa elimu wanayoipata wananchi wake. Hivyo na sisi Wajumbe wa Kamati hatuna budi kuunga mkono programu ndogo ya Elimu ya Maandalizi ambayo inahusiana na kuwahamasisha wazazi kuwaandikisha watoto wao katika skuli za maandalizi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na umasikini wetu, kuwekeza katika elimu ni jambo la busara kwani ndio njia pekee itakayotuwezesha kufika kule ambako tuna ndoto ya kufikia. Kamati imeridhishwa na kiwango cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kulipia gharama za chakula kwa skuli za maandalizi. Programu hii itasaidia

kuwahamasisha wazazi hasa wale wenye hali duni za kimaisha kuweza kuwapeleka watoto wao kupata elimu ya maandalizi, kwani kitendo hicho cha kupata chakula wakati wakiwa wapo skuli itapelekea watoto hao kupenda kwenda skuli.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipokuwa inafanya kazi zake za kawaida kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 imebaini kuwa licha ya wizara hii kuanzisha mtaala mpya wa elimu ya msingi lakini bado wizara haikufanya matayarisho ya kutosha katika kuwapatia vitabu vya kujisomea wanafunzi hao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile skuli za msingi ndio daraja la kufikia sekondari, wizara inapaswa kujipanga vizuri katika kiwango hiki cha elimu ya msingi, kwani wanafunzi walioandaliwa vizuri katika kiwango hicho ndio wanaofanya vizuri wanapofika katika kiwango cha sekondari.

Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo, kamati inaunga mkono mradi wa uimarishaji wa elimu ya msingi ambao unapatikana katika programu ya elimu ya maandalizi na msingi wenye lengo la kuchapicha vitabu vya wanafunzi wa darasa la tano na la sita. Katika kufikia lengo hilo, kamati inaitaka Wizara ya Fedha kuingizia wizara hii fedha zilizotengwa kwa mradi huo kwani vitabu ndio nyenzo kuu kwa mwanafunzi.

PROGRAMU YA ELIMU YA SEKONDARI

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipokuwa ikifanya kazi zake za kawaida katika wizara hii ilikutana na changamoto ya ukosefu wa vifaa vya maabara kwa baadhi ya skuli zilizopo Unguja na Pemba, hali inayopelekea wanafunzi wanaochukua masomo ya sayansi kushindwa kupata mafunzo ya vitendo katika masomo yao.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo kwani wanafunzi walio wengi wanaamini kuwa masomo ya sayansi ni magumu na yanahitaji zaidi mafunzo ya vitendo kuliko mafunzo ya nadharia. Hivyo kuwepo kwa vifaa vya maabara vitachangia sana katika mafanikio ya wanafunzi hao.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaunga mkono jitihada za wizara hii za kutatua changamoto ya vifaa hivyo vya maabara kupitia shughuli waliyojipangia ya ununuzi wa vifaa vya maabara kwa skuli 180 za sekondari Unguja na Pemba. Ni matarajio ya Kamati kuwa, mafanikio ya shughuli hiyo yatasaidia wanafunzi wetu kupata mazoezi ya vitendo na kuwajengea ufahamu zaidi wa masomo yao.

Mhe. Mwenyekiti, Elimu ya juu bado haijapewa kipaumbele kinachostahiki kwani mpaka sasa wanafunzi bado wanahangaika juu ya kupatiwa mikopo kwa ajili ya

kujiendeleza na masomo yao. Ni kweli kwamba kwa mujibu wa sheria ya Bodi kifungu nambari 20(2) kinamtaka muombaji ili apatiwe mkopo ni lazima awe ameomba fani iliyopewa kipaumbele na Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imebaini kuwa hata hao ambao wanavyo vigezo vya kupatiwa mkopo huo kisheria bado hawapatiwi mkopo kwa wakati, kwani kumejitokeza malalamiko kwa baadhi ya wanafunzi juu ya kadhia hiyo. Kamati inaiomba Serikali kuweka utaratibu mzuri ili kusaidia upatikanaji wa mkopo huo katika muda muafaka na kuepusha usumbufu wanaopata wanafunzi wetu hali inayoweza kupelekea kutofanya vizuri kwenye masomo yao.

PROGRAMU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Elimu ni sekta muhimu ambayo kuboreshwa kwa sekta hii kutapelekea mafanikio ya sekta nyenginezo. Kamati yetu imegundua changamoto nyingi katika Kituo cha Elimu Mbadala ikiwa pamoja na ukosefu wa walimu wa kudumu wa fani mbali mbali, ukosefu wa sehemu ya kufanyia kazi za vitendo na uhaba wa vifaa vya kufundishia.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono fungu hili lililotengwa kwa ajili ya kuendesha programu hii ya Elimu na mafunzo ya amali ila vipaumbele vya programu hii vielekezwe zaidi katika kutatua changamoto hizi ambazo Kamati imezibaini kuwa ndio kikwazo cha maendeleo ya kituo hicho.

PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kutaka kufufuliwa kwa michezo katika Sekta ya Elimu, na kwa umoja wetu tunalidhihirisha hili kwa kuunga mkono fedha zilizotengwa kwa ajili ya programu ndogo ya kuibua vipaji vya michezo kwa wanafunzi, kwani progamu hii itakuwa njia tosha ya kuwajengea uwezo wanafunzi wetu ambao wapo katika skuli mbalimbali Unguja na Pemba.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Elimu ni sekta muhimu ambayo kuboreshwa kwake kutapelekea mafanikio ya sekta nyenginezo. Kamati yetu imegundua bado kuna changamoto nyingi katika sekta hii ikiwemo kutopewa kipaumbele kwa watumishi wake na kuwepo kwa tatizo la malimbikizo ya maposho na mishahara ya walimu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sekta ya elimu bado haijapewa kipaumbele kwani walimu wetu walio wengi hawapatiwi maslahi mazuri, walimu wamekosa chombo

huru cha sheria ambacho kitaweza kusimamia maadili na taaluma zao. Mhe. Mwenyekiti , kutokana na hali hii, tunaiomba Serikali kuzitatua changamoto hizi zinazowakabili walimu ikiwemo kuwapandishia mishahara, kuwalipa maposho yao, na kuanzishwa kwa chombo huru kitakachosimamia maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ishalisemea sana tatizo la ukosefu wa hati miliki kwa majengo mengi ya skuli za Serikali lakini bado skuli nyingi zinamiliki ramani tu za majengo na kupelekea kuvamiwa na makaazi ya watu.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili linaendelea kuzusha migogoro mingi na kesi nyingi, hivyo tunaiomba Serikali isaidie upatikanaji wa hati miliki za majengo ya skuli ili kuepusha migogoro isiendelee kutokea, ni mategemeo yetu kuwa Serikali itawajibika katika kutoa muongozo huo haraka iwezekanavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaitaka Wizara ya Fedha kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya programu za Wizara, zinaingiziwa kama zitakavyoidhinishwa na Baraza hili katika katika kikao cha kupitisha bajeti ya mwaka huu wa fedha na zinapatikana zote kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba kuchukua nafasi hii adhimu kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamaii ya Baraza la Wawakilishi, aidha niwashukuru wajumbe wako kwa utulivu wao waliouonesha wakati nawasilisha hotuba hii**.**

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia juu ya mia. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nitoe neno moja tu katika mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapa kuna walimu waliorekebishiwa mishahara yao lakini zile *arrears* zao mpaka leo hawajalipwa. Hili ni jambo linawapelekea walimu wetu kupata usumbufu wa kutosha. Naiomba wizara na serikali yetu iwaonee fungu la hurama walimu.

Walimu ni walezi, walimu wanawafundisha watoto wetu lazima wapate utulivu katika kuwapatia haki zao, na mtu yeyote mwenye haki yake apatiwe, sisi kama Waheshimiwa kunyimwa haki yetu hatukubali na walimu wapewe haki zao Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe ni matarajio yetu kwamba wizara hii tutakuwa na wachangiaji wengi. Kwa hiyo, ningeliomba basi kila mchangiaji ajipange vizuri na baada ya dakika zile zetu za kawaida tujitahidi tutumie kwenye

dakika 15 ili kila mtu apate na hatimaye tuweze kufaidika sote na ujumbe uweze kufika kwa wale ambao tunawalenga.

Baada ya maelezo hayo sasa na wale wote ambao wanataka kuchangia walete huku maombi yao ili tuweze kuwajumlisha na tujue utaratibu wa kuweza kupangana tuweze kwenda vizuri.

Tukimaliza watu ambao tunao huku tutamuomba Mhe. Waziri aje kufanya majumuisho. Tunaanza na Mhe. Hija Hassan Hija, hayupo atachangia kwa maandishi, baadaye Mhe. Mohammedraza Hassanali na baadaye Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa pumzi sote sisi viumbe vyake, na mimi nachukua nafasi hii kukushukuru mpaka muda huu niliokuwa naringa na pumzi hizi ambazo Mwenyezi Mungu amenipa.

Mhe. Mwenyekiti, tumeisikiliza kwa usikivu mkubwa Bajeti hii ya wizara ambayo iliyosomwa na Mhe. Alhaji Ali Juma Shamuhuna pamoja na Mwenyekiti wa Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, labda niseme changamoto katika wizara hii nasema ni kubwa na inataka hekima, busara na usikivu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nishukuru kwa walimu wote ambao kubwa zaidi imekuwa inazungumzwa kwa usumbufu na matatizo yanayowakabili. Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa kuwepo kwangu na kuweza kusoma kama si walimu walioweza kunisomesha na nikafika kwenye Baraza hili Tukufu nisingeliweza kufika na kusema na kusoma.

Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kuwashukuru walimu wote walioweza kunisaidia kwa njia moja au nyengine tukiacha wazee, lakini walimu ndio waliweza kunifanikisha nisome moja na moja mbili, nisome vile vile *aliif*, *bee* na *tee*.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema Mwenyezi Mungu alivyomleta Mtume wetu (*SAW*) alimwabia "*Iqraa*" soma. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilichokuwa naomba Wizara ya Elimu kwamba mimi naamini kuna baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi hapa kaka yangu Mhe. Saleh Nassor Juma Mwakilishi wa Wawi, naamini yeye alikuwa mwalimu ndio tukamwita mwalimu na wengine walikuwa walimu humu.

Sasa nilikuwa nawakumbusha wenzangu mlioingia kwenye Baraza la Wawakilishi mkawa walimu na Mwenyezi Mungu akakufikisheni huku Mwenyezi Mungu akujaalieni lakini tusisahamu tulipotoka.

Mhe. Mwenyekiti, walimu hawa lazima tupate ufumbuzi wao, maisha yao yamekuwa magumu waliosimamia mitihani. Mimi jana nilikuwa na ziara ya maskuli mengi katika Jimbo langu Uzini, maana nimekuja hapa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini. Nilianza ziara yangu Pagali, Bambi, Kiboje na nilipokuwa nakutana na walimu hawa walikuwa wana masikitiko ya pesa zao kutolipwa waliosimamia mitihani na shughuli nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, kuna *problem,* na *we have to find the solution* na tunasema *what is next*. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeliomba huu ni mwezi wa Shaabani mwezi mtukufu sana kwa sisi. Duniani uzuri wa jambo lazima viongozi tuwe wakweli. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaji Dkt. Ali Mohamed Shein aliwaambiwa wasaidizi wake mawaziri wake msipokuwa na jawabu msiripuke rudini mkakae au mtoe kwa maandishi. Sasa mimi naomba sana wazee wangu, kaka zangu, katika vitu ambavyo ni vigumu kutovifanyia kazi ni uzuri wenzangu wakarudi kama maagizo ya Mhe. Rais ili wakaja na jibu ndilo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini uwezo tunao, nia tunayo na tunaweza kufanikisha kwa kushirikiana na sisi wadau pamoja na Rais wetu suala la walimu hawa likapata ufumbuzi. Mwalimu leo anaweza akatoka Kiboje Mhe. Mwenyekiti, yupo anakaa Mikunguni pesa zake za daladala za kupewa hazifiki, hapewi pesa zenyewe, mshahara wake mwalimu akipata mwisho wa mwezi sana atakwenda kununua sembe, mboga pamoja na daladala na watoto wake. Ni sawa sawa kama mimi ni posho yangu ya siku mbili tu sijui wenzangu kama mimi Raza.

Haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, halafu walimu wasipewe mafao yao, wasipewe *over time*, wakubwa wakisafiri mamilioni ya pesa, watu wanakaa kwenye *first class, business class* walimu wanakuwa katika hali ngumu wanaambiwa pesa hamna. Lakini panapotokea kiongozi anataka kusafiri atakwenda kwa Omar King pale, kwa Khamis Mussa, watakaa pale masaa kumi na nane ili wahakikishie tiketi ya kusafiri wanapata. Sasa Mheshimiwa *"hujafa hujaumbika"*, sisi tunaringa na pumzi za Mungu, na fimbo ya Mungu haina sauti.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, suala la hawa watu wetu wa kuweza kuwaisaidia mimi nasema litizamwe. Mimi naamini wizara ni sikivu, lakini tuwe wakweli twende kwa awamu tufahamu nini tunachokitaka. Mimi nafikiri Mhe. Rais ndio kiongozi, tuna Rais mmoja tu nchi hii kama jibu hakuna yule Rais yupo atakuwa

analo jibu. Mhe. Mwenyekiti, naona haya ni mambo ambayo tuipe kipaumbele kwa hawa walimu wetu wafanyakazi wetu.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia hapa Baraza la Wawakilishi Rais amefanya ziara kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, Rais alifanya zaira alikuja Pagali miaka mitatu iliyopita na akatoa ahadi, na ahadi hiyo imetolewa na Mhe. Waziri anayehusika katika Baraza hili la Wawakilishi kwamba kuna utaratibu mzuri wa serikali kupitia Wizara ya Elimu kwamba wanaambiwa wananchi pamoja na walimu waweze kujenga maskuli, suala la kuezeka Wizara wa Elimu itabeba, *of course* Mhe. Mwenyekiti ni jambo zuri, ni jambo zuri na hii nchi yetu pamoja tunatakiwa tuchangie .

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hili suala la Skuli ya Pagali limeahidiwa na Rais wa nchi miaka mitatu. Mhe. Mwenyekiti, baadae nitakuletea hizo picha niwasilishe tu kwako, miaka mitatu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, mpaka jana nakwenda Pagali hili jengo liko vile vile, sasa kama Mwakilishi ni dharau kubwa Rais wa nchi, banda moja na aliahidi kuezeka kaja akatoa ahadi Rais wa nchi. Sasa mtwambie kuna Marais watatu, wanne, kama ni Waziri ni Rais atwambie, lakini Rais wa nchi na mwaka jana mwaka juzi hapa tulizungumza hivi hakuna kilichotokea, hakuna kilichofanyika, hakuna *communication*, hakuna suala la kuitana.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunakuja humu sisi ikifika saa saba tunakimbilia kusali, lakini vitu hivi tunavitolea ahadi humu. Isitoshe hapa Mhe. Mwenyekiti, Skuli ya Kiboje mwaka jana ilipita kwa mbinde hapa, nakumbuka kaka yangu Mhe. Waziri wa Fedha Omar Yussuf Mzee alisimama kwa niaba ya Waziri wa Elimu akaahidi kwamba lile jambo litakwenda tena Skuli ya Kiboje nitakuletea nitawakilisha imeshaota mpaka magugu ndani hii jana nilikuwepo.

Skuli hii nilisema mwanzo jina la Skuli hili pale limeandikwa limefunguliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaji Dkt. Salmin Amour Juma Komandoo, alipokuwa Rais na nilisema huyu Rais Mstaafu na nilisema mwaka jana hapa jamani mkalitoe lile bango la Rais huyu bado Rais Mstaafu.

Mimi mbali na Mwenyezi Mungu sote wengine hapa kama sio Dkt. Salmin Amour wengine tusingelikuwa tunatajika hapa, sisi wengine Dkt. Salmin Amour ndiye aliyeweza kutuwezesha hapa mbali na Mwenyezi Mungu, hakuna kilichofanyika Mheshimiwa na nimeshawaambia wanafunzi bora ondokeni humu. Maana leo Mheshimiwa nina udhu, maana nilisema maneno mwaka jana kwa mwezi huu wa Shaaban sipendi kusema. Hii ndiyo hali na imetolewa ahadi na Serikali na tumekuwa hapa sote.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachoomba ile *communication*, hii ni nchi yetu sisi sote. Serikali imeshafanya mengi, imeshafanya mambo ya barabara, mambo ya nini. Lakini mimi Mhe. Mwenyekiti, sikutarajia bajeti hii iletwe leo. Maana yake nusu ya bajeti ya mwaka Mheshimiwa haikutekelezwa, leo tunaletewa bajeti nyengine humu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa nimekuja kwa niaba ya wananchi, na nimekuja kwa sababu ya matatizo ya wananchi. Sasa ni uzuri kama kuna uwezekano kitaratibu, unajua Mhe. Mwenyekiti, ushamba siyo kuzaliwa shamba, ushamba ni kutofahamu mambo. Kama inawezekana bajeti ile ya mwaka jana ikawa ndiyo ikamilishwe kuliko bajeti ya mwaka huu kwa sababu kuna vingi.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, tunajua hali yetu ngumu ya uchumi, hivi wananchi kuwaambia wananchi waendelee kujenga, halafu watakuja kuezeka na kuna miaka kumi, mimi ninaambiwa kuna miaka kumi majengo mengine bado hayajaezekwa, na kuna majengo mengine Rais hajamaliza. Jawabu tutakuja kuambiwa hapa tayari tunatafuta wafadhili waje wamalize, ni lini.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa nina sababu zangu, kwa sababu kesho munaweza kuniuliza, aah! wewe Mohammedraza na Skuli ya Kiboje, skuli ya nini, umeifanyia nini Wizara ya Elimu kama Mwakilishi, umeifanyia nini Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nimejenga madarasa mawili ya kisasa Skuli ya Pagali amekuja kufungua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akisaidiwa na Rais Mstaafu Mzee Ali Hassan Mwinyi, wakisaidiwa na mabalozi mbali mbali; Balozi wa Oman, Balozi wa India na kaseti ninayo. Maana uniulize nimefanya mimi katika kuisaidia Wizara ya Elimu. Isitoshe hapa nimekwenda kujenga madarasa mawili mapya. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, maana yake mimi nimekwenda siziki magofu, mimi ninaanzia Nyani. Kama kuna magofu ninawaambia kaeni pembeni nionesheni majani nianze hapa. Nimekwenda Miwani nimejenga madarasa mawili ya kisasa pamoja na vikalio, amekuja kufungua pale Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Alhajji Seif Ali Iddi. Isitoshe Mgenihaji walikuwa na upungufu wa madarasa na viti.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tano za ziada.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mgenihaji nimekwenda nimekabidhi viti ambavyo mgeni rasmi alikuwa ni Mama yetu Mama Shein; mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, isitoshe tarehe 14 *inshaallah* mwezi Juni, mwezi ishirini saba wa Shaaban tukiwa hai na uzima, ninawaalika Wawakilishi wote na wananchi wote wa Zanzibar, ninakwenda pale kufungua, nimejenga madarasa mawili ya kisasa kwenye Skuli ya Bambi pamoja na viti kwa ajili ya watoto wetu wa *Form IV* siku ya Jumapili. Kwa hivyo ninatoa mualiko wa nchi nzima pamoja na Wawakilishi; ninafungua Skuli ya Bambi pale pamoja na timu zote za Skuli za Bambi zilizokuwa Jimbo la Uzini kuvipatia vifaa vya michezo. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, isitoshe hapa ninakwenda kusaidia wale wazee kwa ajili ya Wizara ya Elimu, watoto wetu wanaosoma kwenye vyuo kwa sababu kutokana na hali yao. Juzi nimeletewa milioni kumi na tano kama Mwakilishi pesa za wananchi nitakwenda kuzikabidhi pale kwa Wadi tatu. Wadi ya Bambi, Uzini na Kiboje katika kuisaidia Wizara ya Elimu. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ninaposema Wizara ya Elimu ujue sasa kama Mohammedraza nimeanza kuisaidia, sitochoka na wala sitovunjika moyo, tutasaidia nchi yetu kadri ya uwezo tuliokuwa nao. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, katika kumalizia, mimi nataka ninawahakikishie Wizara ya Elimu kwa kuja kuwaambia nitazuia shilingi, hilo kwa mwezi huu wa Shaaban siyo. Lakini ninasema kwamba tukumbuke tu sisi tuliokuwa humu ndani kwamba kuna watu wetu kule hawana sauti na uwezo. Maana yake Mhe. Mwenyekiti, hii Kiboje mwaka jana alipooneshwa, Mwalimu Mkuu alipowapeleka jamaa wa *TV*, yule Mwalimu Mkuu kaondoshwa kule. Sasa mimi niliwachukua waandishi wa nchi nzima nilitegemea labda kuna mtu atanizuia pale, nitaendelea kuisaidia nchi yangu, nitaendelea kuitumikia nchi yangu, nitaendelea kuipenda nchi yangu ili tuweze kufika pahala tukasaidiana sote. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mategemeo yangu kwa Wizara hii na changamoto hii, kile tunachoweza kufanya tufanyeni, kile cha kuweza kusaidiana tusaidieni, kile cha kuweza kukaa kwa pamoja tukaeni kujenga mapinduzi yetu matukufu. Mapinduzi yetu matukufu ni kuwaletea wananchi maendeleo, maji, elimu, huduma mbali mbali, barabara, kilimo, uvuvi. Ndiyo maana ya mapinduzi yetu tukawa leo tunaringia humu ndani. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa haya machache. Mategemeo yangu kwamba siyo hapa, kuna sehemu nyengine tutaweza kufanikisha na ninaamini tutapata maelezo yenye hekma na busara. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mohammedraza. Sasa nafasi...

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha kwa heshima yako.

Mhe. Mwenyekiti: *Inshaallah* mpe Katibu hayo. Sasa nafasi tunampa Mhe. Fatma Mbarouk Said na baadaye Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuchangia machache katika Hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kwanza nichukue fursa hii kumshukuru yeye namna alivyowasilisha bajeti yake hii na Mwenyezi Mungu akampa nguvu ya kuisoma. Niseme kwamba ninamshukuru sana na niwashukuru watendaji wake wote akiwemo Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wake.

Mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri, juzi kajilabu na kanitia tumbo joto kumsifu mama nyumbani lakini mimi ndiye wa awali. Kwa hivyo, ninasema nimshukuru sana, mimi ndiye wa awali, mimi ndiye azizi(*Kicheko*)

Mhe. Mwenyekiti, juu ya pongezi zangu hizo niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 4 ambao una mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano cha 2010-2015.

Kwanza nimpongeze kwa hilo. Katika mambo ambayo yamefanikiwa ni ongezeko la uandikishaji wanafunzi, pia kwa kufunguliwa kwa Kampasi mpya ya Chuo Kikuu. Vile vile kuhamia huko Mchangamdogo, Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa baada ya kumalizika ujenzi huo na ile ile moja katika mafanikio waliyapata.

Mhe. Mwenyekiti, siku zote tunasema kwenye mafanikio na changamoto zinakuwepo, na nimeona changamoto nyingi humu na ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze ili niweze kufahamu.

Nimeona kwenye ukurasa wa 6 Mhe. Waziri amesema kwenye huu mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi, kwamba mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi bilioni moja na mia tatu milioni (1,300,000,000). Kati ya hizo milioni mia moja ni za Serikali na bilioni moja, milioni mia mbili ni za *GPE* na *UNESCO*, hadi mwezi wa Machi pesa zilizopatikana ni kidogo sana.

Kwa mujibu wa ripoti hii wanasema kwamba hizi za *GPE* hakuna fedha zilizopatikana, aah! kwenye pesa za Serikali hakuna pesa zilizopatikana. Nimuulize tu Mhe. Waziri ni kwa nini pesa hizo hazikupatikana na ikiwa kwamba

mradi huu umekubalika na ulikuwa uanze. Kwa nini hasa wafadhili pesa hizo hazikupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ripoti ya Mhe. Waziri nilivyoisoma ni kwamba kuna mafanikio mengi, lakini niseme tu kwamba bajeti zetu zinakuwa tegemezi. Tunaambiwa au kuna usemi wa Kiswahili unaosema kwamba, "*Mtumai cha ndugu hufa maskini*". Kwa hivyo ninaona ni namna gani pesa zilivyokuwa kwa namna tulivyojipanga kwamba tutatumia kiasi hichi, lakini baadae pesa hizo zikawa hazikupatikana.

Kwenye miradi hiyo hiyo ya elimu, kuna mradi huu wa Uimarishaji wa Elimu Msingi pia nimeona kasoro, kati ya pesa ambazo zilitakiwa hapa za wafadhili bilioni kumi na mbili, mia tatu na sitini na mbili. Kati ya pesa hizo SMZ zilikuwa bilioni moja lakini pia pesa hizo kulikuwa na kasoro, karibuni nikaona hizo pesa za wafadhili zilizopatikana ni milioni mia saba na sabini na nane katika hizo milioni kumi na moja. Kwa kweli hili ni tatizo, na ningeiomba sana Serikali bora tutafute pesa na baadaye tuweze kuanzisha ile miradi, kwa sababu naona hili ni changamoto kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona ndiyo yale kwa yale yanajirudia, kila penye mradi basi ninaona kasoro inakuwa ni kubwa sana kabisa. Kwa sababu hata kwenye huu mradi mwengine ambao mradi wa Uimarishaji Elimu Mbadala na Amali.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kasema kwamba kwa mwaka 2014/2015, mradi ulitengewa jumla ya shilingi bilioni saba, milioni mia tano na sabini na tisa, mia tatu na kumi na tano, mia nane na sabini. Kati ya hizo shilingi milioni mia saba za SMZ na bilioni sita, laki nane sabini na tisa kutoka kwa Benki ya Maendeleo ya *AfDB*. Hadi kufikia mwezi wa Mei zimepatikana Tanzania shilingi bilioni sabini za SMZ na ni sawa na asilimia 10.1 ya makadirio na bilioni mia mbili, tisini na tisa sawa na asilimia 4.4 kutoka kwa *AfDB* zilipatikana.

Utekelezaji wa malengo ilikuwa kama ifuatavyo. Kwa kweli nazo pia pesa hizo inaonekana asilimia 85.95 hazikupatikana. Ndiyo ninashauri hivyo kwamba lazima tubadilike ili miradi hii basi kwanza tuwe na kazi ya kutafuta zile fedha zenyewe na halafu ndiyo tuanzishe mradi.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda ukurasa wa 10, vile vile kuna mradi wa ujenzi wa Vyuo vya Kiislamu. Mhe. Waziri amesema hapa mradi unatekelezwa kwa kushirikiana na Serikali ya Falme ya Oman wenye lengo la kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Utamaduni wa Kiislamu kwenye eneo la Chuo cha Kiislamu. Sasa hapa nimuulize Mhe. Waziri kwamba hivi Vyuo ni vingapi ambavyo vinataka kuwepo

kwenye huo mradi, kwa sababu hapa kasema vyuo. Halafu vile vile mradi huu ulipangiwa kiasi gani kwa sababu hapa Mhe. Waziri hajatwambia.

Mhe. Mwenyekiti, halafu vile vile nikienda mbele zaidi kwenye ukurasa wa 25, kuna Elimu Mbadala. Hapa Mhe. Waziri vile vile ametwambia Elimu Mbadala inalenga kuwapatia elimu vijana wenye umri kati ya miaka 10 mpaka 15.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona bado hapa hawa vijana ichukuliwe juhudi ya makusudi ili kuwapatia ile elimu ya lazima, kwa sababu bado hawa watoto ni wachanga, mtoto kutoka miaka 10 mpaka 15, wakaingia kwenye Elimu Mbadala. Kwa hivyo hili ni tatizo, ni lazima tufanye juhudi ya makusudi ili tuwasaidie hawa watoto warudi wapate ile elimu ya lazima.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda ukurasa wa 30, hapa Mhe. Waziri amesema kwamba kuna Idara ya Michezo na akasema kwamba hii Idara ni mpya. Ninataka nimuulize hii ni Idara au Kitengo cha Michezo kupitia Wizara ile, kwa sababu ninajua Idara ya Michezo si mpya ipo zamani. Mimi nilianzia kufanya kazi tokea mwaka 1980 ipo au iwe ni Kitengo, kwa sababu Idara bila shaka kuna sheria ya uanzishwaji wake, halafu kama ni Idara basi aniambie Mkurugenzi wake ni nani. Kwa sababu hii ndiyo yale mambo ambayo tunatafuta pesa lakini sasa pesa zenyewe, kwa kweli tunajilimbikizia mambo ambayo hayana hata umuhimu sana. Kwa sababu ni muhimu michezo, lakini si kuna Idara maalum, sasa tukisema na ndani ya Wizara ya Elimu muna Idara ya Michezo na bila shaka kutakuwa na Mkurugenzi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilitaka kujua au pengine ni makoseo tu. Kwa hivyo Mhe. Waziri akija aniambie hii Idara ni Idara kamili au ni Kitengo tu.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda kwa...

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano za ziada Mheshimiwa.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Bee!

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano za ziada.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Haya ninazifanyia kazi hivyo hivyo.

Halafu Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu hapa nimeona, kuna mambo vile vile kwamba nisome kidogo ili niweze kujua nini kimekusudiwa.

Katika mwaka 2014/2015 Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu ilitekeleza majukumu yake kwa kuzifanyia ukaguzi skuli 376. Skuli 286 za Serikali na 90 skuli za binafsi. Na kupitia ripoti ya ukaguzi iliyofanywa na walimu wakuu miongoni mwa

yaliyojitokeza katika ukaguzi huo ni baadhi ya walimu wakuu kwa kushirikiana na walimu wao, wanasimamia vyema upatikanaji na utoaji wa elimu bora katika skuli zao kwa kiwango cha kuridhisha.

Hata hivyo, ilijitokeza kwamba baadhi ya walimu wakuu wanakabiliwa na changamoto nyingi za kiutendaji, zikiwemo uhaba wa walimu wa sayansi na hesabati, hali iliyopelekea walimu wa sanaa kukosekana kusomesha masomo hayo. Nilitaka kumuuliza Mhe. Waziri sanaa gani hiyo. Maana yake kama ni sanaa, walimu wa sanaa fani yao labda inawaruhusu kufundisha. Hawa siyo ndiyo walimu wenyewe.

Kwa hivyo kwanza anifafanulie Mhe. Waziri atakapokuja ni sanaa gani ya hawa walimu na kama fani ya sanaa, maana yake sanaa kuna sanaa nyingi za maonesho, zipo aina nyingi za sanaa, michezo pia ni sanaa. Kwa hivyo aniambie ni sanaa gani hii ambayo walimu hawa wanayo.

Kwa kweli changamoto zipo lakini nishukuru kwamba safari hii mambo mengi ya kibajeti hizi, bajeti ni kupitia mfumo wa programu. Na tatizo lipo mpaka sasa hivi lipo ni lile tatizo la kuwategemea wahisani, na tumeona kwenye semina kwamba tumeiona kwamba hii ni moja ya tatizo kuwa hawa wahisani wameshindwa kutimiza yale malengo ambayo ya kibajeti na hili ni tatizo la kibajeti.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niseme na mimi kwa sababu bajeti hii imekuja na wakati muafaka na ni lazima tuzipitishe, lakini yale Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali alikwishasema, basi kama kuna mapungufu ambayo yalijitokeza kwa mwaka uliopita, basi ni vizuri tukaona tusianzishe miradi mengine isipokuwa ile ile iendelee.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono bajeti hii. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwakilishi. Sasa nafasi tunampa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, baadaye Mhe. Mohammed Haji Khalid ajiweke tayari akifuatiwa na Mhe. Marina Joel Thomas.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda unatupa kidogo kidogo, basi na sisi itabidi leo tuwe na zamu ya kusifu tu wizara, kwa sababu hii ni siku ya bajeti, kwa hivyo angalau utupe dakika 40, ukosefu wake dakika 50.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwenye kitabu hiki sitokuwa na hoja nyingi. Niseme ukweli Mhe. Mwenyekiti, nitoe pongezi kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti hii wizara ni kubwa, lakini pamoja na ukubwa wake, ukipita pembeni unakuta Wizara ya

Elimu na Mafunzo ya Amali imejenga jengo jipya. Ukiingia katikati utakuta Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imejenga jengo jipya. Kwa kweli nataka kusema wamezitumia vizuri sana pesa za wafadhili tena nawapongeza sana tena sana.

Mhe. Mwenyekiti, wanajisikia raha sana, kila nikitembea nikianzia katikati Dole pale nakuta jengo zuri, nikienda upande wa Chwaka nakuta jengo zuri. Nikienda Kaskazini ndio nyumba, *Wallahi* Mheshimiwa sina cha kuwapa, lakini Mwenyezi Mungu ndiye atakayewapa. Mwenyezi Mungu hana khiyana kutoa sadaka kwa watendaji wazuri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mimi nianzie kwa Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wake. Mhe. Mwenyekiti, kama Rais ana vyeo vyengine, au kuna nishani ya kuwapa, basi moja ni katika wizara hii, kwa kweli wamejitahidi sana kutujengea vyuo vingi sana. Toka hapo nje tu nenda Mazizini, juzi tu jengo kubwa sana pale liko karibu na Kituo cha Polisi cha Kiembesamaki zuri sana, ni wao hakuna watu wengine. Usimamizi bora siku zote ndio unaoleta tija, kukiwa na usimamizi mbaya hakuna tija. Sidhani kama leo wanafunzi watasema kama Zanzibar hatusomi, hilo mimi nitalikataa. Neno la kusema kuwa hatusomi kwa kuwa hatuna vyuo, mimi mtu huyo nitampiga kibao, kwa sababu nitasema hatutakii mema kwa vyuo vilivyokuwa vimeenea hapa *Alhamdulillah*.

Mhe. Mwenyekiti, ni lazima nisifu kwa sababu *support* kubwa wametupa kwenye majimbo, wamejitahidi sana kwenye majimbo yetu. Mhe. Mwenyekiti, Mjumbe mwenzangu aliyeondoka alisema amejenga madarasa mawili katika eneo lake. Mimi nashindwa hata kuhesabu kwa jinsi walivyotusaidia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Wamewekeza sana katika Jimbo letu, huo ni ukweli usiofichika, ni lazima mtu useme ukweli ulivyo. Nitakuwa mimi sipendezi kwa wizara kama sikuwaambia ukweli wa kuwasifu kutokana na matendo waliyokuwa wakitutendea. Sifa yao moja kubwa, unapoanzia wewe basi wao wanakuja kumaliza. Sasa hiyo peke yake ni neema. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sitoona aibu wala sitoona tatizo kusema na kuonesha maeneo waliyotusaidia wizara hii, ili na Waheshimiwa wengine washawishike na wao watengeneze mustakabali kama huu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhimiza kusoma skuli sio lazima uwe na taaluma. Hili nimeligundua, nimefanya *evaluation* kubwa sana na ukiangalia kwenye maeneo wale waliosoma utakuta ni skuli chache, kama uongo nendeni katumeni wataalamu tufanye *evaluation* ya hali halisi ilivyo. Lakini kule kulikokuwa na watu kidogo hawana taaluma, nendeni kaangalieni ndio skuli ziko nyingi sana, na hata mzazi

anapozaa anakuwa hana elimu lakini wanawe wanakuwa na elimu, hiyo ni moja ya raha iliyokuwepo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wametusaidia sana kwenye majimbo yetu, wametumia ipasavyo katika miradi ya wafadhili ili na sisi kuitumia, hilo nawapa asilimia 100 kutokana na yale niliyoyaona.

Mhe Mwenyekiti, kuna mambo madogo madogo ambayo mnaweza kutusaidia, bado utamu mlionionjesha na asali ile *pure* kabisa. Maana yake kuna asali ya aina mbili; kuna asali ile ya kwenye mjiti na kuna asali ya kwenye pango. Nyinyi mmenipa asali ya pango, kwa sababu ni tamu zaidi, nzuri zaidi na ndio inayotoa tiba, pamoja na ile ya nyuki wadogo wadogo ndio walionipa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Lazima Mwenyekiti, unitizame vizuri sana, maana yake ukweli tuuseme hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, tumejiandaa tena na tunataka kupiga hodi tena kwako, kutokana na ule ujabari wenu na kujali wananchi waliokuwa wana maisha duni katika maeneo na kujali nguvu zao. Sasa hivi Mgambo pale tumeshajenga skuli, bado mtumalizie mabati tu na kutupigia plasta. Najua hili suala nikiondoka hapa kesho tayari mafundi wanaletwa. Nishukuru sana kwa hilo mmeliona.

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru sana tena hongereni kwa kutujengea skuli Kirombero *Alhamdulillah*, skuli ile ilikuwa watoto wanashindwa kusoma baada ya kuona nyufa za kuwa wakati wowote inaweza ikapasuka skuli hii, mheshimiwa tunawashukuru sana. Hapa sasa tunawaombeni mtuongezee walimu, ombi letu ni kwamba walimu wa skuli ya Kirombero tunaomba mtuongezee ili wazidi kuendana na lile jengo mtakalotumalizia keshokutwa.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana watu wa Kombaurembo katika skuli yao kwa jitihada zao na kwa kupitia kwenye kamati yao, wamefika pahala mpaka wamepata nyumba ya walimu kwa kuomba misaada midogo midogo. Mhe. Waziri mnaweza mkatusaidia rangi, sio vibaya hiyo rangi hata nikitoka hapa Katibu Mkuu atatoa amri yapelekwe makopo manne tu wala sio mengi sana, kutokana na kuwa mnathamini nyinyi michango ya Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri Kombaurembo pale inangojea walimu waingie ndani, kwa sababu tunawasaidieni walimu wanakaa mbali na tunataka elimu ifike kwa wakati. Sasa tunaomba sana msaada huo, skuli yetu iko nzuri wananchi wamejitahidi kwa kupitia Kamati yao ya Maendeleo jitihada zote ziende pale kwa mwenyewe Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo pamoja na Katibu wake kwa kufikisha lengo hilo, na walimu wa pale nawashukuru sana kwa jitihada zao za kutafuta nguvu za huku na kule. Maana yake mwisho wanatoa mishahara

yao kwa kuchangia na wao. Mhe. Waziri naomba sana hilo kuwa kopo zetu wala sio nyingi, ni kopo nne tu tunaomba za rangi ili walimu waweze kulala katika nyumba nzuri. Mhe. Mwenyekiti, ni nyumba nzuri sana ile waliyojenga wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe ushauri wangu mzuri sana, ushauri huo utatusaidia. Mhe. Mwenyekiti, ni wajumbe wengi sana wamelia kilio cha walimu. Mimi leo nasema kwa masikitiko sana walimu tuwasaidie, Mheshimiwa tusione tabu kuwatafutia walimu mikopo. Sio vibaya mkaweka kumbukumbu mkiondoka pale ikawa kila mwalimu akawa na uwezo wa kukopa gari, hili ni suala kubwa sana na mtawasaidia katika nyenzo. Kwa sababu siku hizi gari ziko bei rahisi sana, watu wako wanaweza kuwakopesha. Mimi sipendelei mwalimu kuendesha vespa, kusema ukweli inasikitisha sana, kwa sababu imetiwa jina baya vespa sasa hivi. Mtu mzima ukipanda vespa unaambiwa, wanaitwaje wale, hilo jina naona tabu kulitaja. *ATM* sijui nani *ATM*, wanaitwa *"tako moja"* wale.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sipendi kumuona mwalimu wangu anakwenda kutoa taaluma ambapo taaluma ile yule anayekwenda kumpa baadaye akawa Rais au baadaye akawa Mwakilishi, halafu leo anapanda vespa. Mhe. Mwenyekiti, haistahiki, naomba sana Mhe. Waziri wapeni ruhusa, gari hapa Zanzibar sasa hivi ni rahisi milioni 3, 4 au milioni 5. Mhe. Mwenyekiti, naomba. Sasa hawa tukiwajenga, kwa sababu unapotaka kumsomesha mtu kwanza jiangalie wewe *refresh* yako, afya yako, bodi yako, uwezo wako na kila kitu chako.

Mhe. Mwenyekiti, mwalimu anapoondoka nyumbani anaanza kusikitika mimi kumbe bizari sijaacha, sijafanya nini. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, yule anayekwenda kumpa elimu basi haitomfika vizuri. Kwa hivyo, mimi naomba sana tuwajengee uwezo, na hili jambo sio baya, lazima serikali ikusaidie Mhe. Waziri kutokana na hali ya bajeti. Nimeona kuna *SACCOS* humu, na *SACCOS* hiyo zimeingiliana na mambo ya mabenki. Hiyo nashukuru, wapeni fursa tena kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, na haya mambo ya *arrears*, waliokuwa hawajapata *arrears* wapiganieni jamani wapewe zile *arrears* zao ili waweze kufanikisha suala zuri kwa walimu kuweza kuwasaidia watoto wetu katika kuwasomesha.

Mhe. Mwenyekiti, walimu ni watu watiifu sana, mimi leo nisingefika hapa kama sikuwa na mwalimu. Mwalimu wangu leo anajisifia kabisa, anajisikia raha kabisa. Lakini mimi cha kumpa sina, ndio leo namtetea hapa tu ili mafao yake aweze kufanikiwa kuyapata kwa wakati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sio vibaya hata walimu wetu mkawatafutia nyumba nafuu, mkaweka mradi maalum wa kuwatafutia vijumba nafuu. Mhe. Mwenyekiti, hii

ndio *system* wanayokwenda nayo wenzetu huko nje na mnatembea huko nje mnaona hali halisi. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli walimu sio watu wa kuchezea, ni watu wa kuhifadhiwa.

Mhe. Mwenyekiti, siku hizi walimu ukifanya *population* kubwa wanakuja kwenye Uwakilishi, wanatuingilia huku bure maskini ya Mungu, wanaacha taaluma kwa sababu gani, wanaona huku kuna hela, hebu wajengeeni katika mustakabali mzuri, wanakwenda sehemu nyengine wanakimbia. Kwa sababu hatujauangalia muhimili huu kutokana na umuhimu wake, *Wallahi* Mhe. Mwenyekiti inasikitisha sana. Siwalaumu kwenda katika nyanja nyengine, lakini nitalaumu kwa sababu wakiondoka wao inaondoka elimu hiyo. Kwa hivyo, nini cha kuwazuia ni mambo haya niliyoyataja hapa, ni mambo mazuri ya kuweza kuwazuia wao, ili na wao wajisikie.

Mhe. Mwenyekiti, utawakuta sehemu nyengine wanapata hela nyingi sana, Mahakama wanapata fedha nyingi, anaona yule wa Mahakamani ndio kamsomesha yeye, hivyo hichi ni kitu cha maajabu makubwa sana.

Mimi naomba Mhe. Rais anisikie kabisa kilio hiki kwa wizara hii. Namuomba sana Mhe. Rais atenge fungu maalum la kuwasaidia walimu. Walimu sijui sifa zao nizipeleke vipi hata ziwe zina kasoro, sio masihara Mheshimiwa. Ukiwaangalia wametusomesha. Naamini Mhe. Waziri kasomeshwa na mwalimu, Mhe. Naibu Waziri kasomeshwa na walimu, Katibu Mkuu kasomeshwa na walimu, Naibu Katibu Mkuu kasomeshwa na walimu, Wakurugenzi na kadhalika. Naomba sana bajeti hii tutenge. Haidhuru tuna programu ndogo ndogo na kubwa humu na ndio mfumo wa sasa hivi tunaokwenda nao. Lakini programu hizi sijaona, ndio maana nikasema tufanye fungu maalum tutumie taaluma zote, tuna uwezo huo ili tuweze kutafuta fungu linaloweza angalau tukaliita fungu la kujikimu, wakaweza kujikimu. Naomba sana.

Mhe. Mwenyekiti, ninawapenda sana walimu na ndio walionipa jeuri ya kusema hapa. Kwa hivyo, ni haki yao, inawastahiki na tuilinde. Kila Mhe. Mjumbe namuomba hapa, kama hakumsifu mwalimu basi tayari ana *weakness*, ana matatizo ya *brain*, anakuwa na matatizo ya akili. Huwezi kusema neno usimsifu mwalimu, hakuna hiyo. Wewe huyu ndiye aliyekuonesha jua la asubuhi, yeye mwalimu, halafu leo kwa nini usimsifu, usimtetee nitashangaa sana hapa kwenye Baraza hili. Uliingiaje humu kama huna taaluma kama sio mwalimu.

Mhe. Mwenyekiti, tuwe *serious* sana na hawa walimu, sio kitu cha mchezo, ni watu wa kudakwa dakwa, maana yake wa kuchukuliwa, wa kuondoshwa. Sayansi hapa Zanzibar inapungua kutokana na mwalimu wa sayansi utamuwekaje hapa, wakati unampa mshahara shilingi 200,000, posho lenyewe la mwezi mmoja kwa

mara tatu. Maana yake anapata mwezi mmoja akae kwa siku tatu tena mwezi mwengine ndio apate posho, kwa nini leo tusimpigie debe hapa. Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tuwapigie debe walimu wetu, na hii iwe ni nyimbo kwa kumalizia bajeti hii.

Tusiisakame hii bajeti imekwisha. Wewe unakwenda kumsakama mwalimu wako aibu, mwalimu yumo humu humu, hii bajeti haitakiwi kutiwa kasoro hata kidogo, sababu huyo aliyekusomesha wewe yumo humu kwenye kitabu, isipokuwa tumjengee mazingira kwenye bajeti hii huyu mwalimu.

Mimi nitaona ajabu Mjumbe leo akipiga buti au akizuia shilingi hapa, mimi nitacheka, unampigia buti mwalimu wako ni kuvunja heshima, ndio mwalimu wako unakwenda kumpigia buti. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitashangaa mtakuwa ni watu wa maajabu, itanibidi huyo mtu kama yuko karibu nimpeleke kidogo akatizamwe akili imetulia.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, unaanza kunipigia na wewe unataka mwalimu nisimsifu hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Nakuongeza dakika tano kwa ajili ya kuwasifu sana walimu, endelea.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniongeza dakika tano, lakini unipe na dakika tano kwa kumuenzi huyu mwalimu wako. Anakusikia mwalimu wako huko, anasema huyo sasa anamzuia Mhe. Makame Mshimba sasa asiendelee kututetea, anakusikia huko, kweli Mheshimiwa, kwa sababu hapa mimi sioni humu, mambo yote waliyotufanyia *Alhamdulillah*.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikawaambieni kwenye maeneo yetu aliyekuwa hakwenda kujitahidi hiyo ni kasoro yake mwenyewe, sio kasoro za hawa. Lakini waliojitokeza wamefanya na wamefanya nawaambieni. Waende watu Jimbo la Kitope wakaangalie *Alhamdulillah*, nendeni kila kona unakopita skuli nani kaisaidia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Skuli wamejenga wananchi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wamemaliza *finishing* yake, sehemu zake utakuja katika Jimbo la Kitope wao ndio mkono wao mrefu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwenye suala la michezo. *Wallahi* nimefurahi sana Mhe. Rais kupita. Kwa sababu mimi ni Rais wa Riadha Zanzibar, sasa haya mambo ni lazima nikubaliane nayo. Juzi tu walifanya *cross country* hapa kwa mashirikiano na ile taasisi yangu. *Wallahi* Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tukijisikia raha. Ndio maana nikasema kwamba itakuwa aibu sisi leo kitabu hiki tukakitoa kasoro. Wale wote waliokuwa *internationally* wachezaji mpira, watu wa riadha,

handball, basketball, kuogelea wametokana na kitabu hiki. Halafu leo unakuja kusema nini ndani yake. Kwa hivyo, mimi nawashukuru sana kuwa wameturejeshea.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa mchezaji mzuri sana wakati huo wa Skuli ya Jang'ombe na Kidongo Chekundu mimi, naam. Nilikuwa sijui kuuchezea mpira, lakini nilifundishwa na walimu wangu. Nilifika katika timu mbili za juu juu, sema sikuwa na uwezo wa kuchaguliwa kwenye timu ya Taifa. Ukija katika mambo ya *handball*, Mheshimiwa nilikuwa siujui mpira, *basketball* nilikuwa siujui mpira, lakini tumeanzia huko chini skuli.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana, lakini hili fungu nasema ni dogo sana, 200 haisaidii kitu hii, kama kweli tunataka kuamua sasa hivi basi tuviibue vipaji vyetu. Zanzibar nataka niwaambieni kwa asilimia 100 kuna vipaji vizuri sana, sio wakimbiaji, sio wachezaji mpira lakini mazingira yanakosekana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri tuwekee viwanja, tafuta kiwanja kimoja tujengee viwanja maalum kwa mambo yetu ya skuli, naomba huo ni ushauri wangu. Maeneo bado yapo tujengewe kinachohusiana na mambo ya michezo ya skuli tu, mwambie Mhe. Rais akusaidie hilo eneo akupe, haraka sana Mheshimiwa.

Wakati leo tumeshaamua humu sasa tujimalize kwa kwenda kutafuta *ground*. Ndio nchi za wenzetu wanakwenda hivyo hivyo mheshimiwa, itaweka jina la wizara hii kabisa. Wekeni jina la *ground* hii ambayo mtakayoipata upya kabisa, sio tatizo wafadhili, wafadhili wapo na nyinyi wafadhili mnao wanaweza kukusaidieni kutokana na hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nishukuru sana, lakini niseme kuwa bado fedha hii ya michezo ni fungu dogo sana na inasikitisha sana. Mhe. Mwenyekiti, nimalizie naunga mkono leo kwa aina yake. Ngojeni niwaungie mkono kwa aina yake. Wajumbe siku zote wanasema kwa asilimia 100, kwa asilimia mia kwa kuwa ndio kiwango mlichoona. Lakini mimi natoa kiwango changu, naiunga mkono kwa asilimia 150. *(Makofi)*

Sasa leo aje Mjumbe, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, aje Mhe. Mjumbe anipite, nitajua kama kweli Wajumbe wamefahamu nini maana ya elimu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Mhe. Mshimba leo tumemuongeza dakika tano, kwa sababu aghalabu yake anakuwa ni Mjumbe wa kwanza. Sasa leo katanguliwa na Mhe. Mohammedraza Hassanali.

Sasa tutamkaribisha Mhe. Mohammed Haji Khalid, na baadaye Mhe. Marina Joel Thomas na Mhe. Mohammed Mbwana Hamad ajiweke tayari.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata nafasi ya kuchangia machache kuhusu Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Nianze Mhe. Mwenyekiti, kwa kusema kuwa unatubinya sana katika hii michango, kwa sababu umezipunguza dakika zetu karibu kumi, kwa wale wenye uwezo wa kuchangia, ningekuomba ulione Baraza lilivyo na muda unaotoa kuna uwezekano bajeti hii ikapita asubuhi hii.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hayo nishukuru sana kabisa kabisa Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri uliokuwa na fasaha na ufanisi wa hali ya juu, lugha yake ni kama lugha yangu ya pole pole iliyofanya kila mmoja amfahamu vizuri na aliyekuwa hakumfahamu Mhe. Ali Juma Shamhuna hatomfahamu Waziri mwengine yoyote. Kwa hivyo basi ningeliwaomba Waziri wengine waliobakia waige mfano wa Mhe. Ali Juma Shamhuna Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.*(Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mbali na kumsifu yeye na pongezi kwa watendaji wake wote wa Wizara sitaki nimtaje mmoja mmoja wote kwa ujumla wao kwa kumsaidia Waziri katika kazi zake mbali mbali na hadi leo kufikia kutoa kitabu hichi kizuri cha bajeti yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na mradi mmoja tu mdogo mradi wa uimarishaji wa elimu ya ufundi, mradi huu ulitengewa fedha kidogo, kwa ajili ya bweni la wanaume wa Skuli ya ufundi Kengeja na miundombinu ya umeme na mambo mengine katika Chuo cha Karume. Lakini fedha zote zilizotengwa hakuna hata shilingi iliyoingizwa katika mradi huu sijui kwa nini ikawa mradi kama huu ikawa haukuingizwa fedha katika skuli hizi za ufundi.

Mhe. Mwenyekiti, ile skuli ya ufundi ya Kengeja baadhi ya wanafunzi wanalala msikitini, leo mradi ulichangiwa fedha lawama si Wizara ya Elimu kwa sababu Wizara ya Elimu au Wizara zote wanangojewa kuingiziwa lawama za waingizaji wa fedha. Wizara hii haistahili kunyimwa maombi yao, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti elimu ni ufunguo wa maisha. Elimu ndio iliyoleta mwanga ya watu tufanye nini na bila ya elimu itakuwa hakuna maendeleo.

Kwa hivyo ili tuendelee elimu lazima ipewe kipaumbele kinachostahiki, na ili mwanafunzi asome vyema yule aliyeko dakhalia apate mahali pazuri pa kusomea, apate pahala pazuri pa kupumzika na apate mahala pazuri pa kulala. Ningependa watoto wetu wapate malezi mema ya kielimu kama nilivyopata mimi nilipokwenda

Sekondari sikuambiwa niende na ndoo, sikuambiwa niende na chandarua, wala sikuambiwa nitoe ada yoyote.

Siku ya mwanzo niliporipoti niliambiwa chandarua hicho chukua, sahani hiyo chukua, betishiti hilo chukua, sabuni hiyo ya mche ya kufulia chukua, *life boy* ya kuogea chukua. Ningependa na watoto wetu hali hii iwarudie ili waweze kusoma vizuri, sio wapelekwe mbanjo watoto walivyofaulu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na hii elimu ya maandalii hii ni elimu muhimu sana ya kumtayarisha mtoto akiwa ni mdogo ili hatimae aingie katika elimu ya msingi ikiwa angalau kapata mwelekeo wa kielimu, lakini pia kwa sababu ni elimu ya maandalizi panatakiwa hawa waangalizi na wao wawe na taaluma ya hayo maandalizi yenyewe. Mhe. Mwenyekiti badhi ya skuli za watu binafsi za maandalizi walimu wao hawana mafunzo ya ualimu kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ningeiomba Wizara ya Elimu kile chuo cha walimu ambacho kilikuwa kinatoa elimu ya vyeti, elimu ile irejeshwe, walimu wa vyeti warejeshwe ili wafundishwe wawe walimu wa shule za maandalizi na hata za msingi. Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mwalimu wa cheti tu ilikuwa nimefundisha watoto *foundation* ni majaji, nimefundisha wanafunzi sasa hivi wengine ni ma- *engineer.*

Kwa hivyo msione kuwa mwalimu wa cheti kuwa hana thamani, si kila mtu lazima awe na shahada au stashahada na hii elimu ya chetu au mafunzo ya cheti naomba yarejeshwe kwa ajili kuwapa taaluma hawa walimu ambao wanafundisha katika hizi skuli za maandalizi. Mhe. Mwenyekiti, mwaka huu wanafunzi wa darasa la sita na saba watafanya mtihani wa taifa kwa kungia darasa la tisa, idadi hii ya wanafunzi ni kubwa mno kubwa kweli kweli, skuli kadhaa zina madarasa ya sabaa yanayozidi matatu na hivyo hivyo la sita yako hivyo hivyo, kwa hivyo idadi ya wanafunzi watakaoingia darasa la tisa mwaka ujao ni wengi mno.

Sina hakika kama Wizara ya elimu imejipanga kuweza kuwahudumia hawa kwa kila kitu pamoja na kuwa ada zote zimeondolewa, lakini sijiu nani anayezirudisha, kwa sababu tangazo la Shehe Karume hakuna aliyelifanya vyengine mpaka leo tukatangaza kuwa imerudishwa upya.

Kwa vyovyote sina hakika na siamini kuwa Serikali ina uwezo wa hivyo ilivyosema, sina hakika na siamini kuwa mna uwezo huo mtafanya watoto waende skuli hawana mabuku, mtafanya watoto skuli wawe hawaandiki mwaka mpya unaanza kesho huu unamaliza. Mmejipanga vipi hata mkasema hivyo, kitabu sio kinachotekeleza mnaotekeleza ni nyinyi. Mnataka kutupa mzigo mwengine mpya, mlivyotangaza hamna uwezo navyo mmesema tu kiutashi, hama uwezo.

Hivi sasa ni kiasi gani cha mabuku mmeshaagizia kwa sababu keshokutwa mwaka tayari unaanza, ni maboksi mangapi ya chaki na kadhalika, mmefanya nini, wanafunzi watakwenda skuli wazee tumeshawaambia na mimi ni mzee zaidi ya shilingi mia mbili ya kutumia skuli, simpi chengine siko tayari kunambia kuwa sina buku Serikali imeshatoa wenyewe. Baba mchango wa chaki, Serikali imejipanga wenyewe. Je ni kweli Serikali na Wizara ya elimu mnayamudu haya mliyosema.

Ningeomba Mheshimiwa katika majumuisho tuendelee kuwatoa wasi wasi wazazi juu ya suala hili. Nimesema hatujiwezi, kwa sababu haya madogo hatuyatekeleza. Je, hili ambalo ni kubwa sana, si kama vile inavyoonekana tu lakini hili ni jambo kubwa sana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti ningeomba Wizara pamoja na ufafanuzi mwingi uliotolewa huko nyuma, lakini bado nina hofu ya suala hili juu ya utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi wanaotaka kuingia Darasa la tisa ni wengi? Je, walimu wenye sifa, madarasa tunayoyapotosha ya kuweza kuchukua *Form I*, zote hizo ambazo zitatokea katika maskuli mbali mbali. Tunao waalimu wenye taaluma hizo tunazozihitaji za Sayansi na mambo mengineyo. Mheshimiwa Mawazo yangu mimi wanaotushauri mambo mengine ushauri wao si mzuri badala ya kutuongezea kiwango cha elimu wanatushauri namna ya kuipunguza, ya kuidumaza elimu yetu.

Kuna mpango sasa Wizara ya elimu kuwa mwanafunzi anapoanza darasa la kwanza hadi *Form VI* aliyeshauri hivyo katoa ushauri mbovu kweli kweli, haiwezekani mtoto asome bila ya kupimwa kuwa aende tu kama maji yanayochiririka katika mchirizi, haiwezekani elimu ina vipimo. Tutakuwa na wengi waliofika daraza la kumi na mbili lakini tutakuwa na wachache wenye elimu ya darasa la kumi na mbili, kama nmanvyotangaza siku hizi; siku hizi angalau mnatangaza vizuri mnasema waliochaguliwa ni kweli mnachagua hakuna mwenye kufaulu mnachagua tu huyu aende huyu abakie, hili nawasifu .

Hawezi mtoto akaingia *Form I* na alama ishirini nikasema hii ni pasi hakuna alama thalathini na sita au thalathini, kafeli lakini mmemchagua aendelee mwisho wa siku anatoka na F *compound*. Pesa nyingi Serikali na vyuo wametumia kumuelimisha na kumsomesha, lakini matokea yake anatoka hana cheti.

Mhe. Mwenyekiti, nigusie kidogo...

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano za ziada.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, nigusie kidogo bodi ya mikopo; bodi hii Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine mengi ni kutoa

mikopo kwa wafanyakazi na wanafunzi ambao wanabahatika kuingia katika vyuo vyetu vikuu, ama vya ndani vya Zanzibar kwa ndugu zetu wa damu Tanganyika hata nje. Lakini je, hii mikopo tunayotoa humu ndani inakidhi haja na tunawapa kwa wakati?

Kwanza inakidhi haja yao ya kukaa *boarding* na mambo mengine yote inawaendesha na je, tunawapa kwa wakati? Juzi nilizungumza na mwanafunzi mmoja *Semester* hii inamalizika katika milioni moja na kidogo mmewapa laki nne na hawa wengine hawapo Zanzibar wanasoma Dar es Salaam na kwengineko.

Wengine ni wasichana watoto wenyewe siku hizi hawakutulia unachompa hakikidhi haja yake nae anataka ale, anywe, sio kunywa pombe anywe maji. Watu wengine ukisema kunywa wanafikiri kulewa; mimi sinywi kwa kulewa anataka ale, anywe, avae apate na mambo mengine katika *semester* nzima unampa laki nne, hizi nyengine azipate wapi na anataka asome atafanya biashara anayoijua yeye mwenyewe, ili asirudi aendelee na masomo yake.

Kwa hivyo tumeamua kutoa mikopo, tutoe kweli na kwa wakati vyenginevyo tunachangia watoto wetu kufanya hivyo baadhi yao kufanya hivyo wanavyofanya, tusijifanye sisi tukawa ni *mas-ul* wa wanavyofanya. Kwa sababu tumeamua kuwasaidia kuwakopesha, tuwakopesheni tena kwa wakati. Mhe. Mwenyekiti, sijui hii mikopo imeanza mwaka gani, lakini waliotajwa kuwa wamemaliza mikopo yao ni 12, hivyo kwa miaka yote hiyo waliomaliza kulipa kikamilifu ni 12 wengine wote wakiwa ni kidogo hapa, hata sijui nitumie lugha gani. Kuwa ni 12 tu kwa kitabu hiki ndio wanaoonesha kuwa ndio waliomaliza mikopo yao kikamilifu.

Mimi naona idadi hii ni ndogo sana kwa uono wangu. Mimi ingawaje sijui ni wangapi waliokopeshwa lakini kwa hawa waliolipa kikamilifu ni kidogo. Kwa hivyo ningeomba hii bodi iwe na ufuatiliaji wa karibu wale ambao ni wafanyakazi waripoti katika kazi zao, ili wakatwe walipe na wengine wakopeshwe. Waliokuwa hawajaajiriwa wakipata ajira wafuatiliwe ili na wao waweze kulipa, ili na wengine waweze kukopeshwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kidogo tu kwa Baraza la Mitihani nacho hiki ni chombo muhimu kinachohusisha mitahi yetu ya ndani ya Zanzibar darasa la saba, na darasa la kumi. Mbali ya kutunga masuali na mitihani na kusahihisha ningeomba pamoja na majibu mazuri ya usafaha ya Mhe. Naibu Waziri asubuhi kwenye suala, kuwe na mpangilio maalum ya walimu watakaohusika na usahihishaji wa mitihani baina ya visiwa vyetu viwili hivi.

Mwaka juzi nilimuonesha *concern* ya namna walivyo kwa upande mmoja wanakuwa wachache sana katika usahihishaji. Ningeomba kuwa na mpango

maalum sio wawe sawa sawa huku ni kukubwa kuliko upande wa pili, skuli za huku ni nyingi kuliko za upande wa pili. Lakini *at list* kuwe na mpango unaokubalika sio kuwa watu 45 waliosahihisha mitihani fulani ikawa 5 tu au 10 ndio wanaotoka upande wa pili, hii itakuwa bado haki na uadilifu haijatendeka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache kwa sababu umeniwashia taa niseme ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Ali Juma Shamhuna, Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kufuta ada ya mitihani ya kidatu cha nne na kidatu cha sita pamoja na kuondoa michango yote ambayo wazazi walikuwa wanachangia katika skuli zetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia pongezi zangu za pekee zimuendee Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kuwatumikia wananchi wetu pamoja na watoto wetu tunaowategemea, ni kizazi cha baadaye kukijenga vizuri ili baadaye waje kuwa viongozi bora.

Pia niwapongeze kwa dhati kabisa walimu wote, kwani walimu wana kazi kubwa. Mhe. Mwenyekiti, sisi sote tuliokuwepo hapa na wengine viongozi mbali mbali kama sio walimu. Walimu wana mchango mkubwa sisi kufikia hatua hii. Nawapongeza sana na nawatakia la kheri katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba niende katika hotuba ya Mhe. Waziri kwa kuangalia mafanikio ambayo yamepatikana katika ukurasa wa 4. Ameeleza humu mafanikio mengi katika sekta hii ya Wizara ya Elimu. Suala la kwanza ameeleza kufanikiwa katika uwandikisha wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya maandalizi, msingi na sekondari.

Ameeleza na takwimu hapa kutoka wanafunzi laki 317,278 kwa mwaka 2010 na kufikia 390,464 mwaka 2015, hili ni fanikio kubwa. Mhe. Mwenyekiti, ukianga miaka ya nyuma watoto walikuwa wakiandikishwa ni wachache sana kutokana na upungufu wa mashule yetu, hiyo ni hatua kubwa ambayo serikali imefanya.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kufunguliwa kwa Kampasi ya Chuo Kikuu cha Taifa huko Tunguu, ambapo pia idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka 1205 mwaka 2010 hadi 2500 mwaka 2015. Naipongeza serikali kwa hatua ambayo imechukua. Pamoja na kuwa chuo hiki kuna programu mbali mbali zinaendeshwa zimeelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni ujenzi wa skuli mpya za sekondari 19 tena za kisasa zimejengwa katika kipindi hiki. Hayo ni mafanikio nilikuwa naomba niyataje kwa sababu wananchi wengine wanaotusikiliza watakuwa hawayatambui, lakini kupitia vyombo hivi watakuwa wanafatilia. Serikali imejitahidi kiasi kikubwa kwa sekta hii ya elimu, kuboresha mambo mbali mbali yakiwemo majengo ya shule, vyuo vikuu na pia uwandikishaji wa wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 2 kifungu namba 7 kimeeleza upatikanaji wa fedha ambapo wameeleza jumla ya shilingi bilioni moja kwa kazi za maendeleo zimepatikana kupitia serikali. Hii ni sawa na asilimia 30.3, fedha hizi ni kidogo sana kwa sekta ya elimu. Ukiangalia Sekta hii ya Elimu ina mambo mengi, ina suala zima la ujenzi wa maskuli ambazo skuli nyingi zimejengwa kupitia wananchi. Kuna suala zima la vifaa vya maabara, kuna suala zima la ujenzi wa nyumba za skuli, nyumba za walimu. Kwa hivyo ukiangalia fedha hizi za maendeleo ni ndogo, licha ya kutegemea wahisani mbali mbali ambao wanachangia shughuli mbali mbali za maendele, lakini hizi ni chache.

Kwa hivyo hapa naiyomba serikali kupitia Wizara ya Fedha iliangalie suala hili kupitia Wizara hii ili kuongezea fedha za maendeleao, haya mahitaji ambayo nimeyataja ujenzi wa nyumba za walimu, vifaa vya maabara pamoja na shughuli mbali mbali ambazo zimeanzishwa hazijakamilika. Zikiongezwa fedha hizi zitasaidia kukamilisha haya mambo ambayo nimeyataja.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye *page number 10*, Mradi wa Uimarishaji wa Skuli za Ufundi. Kwanza niipongeze serikali kwa kuanzisha mfuko wa madawati. Jambo ambalo litasaidia kupunguza upungufu wa madawati katika shule zetu mbali mbali. Hapa nilikuwa nina ushauri tu, huu mfuko wa madawati nilikuwa naomba upelekwe katika skuli hizi za ufundi ambayo ni Skuli ya Mikunguni na skuli ya Kengeja iliyokuwepo Pemba, kwa ajii ya ununuzi wa vifaa katika shule zile.

Hawa ndio tutakaowatumia watutengenezee madawati. Kwa sababu hawa tumeshawapa ufundi lakini hatuwapi nyenzo za kufanyia kazi, ina maana hata ule ujuzi wao walioupata utakuwa hawawezi kuufanyia kazi. Lakini fedha hizi zikipelekwa zikitiwa katika maskuli, zikanunuliwa vifaa mbali mbali hata zile tenda ambazo wanapelekewa watu wengine wa nje itapungua, wanafunzi hawa watachonga madawati na tena yatakuwa bora kuliko hata hayo mengine hawatengenezi yaliyokuwa bora.

Watumiliwe hao hao wanafunzi wetu wa Vyuo vya Ufundi ili kuifanya hii kazi, kwanza watapata ajira na pia serikali itapunguza gharama ya kubwa ambapo pengine madawa hayo wangechongesha katika sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Taasisi ya Elimu ya Zanzibar ukurasa 33. Taasisi ya Elimu ya Zanzibar moja ya jukumu lake ni kubuni, kuandaa mitaala, muhtasari wa elimu ya maandalizi, msingi, sekondari, uwalimu na elimu ya kujiendeleza. Hapa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nashauri, naiyomba niishauri Wizara kuhusu suala zima la somo la sayansi skim. Somo hili lingeanzishwa katika maskuli yetu, inategemea wenyewe watakavyojipanga Wizara ya Elimu, lakini somo la sayansi skimu ni muhimu. Kwa sababu somo la sayansi skimu wanafunzi watafundishwa mambo ya mapishi, mambo ya ushoni, na mambo mbali mbali ambayo yanaendana na hii kozi yenyewe.

Hii itawasaidia kuwajengea uwezo wale wanafunzi ambapo wakimaliza watakuwa wanaweza kukaa pamoja, wakajikusanya kwa pamoja wakajiendeleza au ujuzi wao huu wakautumia na hatimaye wakapata mikopo katika taasisi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, watoto wetu kama hatujawajenga tangu huku chini, hawa wanafunzi wetu na ukiangalia sasa hivi tatizo la ajira ni kubwa, fursa za ajira ni ndogo mahitaji makubwa. Kwa hivyo hawa wanafunzi wetu wakipata somo hili la sayansi skimu wakijengewa uwezo halafu wakajua kwamba sasa dhana ya ajira sio ya serikali tu, wakitoka pale wana ujuzi wao, watakaa pamoja kupitia Wizara ya Bi Zainab itawapa mikopo, wataweza kujishughulisha.

Watoto tutakuwa tumeshawajengea tangu wapo skuli anajua mimi nikitoka nitafanya shughuli fulani. Kwa hivyo somo la sanyansi skimu ni muhimu na naomba Wizara ya Elimu ilipe kipaumbele somo hili.

Mhe. Mwenyekiti, pia somo la ujasiri amali nalo lipewe kipaumbele kwa wanafunzi wetu wasomeshwe ili watoto wetu hawa waondoke na dhana ya ajira serikalini, tutawajenga vizuri ili na wao wakimaliza hata wataweza kujitegemea wenyewe baadaye.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika ukurasa wa 4 hapa kuna skuli nne ambazo zimejengwa za kisasa ambazo skuli 19 pamoja na ujengaji wa Vituo vya Amali vilivyokuwepo Mkokotoni pamoja na Vitongoji, Pemba. Mimi niko hapa nilikuwa nina ushauri tu kwamba katika hizi skuli mpya ambazo zimejengwa ushauri wangu zijengewe uzio, tuombe wafadhili mbali mbali wazijengee uzio hizi skuuli.

Kujenga uzio skuli kutasaidia kwanza kuweka eneo lile lisivamiwe, jengine kutawafanya wanafunzi wetu watakuwa katika hali ya utulivu katika masomo yao pamoja na walimu wao. Pia itasaidia hata ule ufaulu wao utakuwa ni mzuri kwa sababu watasoma katika hali ya utulivu na amani. Kwa maana hiyo watakachosomeshwa watakuwa wanakipokea na hatimae tutatoa watoto waliokuwa wazuri ambao wame - *perform* vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuhusu suala zima la Baraza la Mitihani, hii ni ukurasa wa 41 kuna kiambatanisho cha 33(b) kimeorodhesha matokeo ya mtihani kwa wilaya na kwa skuli mbali mbali. Lakini nilivyoangalia, inaonesha kwamba kwa skuli za Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharibi inaonesha matokeo hayo yamekuwa juu zaidi kuliko skuli za vijijini.

Kwa hivyo hapa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba nishauri, Wizara ya Elimu ifanye japo utafiti kidogo kuangalia tatizo gani ambalo linapelekea wanafunzi wa mjini kufaulu zaidi kuliko wa vijijini. Pengine kuna tatizo na pengine katika utafiti huo mnaweza mkabaini mambo mengi tu.

Changamoto ambazo mtakazozipata mtaziwekea mikakati ambayo itaweza kuwajengea zaidi au kuzitatua ili kuona kwamba zile skuli za vijijini nazo zinaelekea katika muelekeo mzuri wa matokeo yao ya mitihani. Nilikuwa naomba ifanye utafiti ili kuona kwamba kuna tatizo gani ambalo linajitokeza, ili skuli hizi za vijijini unakuwa ufaulu wao unakuwa tofauti pamoja na wa mjini.

Labda kwa ushauri mwengine pengine mnaweza mkafanya mfano kama katika Skuli ya Jambiani, Paje, Michamvi labda mkaziweka pamoja skuli hizi, ili labda pengine ule usumbufu wa mbali inaweza ikawa pengine inaweza ikachangia kiasi fulani. Lakini mkiziweka pamoja skuli hizi tatu za *form IV* kwa hivyo ina maana hawa watu itakuwa hata yale masafa yanaweza yakapungua. Kwa hivyo watakuwa katika hali ya utulivu na wao. Sasa naomba mjifanyie kijiutafiti ili muweze kusaidia kuona kwamba changamto zinaweza kujitokeza mkaziwekea mikakati, ili wanafuzi wetu wale wa vijiji na wao waweze kupata matokeo mazuri ya mitihani yao.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima la mikopo ya wanafunzi wenzangu wameeleza mikopo. Mikopo ni changamoto, mahitaji ni mengi, wanafunzi ni wengi wanaosoma. Lakini hapa niiyombe Wizara ya Fedha izidishe fedha katika mikopo, ili wanafunzi wengi wapate hizi fedha.

Tunaelewa hali zetu za wazazi wengi ni ngumu; kuna wale wenye uwezo na kuna wengine hawana uwezo. Naiyomba Wizara ya Fedha iongeze pesa katika mfuko huu, ili wale wanafunzi ambao wapo vyuoni ziweze kuwasaidia ili wapate wanafunzi wengi. Wanaweza wanafunzi wakapata mkopo lakini anaweza akapewa laki tatu. Pengine huyu nyuma ana deni, na pengine laki tatu hiyo haitomsaidia chochote. Naomba Wizara ya Fedha iliangalie kwa kina hili ili wanafunzi wetu wengi wapate mikopo, ili waondokane na tatizo la usumbufu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala zima la uhaba wa walimu. Kuna uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi, najua Wizara imejitahidi kiasi kikubwa kutatua tatizo hili.

Lakini hapa Mhe. Mwenyekiti, labda nitoe ushauri kuhusu suala zima la uhaba wa walimu. Labda tuangalie kwenye hiki kidatu cha tano na cha sita, hizi skuli labda tuziweke kama mfano tuchukue skuli ya Lumumba labda tuweke labda tuweke kambi ya sanyansi. Labda tuchukue skuli ya Ben-Bella tuweke kambi ya art. Tuchukue labda skuli ya *Haile Selassie* tuweke kambi ya biashara. Hii itasaidia tukiweka pamoja, itasaidia hata wale walimu watakuwa wana utulivu. Mwalimu huyu huyu tunayemtaka asomeshe Ben-Bella huyu wa sayansi atoke aende *Haile Selassie* atoke aende Lumumba, mwalimu atakuwa ana mizunguko mingi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala zima la mafao ya walimu. Nimetangulia kusema kwamba walimu wana kazi kubwa na kazi ya uwalimu ni kazi ya wito na wanajituma sana. Nimuombe Waziri wa Elimu suala zima la mishahara waangalie, hapa malalamiko yapo ya mishahara; kuna walimu wameongezwa, kuna walimu wanayo malalamiko haya tumeyasikia, tunaomba muyafanyie kazi hawa waliokuwa hajarekebishiwa mishahara yao. Naomba Wizara ichukue hatua iwarekebishie. Suala la maposho mbali mbali ambayo walimu wanadai, Wizara naomba ilifanyie kazi kupunguza yale malalamiko ambayo yanajitokeza. Na pia suala la stahiki zao Wizara ilifanyie kazi ili kupunguza haya malalamiko ambayo yanajitokeza siku hadi siku. Kwa sababu walimu wanafanya kazi kubwa na wanajitahidi kwa kiasi kikubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kuna hii Wizara ya Afya juzi walifanya zoezi la kutoa vyeti kwa wauguzi wale wastaafu. Niiulize Wizara ya Elimu je, hii Wizara ya Elimu inafanya jambo hilo, kama haifanyi waige. Unajua kufanya hivi inawajengea thamani wale wastaafu kwa sababu wameitumikia nchi hii. Kama hawajafanya Wizara ya Elimu kama hawana zoezi hili basi waanzishe wawaige Wizara ya Afya. Hii itawajengea wale walimu waonekane wana thamani na wanatambulikana.

Mhe. Mwenyekiti, naona baada ya hapo naomba niunge mkono Wizara hii ya Elimu kwa kazi nzuri waliyoifanya na nawatakia kila la kheri. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia asubuhi hii kuwepo katika Baraza hili kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu ya kuihoji serikali pamoja na kuwaelekeza, kuwaelezea kero za wananchi ili serikali iweze kutekeleza yale magumu ambayo yanawakabili wananchi wetu.

Mheshimiwa nikupongeze kwa kunipa nafasi ingawa umetupangia dakika chache, lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kushirikiana kwao na kuweza kuisoma hotuba hii vizuri na kwa ufasaha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 10 wa kitabu kilichopo mbele yetu. Hapa niende katika mradi wa Ujenzi wa Vyuo vya Kiislamu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu hapa;

"Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa na SMZ kwa kushirikiana na Serikali ya Falme ya Oman wenye lengo la kuendeleza ujenzi wa kituo cha Utamaduni wa Kiislamu katika eneo la Chuo cha Kiislamu Mazizini."

Mhe. Mwenyekiti, hii ni azma nzuri sana na niseme kwamba ikiwa kuna jambo ambalo lilikuwa liwe zuri sana basi hili limekuwa jambo zuri miongoni mwa mambo mazuri katika Wizara hii ya Elimu. Kwa sababu kurejesha utamaduni wa Kiislamu Zanzibar ni jambo la msingi.

Mhe. Mwenyekiti, utamaduni wetu kwa kweli umetekwa nyara. Kwa sababu kuna vijana wengi wa Kizanzibari... hapo zamani utamaduni wetu ulikuwa ni mzuri tu, heshima kubwa, nidhamu ya hali ya juu, mavazi mazuri yenye kumuenea mtu. Leo utawakutia baadhi ya vijana wa Kizanzibari wanawake wanavaa suruwali refu za kubana, lakini wanaume wanavaa herini na cheni.

Huu sio katika utamaduni wetu wa Kizanzibari, kwa hivyo serikali kuiruhusu Falme ya Oman kujenga jengo kubwa lile pale kwa ajili ya kuendeleza utamaduni wa kiislamu Zanzibar. Ni jambo zuri na naomba jambo hili liwe ni lenye kupewa nafasi kubwa na liwe endelevu, pale litakapofunguliwa jengo lile basi tunapaswa sana kuwapa mashirikiano wale walimu watakaopewa kuwaendeleza vijana wetu wa kizanzibari watakaosoma pale na iwe ni chachu ya kuwaendeleza wengine ambao wapo katika mazingira ambayo hawasomi pale, lakini watapata maelekezo ya kuishi vizuri na kuendeleza utamaduni wetu kwa vijana ambao wamepitia pale. Mheshimiwa hili nipongeze sana.

Halafu niende katika ukurasa wa 15 wa kitabu hiki katika Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi. Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ya Skuli za Maandalizi na Msingi hii ni Idara muhimu sana kwa sababu huwezi kufika Chuo Kikuu kama hujaanza maandalizi wala hujaanza msingi na sekondari ndio ukafika katika elimu ya Chuo Kikuu na kwengineko.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na malengo mazuri ya wizara kuifanyia Idara hii ya Maandalizi, elimu ya maandalizi, miundombinu mbali mbali ya kuiendeleza, lakini niseme kwamba bado tuna changamoto nyingi ambazo zinazikabili skuli zetu za maandalizi. Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto ambazo zinazikabili skuli za maandalizi kwanza ni ukosefu mkubwa wa walimu wa Skuli za

Maandalizi. Hilo la kwanza. Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Waziri ajipange vyema katika kuwaajri walimu kwa ajili ya skuli za maandalizi.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto ambazo zinaikabili elimu ya maandalizi ni ukosefu mkubwa wa madarasa ya maandalizi. Maeneo mengi sana yana nia na lengo la kuendeleza skuli za maandalizi, lakini wanakwaza na uwezo wa kuweza kujenga madarasa ya kusomesha watoto wa maandalizi.

Kwa hivyo ushauri wangu kwa Serikali waendeleze kuyajenga majengo ya maandalizi, lakini pia kwa watu walionesha nia ya kujenga skuli kwa ajili ya maandalizi basi Wizara iyachukue majengo haya mara moja, ili watoto wapate kuandaliwa kama ilivyo jina la skuli hizi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuendeleza juhudi za wananchi kwa kujenga mabanda ya maandalizi niwapongeze sana vijana wangu na wazee wangu wa Chwale Chambani si Chwale ya Kojani. Chwale Chambani; kuna vijiji kama vitano vimeshirikiana pamoja, kijiji cha Chwale, Matele, Usanga, Kekewani, na Tondooni. Vijiji hivi vimekaa pamoja na viliamua kujenga skuli ya maandalizi ili kuwakomboa watoto wao kwenda masafa ya mbali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mhe. Waziri na kumuomba msaada wake wa wizara kwa hali na mali vijiji hivi wamejenga banda lenye vyumba viwili na ofisi, banda hili limekamilika katika hatua ya awali ni hivi karibuni nimekwenda pale kama mwakilishi wao wakaniomba na nimeliezeka banda hili kwa kushirikiana na mbunge tumelimaliza kuliezeka, ninamuomba Mhe. Waziri banda hili alimalizie kwa plasta pamoja na fanicha ili wanafunzi wapate kukaa kwa nafasi. Ninashukuru kwamba Kamati ya Uwezeshaji Ustawi wa Jamii, ilipokuwa na ziara zake Pemba maafisa wanaohusiana na maandalizi Afisa Husika, alitwambia kwamba alikwenda kulikagua banda hili na ameiona hatua iliyofika na kwa kweli alipongeza sana.

Kwa hivyo ninaiomba Wizara ya Elimu ilipokee banda hili mara moja ili watoto wale waepukane na kusoma chini ya miembe. Mvua ilionyesha katika kipindi kilichopita sote ni mashahidi watoto hawa na wazee wao walisumbuka sana na ilibidi masomo yakatwekwa kipindi
kirefu kwa sababu hawana pa kukaa. Banda limejengwa limeshaezekwa, tunaomba kwa niaba ya wananchi hawa tulikabidhi wizara ili wizara watumalizie banda lile kwa kulifanyia *finishing*.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika Elimu ya Msingi. Elimu ya msingi baada ya maandalizi ni elimu muhimu na ile imeitwa msingi kwa sababu jengo bila ya msingi haliwi. Ina maana kwamba elimu ya msingi ni elimu

muhimu ambayo inamuandaa kijana awe madhubuti kwa ajili ya kuendelea na elimu ya sekondari.

Mhe. Mwenyekiti, elimu ya msingi katika visiwa vyetu vya Zanzibar imekabiliwa na changamoto tena nyingi, miongoni mwa changamoto ambazo zimeikabili elimu hii ni ukosefu mkubwa au upungufu mkubwa wa walimu hasa katika skuli za vijijini.

Unapotembea vijijini katika skuli nyingi za msingi basi takriban walimu wengi wana vipindi 40 na zaidi, hivyo vipindi 40 watasomesha vipi. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri alione hili na kwa kweli kwa sababu kuna walimu ambao wameshasomea muda mrefu hawajaajiriwa, apange utaratibu wake wa kushirikiana na Wizara inayohusika na ajira, vijana wetu hawa waajiriwe ili upungufu huu wa walimu uondoke.

Mhe. Mwenyekiti, tuna kazi kubwa katika skuli za msingi, hivi sasa kuna huo utaratibu wa ufanyaji wa mitihani wa darasa la sita pamoja na darasa la saba kwa mwaka huu walimu tumewapa kazi kubwa kuwaandaa wanafunzi wa darasa la sita kwa ajili ya mitihani na darasa la 7. Lakini hapa ningemuuliza Mhe. Waziri mitihani hii ambayo inafanyika mwishoni mwa mwaka huu darasa la sita na la saba mitihani yao ni mimoja au la sita watafanya yao na la saba yao. Lakini pamoja na hivyo ningemuuliza Mheshimiwa amejiandaa vipi kupokea idadi kubwa ya wanafunzi wa *form I* baada ya mitihani yao.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyengine ambayo nataka niizungumze hapa kuna walimu wetu ambao wanasomea Diploma ya Sayansi Mbweni, walimu hawa ni muhimu, lakini miongoni mwa changamoto ambazo zimewakabili Mheshimiwa ni kukosa muda, wizara haikuwapa ruhusa ya kusoma. Kwa sababu imewapa ruhusa nusu haikuwapa ruhusa kamili, Mheshimiwa hili ni tatizo. Mwalimu anatoka Bumbwini anakuja kusoma Mbweni asubuhi lakini wakati huo huo saa sita na nusu anatakiwa awe skuli anafundisha, ufanisi uko wapi.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri hili aliangalie kwa kina kwa kuwa *course* ile ni endelevu walimu wote ambao wamepangiwa kusoma elimu ya diploma ya sayansi wapewe muda wa kusoma wasiwepo kazini, siku kazini asubuhi, mchana wanakuwepo skuli au wanakuwepo skuli asubuhi mchana wanakuwepo masomoni.

Mhe. Mwenyekiti, ufanisi haupatikani. Mwalimu anapata tabu yeye ya kusoma lakini pia na wanafunzi wanaosomeshwa hawapati ule mustakbali mwema wa masomo kupitia kwa mwalimu yule. Kwa sababu mwalimu hakuwa na muda mzuri wa kujiandaa kwa ajili ya kutoa elimu.

Mhe. Mwenyekiti, umetupangia muda mdogo sana kwa kweli niende katika Bodi ya Mikopo ukurasa wa 40. Bodi ya Mikopo ni bodi muhimu lakini ina changamoto, miongoni mwa changamoto ambazo zinaikabili Bodi ya Mikopo inawezekana kwamba ni fedha chache ambazo wanapangiwa kupewa na Wizara ya Fedha. Lakini na wao wanapotoa mikopo wanawacheleweshea vijana wetu na wanapata tabu, katika maeneo yao wanayosoma.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana kwamba Wizara hili iliangalie kwa kina vijana wapo nje ya Unguja wanasoma, nje ya Zanzibar wengine kama hapo Tanzania Bara. Wengine wanasoma hapa hapa lakini masafa ya kwenda na kurudi. Kwa hivyo nawaomba sana Bodi ya Mikopo itoe mkopo ulioahidiwa kupewa kwa mwanafunzi apewe kwa wakati. Lakini nisikitike na wizara kwamba mimi ni mjumbe wa kamati ambayo inasimamia Wizara ya Afya tumewaomba mara nyingi twende Bara kwenye Bodi ya Mikopo na kwengineko, ili kuangalia changamoto ambazo zinawakabili vijana wetu, lakini Wizara ya Elimu mpaka tunamaliza mzunguko wetu uliopita wameshindwa kutupeleka, jamani watoto wetu wana changamoto nyingi.

Sisi kama watetezi wao tulikuwa tunapaswa twende tukawaone kusikiliza kuna lipo na lipi la kuweza kuwasaidia na kuna lipi la kuweza kushauriana na Wizara ili kukwamua changamoto ambazo wanazo.

Ushauri wangu kwa Serikali kwa ujumla wake katika kipindi kijacho basi kila kamati inayohusika na wizara husika ikiwa kuna mambo ya kuyafatilia, Tanzania Bara au kwengineko basi wizara ijipange vyema katika bajeti yake iwapeleke kwa sababu wanajifunza mengi na vile vile wanapata mambo mengi kupitia kwa vijana wetu ambao wapo masomoni nje ya hapa.

Nikiendelea katika Bodi ya Mikopo kwa kuwa wasomaji wengine miongoni mwao ni wanachama wa Mfuko wa ZSSF, naiomba Wizara ya Elimu ishirikiane na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wapange mipango endelevu ili vijana wanaosoma basi ZSSF iwawezeshe kwa sababu ni wanachama.

Aidha, wazee wao yaani vijana ambao wanasoma ambao wazee wao ni wanachama wa ZSSF basi wapatiwe aidha mkopo au fungu maalum kwa ajili ya kuwawezesha watoto hawa. Kwa sababu lengo la ZSSF ni kumsaidia mtu mafao na miongoni mwa mafao ni elimu, unasubiri mpaka mzee anaendea mkongojo ndio unakuja kumpa. Hapana, tunaiomba Serikali ifanye mipango endelevu kwa ajili ya vijana wetu wanaosoma wapate msaada kupitia ZSSF, ili waendelee na kusoma pamoja na mikopo wanayopata lakini na mfuko wa ZSSF utoe huduma kwa ajili ya vijana wetu hawa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na Bodi ya Huduma za Maktaba ukurasa wa 44. Kwa kweli niseme kwamba hii Bodi ya Huduma za Maktaba ni Bodi muhimu sana kwa sababu Maktaba ndio roho ya elimu. Elimu bila ya kuwepo maktaba basi inakuwa haina raha, haina ladha lakini kuwepo kwa Bodi ya Maktaba na wamesema hapa kwamba wameingiza vitabu vingi kutokana na kuwaendeleza vijana wetu wa fani mbali mbali.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ninaipongeza sana Bodi hii ya Maktaba lakini natoa ushauri kwamba watoe elimu tosha kwa vijana wetu kwa sababu wanafunzi wengi ambao wanaishi vijijini miongoni mwao hawajauona au hawajaufahamu umuhimu wa maktaba. Kwa hivyo Bodi itoe taaluma kwa vijana, ili vijana wetu wakimbilie maktaba ili kupata faida kubwa katika masomo yao.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 55. Ukurasa wa 55 niende katika tamko hili la vipaumbele. Miongoni mwa vipaumbele Mhe. Waziri alisema hapa kwamba kwa mwaka 2015/2016 vipa umbele vya Sekta ya Elimu ni kuongeza upatikanaji wa fursa ya elimu kwa usawa katika ngazi zote za elimu na mafunzo ya amali.

Nakuja nukta ya tatu; michango iliyokuwa ikitolewa na wanafunzi katika ngazi ya elimu ya msingi itafutwa rasmi kuanzia mwezi Julai, 2015. Mhe. Mwenyekiti, hii ni azma nzuri sana lakini azma hii kwa kweli inatakiwa wizara itoe taaluma ya kutosha kwa wazee wa watoto hawa, kwa nini? Kwa sababu michango ya elimu katika kipindi ambacho wanachangia wazee ilikuwa inafaidisha mambo mengi, si chaki tu na mabuku. Ilikuwa ni chaki, mabuku pamoja na uendelezaji wa majengo ya skuli, michezo na mengineyo.

Sasa ninaiomba wizara ili iwapunguzie hoja nyingi walimu wakuu kwa wazee pamoja na Kamati za Skuli, wizara itoe taaluma ya kutosha na tu isitowe taaluma kwenye radio tu bali ipite skuli kwa skuli au Wilaya kwa Wilaya au Jimbo kwa Jimbo, ili kuhakikisha kwamba wazee wameifahamu vyema dhana hii. Vyenginevyo Skuli zinaweza zikashinda kupata ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nilikuwa na mambo mengi ambayo niyazungumze lakini umeniwashia taa kwa mara ya pili nitaheshimu, nataka nizungumze dakika moja kuhusu mishahara na maposho ya walimu.

Tuna walimu wetu kadhaa bado tunapiga kelele jamani nani kama mwalimu, walimu wapewe mishahara yao ilikatwa wakati wa mabadiliko ya mishahara na maposho ya likizo na vyenginevyo, wapewe kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, nakushkuru kwa kunivumilia na sana kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu kabisa kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Elimu.

Mimi nianze kwa kuonesha hiki kitabu ambacho Mhe. Waziri ametuletea, hii itakuwa wizara sijui ya tano au ya sita lakini *quality* ya kitabu kama hiki sijaiona mimi. Hata Mhe. Haji Omar Kheri aliyekuwa na vitabu vitatu basi *quality* ya vitabu vyake vilikuwa ni *water proof,* sasa sijui wachapaji maana yake vyote hivi vimechapwa na mchapaji wa Serikali; hii Wizara ya Elimu ameionea au sijui ni maagizo ya Wizara ya Elimu yenyewe.

Ningependa tu kushauri kwamba vitabu kama hivi kwa sababu sijui ni *tissue paper* zimetumika hapa au vipi lakini hivi vikipigwa na mvua kidogo tu huna tena kitabu. Kwa hivyo ningeomba mara nyengine vitabu kwa sababu ni mchapaji huyu na ni wizara zote hakuna kubwa wala ndogo basi viwe *of the same quality,* hilo la kwanza.

La pili Mhe. Mwenyekiti, uamuzi wa Serikali kwamba elimu kuanzia bajeti ya mwaka 2015/2016 yaani Julai, 1 haitakuwa bure lakini itakuwa bila ya malipo. Mimi nilisoma skuli baada ya Mapinduzi na tamko la Marehebu Rais wa Kwanza wa nchi hii, Mungu amrehemu aliko, ilikuwa ni elimu bure. Tafsiri ya vitendo vya kauli ile ni wanafunzi nikiwemo na mimi, zaidi ya sare ya skuli kiatu kama utakipata, soksi, suruali, shati na mkoba wa ukili kwa kutilia vitabu lakini kila kingine kilichobakia ilikuwa mzee halipi. Sasa na mimi naungana na Mhe. Mwakilishi wa Chambani Mhe. Waziri utakapokuja hapa kufanya majumuisho utueleze kinaga ubaga maana ya elimu bila ya malipo kwa elimu ya msingi, maana yake nini?

Twambie kabisa nimesema hapa zamani ilikuwa vitabu, *text books (*vitabu vya kusomea), madaftari (*exercise books*), penseli, dawati, kiti, meza na zile kalamu za michovyo mnazijua mpaka *gloating* la kufutia wino kama ni mwingi.

Sasa je, tafsiri ya kauli ya Rais ina maana hii? Hilo ni moja tufafanuliwe vizuri ili wananchi wafahamu mwanafunzi wa elimu ya msingi mimi kama baba au mzazi natakiwa nini na nini na nini. Lakini naamini kauli ile itafata misingi hii ambayo nimeieleza na ni matumaini yetu kwamba wanafunzi wa shule ya msingi kuanzia tarehe 01 Julai, maana yake bajeti ndio inapoanza zaidi ya *uniform* na mkoba wa ukili au vitu vya kuhifadhia vitabu hatatakiwa tena kuchangia chochote.

Lakini kama hilo halitoshi mheshimiwa suala la wanafunzi kulipa tena si kulipa tu skuli zinatofautiana hata viwango vya ada vilivyokuwa vinawekwa vilikuwa vinaekwa na Kamati za Maendeleo ya Skuli, vilikuwa vinatofautiana. Kulikuwa na ada za kuingia darasa jengine, unatoka darasa la tatu uingie la nne kama hujalipa huendi.

Kulikuwa na ada ya kununua madeski, huna unaambiwa rudi, kulikuwa na ada hata ya kujenga skuli. Sasa yote haya yasije yakageuzwa tusizungumzie darasani tu daftari, kitabu cha kusomea, kalamu isiwe ni hivyo na hayo mengine yote vyenginevyo itakuwa mmebadilisha lugha tu. Lakini hakutokuwa na tofauti ya kauli ya Rais aliyokusudia na huko nyuma tulivyokuwa tunatokea.

Mhe. Mwenyekiti, walimu ni watu kama sisi wana mbinu tofauti, mimi najua kwamba kama waziri hajui basi namwambia kwamba kuna walimu wanapeleka biashara zao maskulini na hii imetokana na nini? Hali ya walimu ni mbaya.

Kwa hivyo, njia nyengine anakwenda kusomesha lakini upande huu ana mkoba mna sambusa, kuna kachori, luna kababu, kuna chipsi. Kuna skuli nyengine mwanafuzi kama hana pesa za kununulia anakopeshwa na lazima alipe, sasa ni yale yale. Mimi jamani sina pesa aah chukua utakuja kulipa tunakamatwa huko majumbani sisi, mimi mwalimu kanambia kama sikwenda kumlipa pesa zake atanipiga. Sasa na hili Mhe. Waziri nalo mlione tusijekuwa tumefunua tandu tukafunika nge, tandu anauma na ng'e anauma lakini ng'e ana sumu kali zaidi kuliko tandu. Kusiwe na ujanja wowote na hili ni jukumu lenu Wizara ya Elimu, kusiwe na ujanja wowote wa mbadala wa gharama. Hizi biashara za skuli kwa walimu nasema tena, mimi sisemi zipigwe marufuku lakini angalau zisiwe zinawa-*disturb* wanafunzi wenyewe, wanafunzi wamekwenda pale kusoma hali zetu tunazijua, wengi humu nasema ni wote watoto wa wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, tumesoma skuli unatoka asubuhi hata maji ya kunywa hujanywa achilia mbali chai unarudi kwenu saa nane midomo imekauka, kwa waliokuwa wanajipata pata *Alhamdulillah*, kuna maandazi yanauzwa na hizo biashara walikuwa hawafanyi walimu, biashara walikuwa wanafanya wanafunzi wanapewa mikoba wakati wa risesi pale wote wananunua. Mwanafunzi hawezi kumlazimisha mwanafunzi mwenzake kwamba lazima ununue, lakini mwalimu anaweza. Kwa hivyo, hili Mhe. Mwenyekiti, naomba lieleweke vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili upungufu wa walimu, humu mna jadweli nyingi tu kila mwaka *enrollment* yaani uandikishaji wa wanafunzi unaongezeka tena kwa asilimia kubwa tu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hakuna uwiano wa kuongezeka kwa wanafunzi na walimu. Mimi nina skuli moja kule jimboni kwangu ya Mjini Kiuyu ni katika hizi skuli mpya, sasa hivi wako darasa la saba tangu ianzishwe. Madarasa

ni manane, walimu ni watano sasa hebu niambie unatafuta hata ile *free period* ya mwalimu huipati na kuna *class* nyengine zinakaa hazina walimu, walimu watano madaraka manane, kila mwalimu akiingia darasa moja maana yake madarasa matatu hayana walimu. Sijui tunafanya kitu gani, sijui tunafanya jambo gani na darasa lenyewe utakuta kuna wanafunzi 60 mpaka 80. Kwa hivyo, walimu mara nyingi hawatoi *homework,* kwa sababu gani?

Kwa sababu wewe unasomesha *subject* tatu; kwa siku kila *subject* ukitoa *homework* kila *class* watu 80 maana yake ni madaftari 240 utakwenda kweli kuyasahihisha hayo. Na hata *class work* skuli nyingi wanafunzi wanabadilishana, mimi nachukua la huyu na langu mimi anachukua mwengine, mwalimu ana-*dictate* hesabu namba tatu, nne na nne nane aliyepata nane tia *write* wala mabuku yale mwalimu hayaangalii katia *right*, katia *wrong.* Suala la walimu lina umuhimu wake mkubwa, vyenginevyo tunafikiria watoto wetu wanakwenda shule kumbe kuanzia asubuhi mpaka saa saba hajaja mwalimu hajamuona wala hajasoma jambo lolote. Hili mimi nataka niliunganishe kidogo na hesabu.

Mhe. Mwenyekiti, sijui waziri atatwambia anahitaji walimu wangapi na ana wangapi. Na si suala kwamba hakuna mwenye sifa kuna wanafunzi wengi wamemaliza mafunzo ya ualimu kutoka vyuoni wanaranda, wengi tu unaweza ukasema kwamba tunatafuta mwalimu wa sayansi. Hivyo kweli darasa la kwanza mpaka la tano mwalimu aliyesoma ualimu hawezi kusomesha?

Mimi nakubali walimu wa sayansi sawa, lakini walimu wa sayansi kwa skuli maalum. Mhe. Waziri utwambie unahitaji walimu wangapi na unao wangapi, na hawa kama wataajiriwa wote utahitaji kiasi gani ili ikiwezekana Baraza hili hizi programu hizi ambazo umeandika humu skuli ya maandalizi, skuli ya sekondari tujue kwamba tunakata hapa tunapeleka kule, ili kuhakikisha skuli zetu zote za msingi kwanza zina walimu wa kutosha.

Mimi rai hii natoa kwa sababu huu si mwaka wa kwanza wala wa pili, wala tatu imekuwa kama ni mazoea siku zinakwenda, wanafunzi hawasomi, wanaosoma na masomo yenyewe ndio kama hivyo.

Kwa hivyo, ni vizuri Mhe. Waziri ukija hapa utueleza unahitaji walimu wangapi, tunao wangapi na hawa katika bajeti ya mwaka huu au unahitaji ili uwakamilishe ungehitaji kiasi gani ili Baraza hili lione umuhimu wa elimu bila ya elimu hakuna nchi yoyote ambayo ina mwelekeo, elimu ndio msingi wa kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye *page* 108, hapa kuna jadweli nilitaka kufanya marekebisho tu kidogo, 108 Skuli ya Minungwuni hizi ni skuli ambazo bado kuezekwa. Nimefanya mahesabu yangu nikakuta kwamba madarasa yaliyokwishaezekwa bado plasta na sakafu ni madarasa 69 lakini skuli 20, yaliyofikia hatua ya kuezekwa ni madarasa 218 kwa skuli 38.

Mhe. Mwenyekiti, skuli 38 hatua hiyo imefikiwa na wananchi, skuli 38 kila moja uipe milioni 50 tu unamaliza plasta, unamaliza na kuezeka. Hiyo ni 1.9 bilioni unamaliza bughudha ya skuli ambazo hujazieka na kuzipiga plasta utabakisha na zile skuli 20 tu.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni kikao kilichopita tulizungumzia hii ada inayotolewa na wasafiri na inatumika kwa ajili ya kununua madeski, ikafanywa hesabu hapa upande wa serikali huo ikaja hesabu ya kwanza kwamba kwa gharama hii aliyotwambia Waziri wa Elimu na fedha ambazo Waziri wa Fedha, ametwambia kila deski na tuliweka pamoja kila kitu meza, kiti, deski zote tuipe deni moja kubwa. Deski tukakuta kwamba kila deski inawezakana ikawa ni kiti au meza itagharimu 620,000 kila moja. Waziri wa Fedha akasema hapana, ilikuwa ni nusu tu, tukasema haya na iwe nusu 320,000.

Hivyo kweli ni deski gani hilo labda la dhahabu ni 320,000 kwa deski moja tena tumefanya kama ni deski, au kiti, au meza wakati deski ina *highest price*. Kiti pengine ni robo tu ya bei ya deski, meza ni nusu tu ya bei ya deskti tukasema wote hivi tuvipe bei moja kubwa 320,000.

Mhe. Mwenyekiti, nimekwenda *home furniture* Dar es Salaam, *the best desk* ni 165,000 safi kabisa halina mikwaruzo, sio kama hili ambalo mwanafunzi akifanya hivi inabidi akatiwe *iodine* plasta. Tungefanya hiyo hesabu ya 165,000 *per desk* fedha ambazo zingebaki ni 2.6 bilioni na tunahitaji *only* 1.9 *billion* ya kumaliza skuli zetu ambazo hazijaezekwa na plasta, matumizi mabaya ya fedha za watu.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba uje hapa utueleze vizuri ile hesabu siku ile haikukaa vizuri, leo una uwanja mpana ni kiasi gani umepewa, umenunua kiasi gani kwa gharama gani halafu tukuulize kwa nini ikawa bei hii.

Mhe. Mwenyekiti, mkopo wa wanafunzi vyuoni, Mheshimiwa Mwakilishi wa Chambani amezungumza vizuri tu mimi nataka kuongeza. Juzi Ijumaa walikuja wanafunzi hapa kuwawakilisha wanafunzi wenzao kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; kule kuna jumuiya tangu enzi na jadi wanafunzi wanaosoma Mlimani kutoka Zanzibar wana jumuiya yao, wanafunzi wa Zanzibar. Wamekuja hapa watatu Mwenyekiti na Katibu na Mshika Fedha wa hiyo jumuiya, kuja hapa Baraza

la Wawakilishi kuonana na wawakilishi wote ikiwezekana lakini tukaenda baadhi yetu. Ni kwamba wametueleza mambo ambayo yanawakuta kama mzazi hasa utasema bora mwanangu arudi, wamepata mkopo 1.3 milioni kwa mwaka mpaka mwaka unamalizika wamepewa *four hundred thousand*. Sasa basi, imebidi baadhi ya wanafunzi wanawake wabadilishe tabia, ndio huna hata hela ya kununua chipsi unataka kusoma unafanyaje, unakwenda kujiuza.

Kwa hivyo, sababu nyengine ya watoto wetu kuharibika inasababishwa na serikali, halafu hapa tumeambiwa kwamba mwaka huu ninayo hesabu hapa ilikuwa wapewe mkopo wanafunzi 1200, wamepewa mkopo 1611 ongezeko la asilimia 34 wanafunzi 411.

Sasa inakuwaje kwamba mnapata *additional* lakini kumbe kuna watu hamjawapa pesa kwa kujikimu na shughuli nyengine kiasi hicho ambacho mnakieleza, kulikoni ipo namna. Watoto wetu wanaharibika na mnawaharibu nyinyi kama hamna mikopo waambieni kwamba hatuna mikopo, wale ambao hawana mikopo wazee wao wanahangaika hangaika mbona hakuna hili. Sasa kama serikali inaji-*commit* kwamba huu ni mkopo tunakupeni basi iwe ni mkopo kweli wasituharibie watoto kiasi hicho. Sasa wanawake wanapokwenda kuuza wanaume waende wapi, si mtihani huu.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho najua unanivumilia katika skuli ambazo hazijaezekwa Wilaya ya Wete mimi nina skuli mbili ya Minungwini imo kwenye orodha hii na ya Kangagani. Bahati nzuri hizi rikodi zao haziko sawa kwanza Minungwini, si madarasa mawili ni *five classes* na hivi ninavyokwambieni *Alhamdulillah* tumehangaika hapa na pale Skuli ya Minungwini imeezekwa kwa bati la kisasa na si muda mrefu tutamuomba Waziri atafute tarehe ya kwenda kufunguliwa rasmi. Kwa hivyo, *record* zenu muweke vizuri, si madarasa mawili ni matano na sio kwamba sasa hivi ninavyokwambieni imeshaezekwa na watu wanamalizia *finishing*.

Skuli ya Kangagani tumeijenga kwa chenga na unga mpaka yale matufali baada ya kuwa meupe sasa ni meusi kila siku ahadi, kila siku ahadi tunahangaika. Nimeshapeleka mimi mabati 420 palipobakia pesa mnazo tusaidieni. Tusaidieni Skuli ya Kangagani sasa hivi wanafunzi sijui waende *shift* tatu au sijui *shift* nne ni mtihani, *shift* mbili hazitoshi hawana pakusomea jengo hilo la sekondari lina zaidi ya miaka minane, tunajenga kwa chenga na unga, tunaomba hapa na hapa. Tusaidieni hapa palipobakia, nasema tena mabati kamili yapo tayari tushayapeleka, tusaidieni mbao tuezeke. Tutaweka mchanga wenyewe hivyo hivyo tutasomea, kwani hayo madarasa mengine ambayo yamejengwa si hivyo hivyo, unakwenda darasani utafikiri uko baharini pwani, mashimo kama bao la soo, tutasoma hivyo

hivyo tupeni mbao za kutosha bati tunazo ili tuezeke kabla ya bajeti hii kumalizika, *Inshaallah*.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba hali mbaya sana, wanafunzi wanaosoma nje ya nchi nimeangalia humu kitabu hiki cha Mhe. Waziri *page* 135 ukifungua pale. Hii inaonesha wanafunzi Wazanzibari walioko au wanaosoma vyuo vya nje 135, Malaysia, China, Ukraine, Egypt ni 14, India haikuandikwa nambari hapa lakini kwa mujibu wa nambari India ni 13, Egypt 14, jumla ya wanafunzi 198.

Mimi nina rafiki yangu watoto wake wako Algeria, Algeria humu sijaiona tena kila mwaka hata kama *scholarship* zenyewe pengine zinatoka Bara, lakini hawa ni Wazanzibari na wala hawakupata *scholarship* hii kwa sababu wanakaa Bara. Hivyo Wizara ya Elimu haina rekodi hii, wako wengi tu Algeria.

Sasa Mhe. Waziri labda atueleze matayarisho ya kitabu hiki ilikuwa haraka haraka kiasi ambacho mambo mengine humu hayamo na kwa hivyo kitabu hiki ni *incomplete* au hivi ndio usahihi wenyewe. Kama ni usahihi wenyewe hawa wanafunzi wengi tu Wazanzibari walioko Algeria wanasoma masomo mbali mbali, kwa nini hawakuingizwa humu na pengine si Algeria peke yake kuna mambo mengine msione tabu twambieni ili tuweke kumbukumbu vizuri. Kwa sababu hapa mtu anaweza kusema hee, kitabu hiki hatusomi peke yetu sisi, vitabu hivi tukishasoma sisi watu wanavichukua wanakwenda kusoma, hii mbona mwanangu mimi hayumo humu na mwanangu yuko Algeria, mbona kiko hivi mtawatia wazee wengine wasi wasi. Kama kitu ni *incomplete* bora kisiingizwe wakapewa watu wasiwasi, kikiingizwa kitu humu iwe ni *complete* na kama nilivyosema hii ni Wizara ya Elimu ndio kila kitu.

Kwa hivyo, ukiweka rekodi nyengine humu kama vile hakuna *proof reading*, kama ni *drafting*, ingekuwa ni rasimu mimi nisingekuwa na tatizo lakini *final product* ya kitabu kimeletwa hapa kwamba kila kilichomo humu ni sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote sina budi na mimi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai huu tukaweza kukutana katika Baraza lako hili tukufu katika kufanya majukumu yetu.

Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi angalau niweze kusema machache katika wizara hii. Tatu nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

kwa hotuba yake nzuri ambayo alikuwa akiitolea ufafanuzi mkubwa siku aliyoiwasilisha na aliwasilisha vizuri. Kwa hivyo, nampongeza sana yeye na watendaji wake wote kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu katika ukurasa wa 15, lakini kabla sijaendelea huko pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa kuiona hii Wizara ya Elimu na kuwaona wazazi walivyokuwa na mzigo mkubwa katika kutoa ada zile za wanafunzi ambapo ni jambo lililokuwa likiwasononesha wazee hasa ukizingatia watu wetu ni wanyonge.

Kwa hiyo, Mhe. Rais nampongeza sana, nampongeza kwa dhati kabisa juu ya kuwaonea imani wananchi wake kuondosha ada hii na wazee sasa kuondokana na ule moyo kudundwa dundwa na hofu kila kipindi cha malipo kinapofika.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu huu katika ukurasa wa 15 ambapo kuna Elimu ya Maandalizi na Msingi. Niipongeze sana idara hii kwa kujitahidi kusimamia upatikanaji wa elimu kwa watoto wetu ambapo watoto wameanza kutayarishwa kielimu wakiwa wadogo kabisa, hali ambayo inawajenga uwezo mkubwa na ufahamu mzuri wanapoingia darasa la kwanza.

Nipongeze sana kwa hatua hii lakini niiombe serikali wale walimu wetu ambao walikuwa wakiwafunza wanafunzi katika kile kipindi cha "Tucheze Tujifunze", basi ningeomba walimu hawa wakawapatia na wao ajira katika skuli zetu hizi za maandalizi kwani ni muda mwingi na wao wamekuwa wakijishughulisha na kufunza watoto. Kwa hiyo na wao tuwapatie ajira waweze kujisikia na wao.

Mhe. Mwenyekiti, pia idara hii imechukua jukumu la kuvitembelea Vyuo vya Qur-an. Hii ni hatua nzuri na tunaipongeza pale ambapo wametoa Juzuu 2000 kwa kuwapatia wanafunzi kuwapunguzia changamoto katika masomo yao. Kwa hiyo, serikali niiombe kwa kuwa ndio tegemezi kwetu na ndio tegemeo la wananchi basi kuendelea kuwapatia vifaa wanafunzi hawa wa katika Madrassa, ambapo na wao wanakuwa wanakabiliwa na changamoto nyingi hasa kuwapatia Mas-hafu na vitabu vyengine vya Kidini ambavyo vitaweza kuendeleza katika masomo yao.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa 34 ambapo kuna Mamlaka ya Mafunzo ya Vyuo vya Amali. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze serikali kwa jitihada zake na niseme tu serikali kama ilikuwa imekusudia kuvianzisha hivi vyuo vya amali kwa dhamira nzuri kabisa, kwani ilielewa kabisa kufanikiwa kuvianzisha vyuo hivi vya amali na tukaweza kuviendesha, basi vijana wetu wangeweza kuondokana na umasikini na pia wangeweza kupata ujuzi na ambapo tunasema ujuzi huwa hauzeeki. Kwa hiyo, wanafunzi wanaotoka pale

wangeweza kuwa na ujunzi mzuri ambao ungeweza kuwafanya waweze kujiajiri wao wenyewe na kuondokana na umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niiombe serikali kwa sababu vyuo hivi vinaonekana kuwa na changamoto kubwa na kama hatukuviangalia kwa umakini tunaweza tukapoteza vyuo vyetu hivi na lile lengo la serikali ambalo limekusudiwa kwa dhati kabisa likaweza kukosekana. Mheshimiwa kwa nini nasema hivyo? Vyuo hivi vinakabiliwa na changamoto kubwa kwanza ikiwemo ukosefu wa vifaa vya walimu kufundishia wanafunzi katika vyuo vyetu hivi.

Sasa vyuo hivi vitakapokuwa walimu wenyewe hawana zana za kufundishia, kwa maana hiyo inaweza ikasababisha hata wale walimu wakakosa ile hamu ya kuwafunza wanafunzi kwa sababu hakuna cha kuwafundishia.

Pia katika Vyuo hivi vya Amali walimu wetu imekosekana ile *scheme of service*. Mheshimiwa tulikuwa tunasisitiza hapa kuiomba serikali katika idara zetu au wizara nyingi kwamba *scheme of service* ni muhimu kwa kuziweka kwa walimu wetu zingeweza kuwaweka katika malengo mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, pia serikali iliwaahidi wanafunzi wale ambao walimaliza mwanzo vyuo hivi vya amali basi vilisema kwamba vitawapatia mikopo ili wanafunzi hawa watakapotoka pale waweze kwenda kujiendeleza katika fani zao zile walizofanikiwa kujifunza. Hili basi lingekuwa ni msaada mkubwa kwa serikali, wanafunzi wale wangetoka na ujunzi na wangetoka na mikopo katika vyuo basi wangeweza kwenda kuanza kujiajiri na pengine wangefanikiwa hata kuwaajiri wenzao.

Mhe. Mwenyekiti, kuna walimu pia ambao walikwenda Iran kimasomo katika Vyuo vya Amali. Mhe. Mwenyekiti, niiombe sana serikali walimu hawa walipata dhiki sana wakati ule wa kwenda maposho yalikuwa madogo, lakini pia wamerudi bado fedha zao hawajaingiziwa hadi hii leo. Mheshimiwa niombe sana kwani walimu kama wenzangu walivyotangulia kusema hapa ni watu wenye kazi kubwa na nzuri ambayo inaleta manufaa kwa jamii nzima.

Vile vile niiombe serikali kwa nia safi kabisa kuviachia hivi vyuo vya amali viweze kujiendesha vyenyewe, vyuo hivi tutakapoviachia wenyewe kujiendesha vinaweza vikafanya kazi moja nzuri na ikaweza kuleta tija. Sio vibaya kuiga jambo zuri tunaona wenzetu wa *VETA* hivi sasa wanakwenda vizuri katika vyuo vyao, hebu na sisi tuwaachie vyuo vya amali viweze kujiendesha na mamlaka iwe msimamizi wao au tuweze kuwaingizia bajeti zao, katika Halmashauri zao za Wilaya ili waweze kujiendesha. Vyuo hivi vina changamoto kubwa na ni vizuri tukaviangalia kwani huu ndio msaada mkubwa kwa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu huu katika ukurasa wa 30. Hapa kuna Idara ya Michezo, nachukua fursa hii na mimi kuipongeza sana idara hii na kwamba idara hii ilikuwepo mwenzangu Mhe. Fatma Mbarouk alisema kwamba hii si idara ngeni kwetu, ilikuwepo michezo ikifunzwa skuli lakini hapo katikati baadae tukaja tukaacha.

Sasa serikali kwa kuona umuhimu huo na ikaanzisha tena mimi nachukua fursa hii kuipongeza kwa sababu tunasema michezo ni afya vijana watakaposhiriki katika michezo watakuwa na afya nzuri. Lakini pia michezo ni ajira vijana wetu hawa wakiandaliwa vizuri katika michezo wanaweza wakaibuka na vipaji vizuri ambavyo vikawajengea sifa nzuri baada ya kumaliza masomo yao.

Mhe. Mwenyekiti, pia kwa sasa ajira tayari tunazo, kama Jeshi la Polisi au Jeshi lenyewe. Mimi hata katika bajeti zilizopita niliwahi kuhimiza kwamba gwaride liendelee kuchezeshwa skuli, kwa sababu gwaride hili litakapoanzishwa ajira hii ya polisi na jeshi lenyewe tayari mwanafunzi akitoka pale ana ujuzi wa kulielewa gwaride kutoka skuli na inakuwa ni rahisi sana atakapopata ajira kuweza ku-*cover* mara moja yale mafunzo atakayofundishwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitoe mfano mdogo tu ambao vijana hawa wakati walipoteza mwelekeo wa kukosa kujifundisha gwaride skuli. Mimi kuna mjukuu wangu mmoja tulimpeleka JKU ilikuwa kazi kubwa sana ya kufundishwa gwaride lile, akiambiwa peleka mkono kushoto anapeleka wa kulia, akiambiwa peleka kulia anapeleka kushoto. Kwa hiyo ilikuwa kazi kubwa mpaka alifungwa jina katika mgongo wake akaandikwa nanga namba 2. Kwa hiyo, si jambo la busara ni vyema hili gwaride tukaendelea kulifunza ikiwa maskuli na ikaja ikawarahisishia vijana wetu watakapokumbana na ajira hizi.

Mhe. Mwenyekiti, pia niendelee na mchango wangu huu katika ukurasa 40 ambapo kuna Bodi ya Mikopo, wenzangu waliotangulia walisema na mimi naomba nisisitize. Ni kweli wizara ina jitahidi katika kutoa mikopo ya wanafunzi, tunaipongeza kwa hatua ambayo inatoa na tunaelewa changamoto ambazo zipo katika serikali yetu, lakini bado tuiombe Bodi hii iweze kuwapatia wanafunzi mikopo kwa wakati. Kwa sababu vijana wetu wanahangaika, vijana wetu ni wanyonge na ukeshamwambia umepata mkopo huwa tena ile roho imeshategemea. Kwa hiyo, bado kapata mkopo lakini bado dhiki hizo ziendelee kutatuliwa na mzazi wake.

Hivyo, niombe tu Mheshimiwa hili bado tuendelee kulitafutia tena ufumbuzi wa kudumu ili wanafunzi tukijua huyu kapata mkopo basi ajuilikane huyu anao, kwa hiyo mzazi kama ana watoto wawili pengine huyu kabahatika mkopo ajue yeye anadima na huyu mmoja ambaye hajafanikiwa kupata mkopo.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa sio mkubwa sana, mchango wangu ni mdogo sana lakini wenzangu walisema kuhusu upungufu wa walimu na mimi naomba hili nilitie msisitizo kwa sababu kuna walimu ambao walisomea ngazi ya cheti na wamesoma tangu 2007 wapo mpaka hii leo wanaranda mitaani. Mheshimiwa hili ni jambo la kuwafikiria sana hata pale tunapoajiri basi ingelikuwa tunafikiria kuchukua hawa huku kidogo, tukaajiri na hawa wengine wapya kidogo, ili na wao tukawapa moyo asije akaona mtu ah, kumbe kwenda kusoma ualimu ni kupoteza nguvu zako bure halafu ajira hakuna sisi tupo tangu 2007 hatujaajiriwa.

Kwa hiyo, mimi niombe kuthamini kwa sababu hata kile walichokisoma wataweza kupoteza muda umekuwa mwingi sana. Kwa hiyo basi, serikali kwa juhudi zake iweze kuwafikiria hawa na kuwaajiri ili kupunguza hiyo changamoto za upungufu.

Pia nakumbuka kuna changamoto ya upungufu wa walimu wa sayansi, hili ni kweli na serikali imeonesha kila jitihada kwa sababu mmefanya mpaka kutuletea walimu wa Nigeria kwa kuona mnataka kuhakikisha vijana wetu wanaondokana na changamoto hii. Naipongeza serikali kwa juhudi zake hizo lakini bado niombe wizara iangalie kuna vijana wa *Form VI* ambao walisoma, lakini pengine kutokana na uwezo wa kujiendeleza wao wenyewe kuendelea na vyuo kutokana na unyonge au wamekosa mikopo, kwa hiyo wanashindwa kujiendeleza. Lakini hawa walimu huwachukua wakawatumilia katika skuli kuendelea kuwafundisha vijana wetu.

Kwa hiyo, kwa nini serikali isingechukua juhudi za kuwaajiri hawa na wao kwa sababu wameshafika *Form VI.* Hivyo ni vizuri wangewaajiri halafu wangeweza tena kupata hatua ya kuendelea kusoma vizuri na tukaweza kuongeza wale walimu wetu wa sayansi.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu waliopita waliwapongeza sana walimu na mimi nataka nichukue fursa hii kuwapongeza sana walimu wetu. Niwapongeze walimu wote walimu ambao wametufunza *Qur-an* lakini na walimu ambao wametufunza maskulini.

Hawa ni watu wenye kazi moja kubwa sana kwa hiyo serikali niiombe kila mara kuwaangalia walimu katika hali nzuri ya kuwathamini kwa juhudi zao kubwa, kwa sababu kila mtaalamu ametayarishwa na mwalimu. Kwa hiyo, kazi yao inaonekana ni kubwa sana na inahitaji matunzo makubwa ili walimu hawa waweze kuendelea na kazi yao, fani ngumu ya kazi yao lakini kama tutakuwa tunawapa moyo mzuri kila wakati basi walimu wanaweza wakaendelea kufanya vizuri katika kutusomeshea vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka niseme hayo tu machache katika wizara hii, lakini nichukue pia fursa hii kuzidi kuwapongeza sana Wizara ya Elimu kwa juhudi zao

na yale mafanikio yote ambayo wamejaaliwa kufanikiwa. Tunawapongeza serikali kwa hatua hiyo na *inshaallah* shida huwezi ukazimaliza mwanadamu kwa wakati mmoja, shida zinaendelea kuwepo kwa mwanadamu kila wakati.

Kwa hiyo, unapopata lile ambalo moja umeweza kulitatua unapaswa uchukue shukurani kwa Mwenyezi Mungu, tunaishukuru wizara na tunaipongeza na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia kila yale mema ambayo tumeyakusudia tuweze kuyafikia kuyafanya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nadhani kwa sababu mimi sina usemaji sana anaweza akapata na yeye dakika kumi Mhe. Ibrahim Makungu.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai na hatimaye kutupa afya na uwezo wa kutoka katika maeneo yetu hadi hapa, hii ni hazina kubwa aliyotujaalia *Allah* na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze pale alipomalizia Mhe. Panya Ali Abdalla katika suala zima la walimu. Mheshimiwa ili mwanafunzi aweze kujifunza basi anahitaji mambo yafuatayo:

Kwanza mwalimu, pili mazingira ya kujifunza. Kwa hivyo, nianze na hawa walimu.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna watu wanastahiki pongezi katika visiwa hivi na wanaofanya kazi katika mazingira mazito sana basi ni walimu. Walimu wa Zanzibar wanafanyakazi katika mazingira mazito mno na kwa kweli kinachowasukuma zaidi kuendelea kufanyakazi hapa nchini basi ni uzalendo.

Kwa hiyo, nachukuwa fursa hii kuwapongeza sana walimu pamoja na matatizo yaliyonayo katika kazi zao na ugumu wa maisha kuendelea kutufundishia watoto wetu. Kwa hivyo, nawashukuru sana na nawapongeza sana walimu.

Mhe. Mwenyekiti, mwalimu tunaweza kumlinganisha na mfinyazi au sonara. Mfinyanzi unampeleka udogo, hauna matumizi yoyote. Lakini mfinyazi huyo kupitia taaluma yake ya kufinyanga anakutolea mkungu, anakutengenezea nyungu, anakutengeneza kikaango, anakutengenezea mtungi wa kutilia maji na hata chetezo cha kujifukizia udi. Huyu ndie mwalimu umempelekea kitu hakina maana

atakutolea mambo yote haya yenye matumizi mazuri na muhimu sana kama vile chetezo.

Mimi nasikitika sana nashukuru kama Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais mdogo wangu pale Mhe. Mohammed Aboud Mohammed yupo hapa na ananisikia katika hili. (*Makofi*)

Sonara umampelekea kipande kidogo hiki cha dhahabu ambacho hana matumizi yoyote unampelekea dhahabu huwezi kuitumia, unamepeleka sonara na sonara anaifyatua ile dhahabu kukutengenezea pete wanavaa kina mama wanapendeza sana, anakutengenezea mkufu anavaa mama anapendeza na unampenda, anakutengenezea hata kipini kile cha kwenye pua yake, huyo ndie sonara na huyo ndie mwalimu.

Leo sisi inasikitisha sana Mhe. Mwenyekiti, mwalimu mwenye sifa ya mfinyazi, mwalimu huyu mwenye sifa ya usonara kwamba kwa kweli hatuwapi bahashishi yakiwemo mishahara minono pamoja na maposho ya kuridhisha inasikitisha sana. Nimefanya tafiti Mhe. Mwenyekiti, kadhaa kwa hizi nchi zikizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara zile Kusini zilizopo katika Bara Arabu na zile za Ulaya, nikaona walimu wa Zanzibar wako chini kimaslahi katika nchi zote hizo wao wako chini kabisa.

Mimi nili-*play interest*, mwenyewe ni mwalimu tena wa Sanyansi *Biology/Chemistry* . Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa nilifanyakazi Wizara ya Elimu karibu miaka 18 pale nikaona mambo magumu lakini nikafanyakazi kwa uzalendo, nikaingia kwenye siasa siku zile nikafukuzwa kazi.

Sasa hapo ndipo nilioona tafauti ya mwalimu wa Zanzibar na mwalimu wa nchi nyengine. Mimi nikenda kufundisha mashule kadhaa pale Bara, nikafundisha Bopaklai Tanga, *Jabal-hira Islamic centre* , *Bwiru Girls* mwanza, mshahara niliokuwa naupokea pale Bopaklai basi nilikuwa naweza kujilipa miezi mitatu huku nilipokuwa nafanyakazi Wizara ya Elimu, ni tatizo.

Ndio nikasema hawa walimu wetu wanafanyakazi kwa uzalendo tu na ingekuwa si uzalendo ingekuwa tatizo. Mie baada ya kufukuzwa kazi Wizara ya Elimu nimekwenda kule nikaona hasa kwamba kweli watu wanafanyakazi kiuzalendo. Nilipokuwa *Bwiru Girls* nilikuwa naweza kujilipa mishahara mitatu ya SMZ, nilipokuwepo Bopaklai halkadhailika nilipokuwa *Jabal-hira Islamic centre* ndio kabisa karibu mishahara minne, hapa katika kiwango hicho hicho cha elimu nilichokuwanacho.

Sasa jamani ni tatizo na mimi naomba tu kwamba Mhe. Mwenyekiti, na serikali ipo pale Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mhe. Mohammed Aboud naomba kwamba kwa vyovyote vile walimu tuwaangalie. Inasikitisha sana Mheshimiwa kwamba hadi hivi sasa alisema hapa Mhe. Mohammed Mbwana kwamba hadi hivi sasa tangu mishahara irekebishwe walimu hawajapa *area* zao, ukiangali basi ile *bus fare* mtu anakaa miezi mitatu minne hajapata mwalimu kutoka mjini hapa kwenda kusomesha Mkokotoni tena mwalimu mwenyewe mwanamke, humlipi *bus fare* kwa wakati na mwalimu huyu pengine hana mume, unaona anatakiwa ende kazini Mkokotoni akafundishe saa saba katoka shule, saa 9 yuko Mkokotoni na anaitakata Kinuni, hapa ndipo anapokaa tuseme na yuko saa 9:30. Tangu saa 7 yuko Mkokotoni mwalimu huyu mwanamke atakuja saa ngapi kushughulikia familia yake hapa mara moja mwalimu anaweza akaja akajitia katika mambo madogo madogo haya ambayo yana matatizo, hili ni tatizo Mheshimiwa, ni tatizo lazima hawa walimu tuwaenzi, tuwatunze na kuwajali.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali pale angelikuwa si mwalimu angeweza kutufafanulia hapa haya mambo ya sheria humu ndani na Mhe. Mohammed Aboud pale waziri makini na mahiri wa serikali hii, angelikuwa si sisi walimu tuliomfanya akawa hivyo angeweza kweli kufafanua mambo. Lazima muone haya mambo jamani, mimi nilikuwa naona haya nilipokuwa nafundisha Shule za SMZ nilipokuwepo pale Jabal-hira nilipewa suti hizi za kizungu nikapewa na mwambao suti. Mwambao suti unapewa kanzu, unapewa koti, kofia na *sandals* unavaa unaingia pale mwambao suti kwenda kufundisha siku za Ijumaa pale *Jabal-hira Islamic centre*.

Mbali hizo nilizokuwa nikipewa *safari suit* nilizokuwa nikipewa pale hizo za kizungu kama alivyaa Mwanasheria Mkuu wa Serikali niliwahi kupewa tatu pale siku kama wanakuja wageni *official* tunapewa pale. Leo nenda kamuangalie mwalimu wa SMZ umlinganishe na mwanafunzi tu wa waziri Mohamamd Aboud pengine au Naibu Waziri wa Elimu pale. Muangalie mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Vitongoji au Wawi Sekondari au Shamiani nilipokuwa nafundisha pale mimi umuangalie na mtoto wa Waziri wa Elimu. Mimi nina yebo yebo, yeye ana buti. (*Makofi*)

Hebu tunaangalie *Public relation* atakuwa nayo kweli mwalimu, hebu mpandisheni hadhi kidogo mwalimu. Nyie mnazungumza tu ma- *Engineer* tu na watu wengine. Hawa ma- e*ngineer* wasingefika kama si walimu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha zaidi ambalo nitakuja kulitolea ufafanuzi kwenye Mafunzo ya Amali. Kasema hapa Mhe. Panya Ali Abdalla kuna walimu katika Taasisi za Mafunzo ya Amali walikwenda ziara ya kimafunzo mwaka 2014 mwisho mwisho hivi Iran. Nawapongeza sana Mafunzo ya Amali kwa kuweza

kuwapatia mafunzo yale, wakaambiwa kwamba hamna hela na miongoni mwao alikuwa mdogo wangu mmoja pale na yeye anafundisha pale Chuo cha Mafunzo ya Amani Vitongoji nguo ya kutoka akenda Dar - es Saalam hana achalia mbali Iran.

Basi anatakiwa aende Iran na mtumba wa shati na huku kavaa yebo yebo ili mradi Iran huwezi kufika Dar- es Saalam unaona haya je, Iran na huu mtumba akalazimika kuuza vigombe vyake wakaambiwa tu nyie nendeni tu huko pesa hapana sasa hivi, akauza ngombe wake wawili madume akenda tengeneza pale kwamba akirudi atapewa pesa akanunue madume yake aweke inasikitisha sana.

Mimi nilifikiri wameshalipwa laiti kama isingekuwa Mheshimiwa Panya Ali Abdalla alienikumbusha pale niliona kama ningepongeza kwa kulipa kumbe hadi leo hii hawajalipwa hii ni idhilali. Utakapokuja waziri hapa katika kujibu, ili nipitishe bajeti hii lazima unieleze kwamba kama hujawalipa walimu wale wa Mafunzo ya Amali waliokwenda Iran mwaka jana kwa ziara za kimafunzo utawalipa lini. Kwanini hujawalipa na lini utawalipa ndio naweza kupitisha hapa. Lakini kinyume na hapo tutakujabanana hapa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nianze Idara ya Sera na Mipango katika ukurasa wa 5. Mhe. Mwenyekiti, hii idara majukumu yake makubwa ni kufatilia rasilimali na misaada ya wahisani. Rasilimali za wizara pamoja na misaada ya wahisani. Mheshimiwa hivi karibuni hapa moja kati ya rasilimali za wizara ni pamoja na majengo na ardhi ambayo majengo hayo yamo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni wakati mimi ni Mjumbe wa kamati hii ya mambo ya wanawake na watoto mwaka juzi nilipokuwa Mjumbe wa kamati. Katika kutembea na wizara tukaona kwamba kunamzozo baina ya mfanyabiashara mmoja na SUZA *Department* ya pale Nkurumah pale kwamba huyu mfanyabiashara kachukuwa ardhi kamega Nkurumah anasema ni yao. Sasa lile tatizo namuuliza Mhe. Waziri mzozo wa ardhi ulipo baina ya mfanyabiashara na Chuo chetu ya SUZA *Department* ya pale Nkurumah huu umeshatatuka au bado upo.

(b) Hili tatizo la ardhi lililopo vile vile la umiliki wa ardhi baina ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya hapa Mbweni na ile ardhi iliopo karibu na ufukwe hapo. Tatizo hili limeshatatuka nalo au bado mnaendelea kuliachia iendelee kuliachia achia tu waendelee kuchukuliwa ardhi zao wale.

Halafu Mheshimiwa pamoja na nyinyi kumegewa ardhi yetu nyie mna tatizo mnajenga Shule katika ardhi za watu bila ya kuwapa maslahi yao. Hebu nambieni sasa mzozo baina ya Wizara ya Elimu katika Skuli ya Ndagoni mmejenga majengo

katika ardhi si yenu. Je, tatizo lenu nyie na warithi mzozo ulipo baina ya Shule ya Ndagoni na warithi wa Marehemu Ayoub Suleiman ambaye mrithi wake mkubwa ni Suleiman Ayoub Suleiman tatizo hili mmeshalimaliza au bado mnaendelea kukaa na ile familia ikiendelea kunyanyasika tu pale.

Napenda Mhe. Waziri niseme katika hapa unisikilize vizuri mzee wangu pale muasisi mwenzangu pale ni kwamba kiongozi ni Naibu wa Mwenyezi Mungu katika Ulimwengu, uadilifi wake namwakwambia wewe Mhe. Waziri mpenzi wangu na swahiba wangu. Kwamba kiongozi ni Naibu wa Mwenyezi Mungu katika uso wa ulimwengu uadilifu wake unapimwa, tusije tukenda huku mbele ya Mwenyezi Mungu ikawa hamjalitatua hili tatizo la Ndagoni ile ni mali ya watu na hivi sasa kila umuonae mguu majanini, mguu kaburini. Nakuomba Mhe. Waziri hili ulitatue kabla hujenda jibu kwa Mwenyezi Mungu utakuwa "*mas-ul*".

Sasa Mheshimiwa niendee katika Chuo Kikuu cha Taifa, *SUZA, State University*. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nitoe fursa hii kumpongeza sana huyu kijana wetu Profersa Idrissa Rai. Kama kuna kijana makini sana, mahiri na muadilifu sana katika kufanya shughuli zake za kiutendaji na katika kusimamia taaluma katika nchi hii basi Profesa Idrissa Rai. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hapa tulimshauri Profesa huyu na siku za nyuma nilipiga kelele sana na nikaiomba sasa nyinyi serikali mumuwezeshe Profesa Rai kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi kwamba iweze kuanzishwa *Faculty* ya ***Environment*** pale. Kwa hivyo, nashukuru kwamba imeanzishwa *Bachelor Degree in Environment Science*. Kwa hivyo, naishukuru sana serikali kwa kusikiliza ushauri na namshukuru sana Profesa Rai kwa kusimamia ile *Faculy* ya Idara ya Mazingira pale Chuoni.

Sasa mimi napenda sana taaluma ziendane na wakati, huu ni wakati hasa wa kuanzisha ***Faculty* ya** *Environment* pale SUZA muwawezeshe hawa kufungua *Faculty* nyengine muhimu katika nchi mtoe kipaumbele muwe na masikio ya kutusikiliza na kutupima sisi wanasiasa.

Hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kesho kutwa tunaingia katika mambo ya mafuta, tunafanya tafiti za mafuta. Inasikitisha sana kwamba mimi nimefanya sana *study* Vyuo Vikuu vya Zanzibar vilipo ikiwemo SUZA nimefanya tafiti *University of Dar - es Salaam*, *University of Morogoro* nimefanya hata *UDOM*. Nikaangalia ni wanafunzi wangapi Wazanzibari kwa sababu tunataka kuchimba mafuta hivi karibuni eti nikaangalia wanafunzi wangapi Wazanzibari wanaofanya mambo ya *Geology*, wangapi wanaofanya mambo ya *Petroleum Chemistry*, nikaangalia na wanafunzi wangapi Wazanizabari wanaofanya *Excavation of Petroleum* hamna ni wawili tu. Hili ni tatizo Mhe. Mwenyekiti.

Wapo wanafunzi wawili tu ndio wanafanya *Geology* na mmoja anafanya *Geology* pale Mzanzibari pale *University of Dar- es Salaam* na mmoja anafanya *Petroleum Chemistry* pale. Ni tatizo Mheshimiwa. Mimi nasema katika hili Mheshimiwa naomba unilinde kidogo hizi kofi maana nataka kujenga hoja muhimu ambayo itaisaidia serikali. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe muacheni amalize dakika yake moja iliyobakia. Tuendelee.

Mhe. Saleh Nasssor Juma: Mheshimiwa naomba sana kwamba serikali imsaidie Profesa Rai aweze kuanzisha *Faculty of Petroleum Chemisty* pamoja na *Geology* pale kusudi tuweze kutoa wataalamu watakaotusaidia kesho kutwa katika *of Petroleum Excavation*.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie dakika moja kwa Idara ya Mikopo. Kwamba nimpongeze huyu Kurugenzi lakini vile vile awezeshwe. Hii kuchelewa kote ni kwamba serikali inafanya hiyana haimuwezeshi yule kijana ni madhubuti na makini sana, mimi namjua Mkurugenzi kama atapatiwa uwezo huyu wanafunzi hawatayumba hawatababaika awezeshwe ikiwa tunataka kwelai taifa hili liendelee lazima tupate wasoni na wasomi wengi sisi wazazi ni masikini. Lazima wanafunzi wapatiwe mikopo na mikopo haiwezi kupatikana kama serikali haijatoa kipaumbele na kumuwezesha Mkurugenzi kuweza kutoa pesa za kutosha tena kwa wakati ili wanafunzi wetu wasipotee na wale kina mama kule wakaanza kuingia katika mambo haya mabaya.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba aje anieleze Waziri kule Ndagoni wamemaliziana vipi ndio nimuungie mkono hii hoja yake ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano ambayo mmekuwa mkinipa kwa kipindi chote cha toka asubuhi mpaka hivi sasa. Waheshimiwa Wajumbe katika orodha ambayo watu waliomba kuchangia mpaka sasa hivi nimebakiwa na wachangiaji wawili tu ambao watamaliza jioni hii na baadae tutamkaribisha Mhe. Naibu Waziri Elimu, ili na yeye aweze kutoa mchango wake pamoja na kama kuna maeneo ambayo anataka kujibu atamsaidia Mhe. Waziri na hatiame tutamkaribisha Mhe. Waziri kwa ajili ya majumuisho.
Baada ya hayo sasa naomba kusitisha kikao hichi hadi saa 11:00 barabara za jioni hii ya leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Sasa tutamkaribisha Amina Iddi Mabrouk na baadae tutangaza. Tuendelee Mhe. Amina.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii ya leo kuwa mzima, lakini pia nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kumpongeza Mhe. Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa namna wanavyojitahidi katika kuwapatia elimu bora watoto wetu. Baada ya utangulizi huo Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa sana, kwa sababu mengi yameshazungumzwa na sijisikii vizuri sana. Kwa hivyo naomba nichangie mchango mdogo tu lakini nina hakika kwamba utasaidia katika kuimarisha elimu bora ya watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiingia katika kitabu hiki niingie kwenye ukurasa wa 6. Nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuanzisha mradi huu wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi. Mhe. Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba elimu ya mtoto inaanzia pale katika maandalizi. Msingi wa nyumba yoyote, ili iwe nyumba imara basi ipate misingi bora. Na msingi bora wa watotot wetu, ili mtoto awe bora katika elimu hakuna budi basi apate maandalizi bora ya kumfanya awe na elimu bora.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo niingie sasa katika mchango wangu. Nidhahiri kwamba Mhe. Waziri ameeleza hapa katika kitabu chake kwamba mradi huu kwamba mradi huu umechangiwa shilingi bilioni moja nukta.

Mhe. Mwenyekiti, sera hii ya Elimu ya Maandalizi kama ninakumbuka vizuri ilianzishwa kipindi kile ambacho Mhe. Haroun Ali Suleiman alikuwa Waziri wa Elimu. Ninaamini kwamba alifanya utaratibu huu kwa nia nzuri tu na mimi nipongeze skuli binafsi kwa kutekeleza kwa vitendo elimu ya maandalizi. Sote mashahidi tunafahamu kwamba mtoto anapoanza elimu ya maandalizi ni dhahiri kwamba anaendelea kufanya vizuri katika skuli ya msingi mpaka sekondari hadi kufanya mtihani wa *Form IV*. Na ni dhahiri kwamba mtoto anapokuwa hajapata elimu ya maandalizi, kwa kweli si rahisi sana kufanya vizuri labda iwe bahati tu, lakini mara nyingi mtoto anapokuwa hajapata elimu ya maandalizi hawezi kufanya vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba niipongeze tu skuli ambazo ninazozifahamu, kwa mfano Skuli ya Feza ambavyo inafanya vizuri tu katika elimu ya maandalizi na watoto wao wanafanya vizuri kwenye msingi, sekondari hadi kufanya mtihani wa *Form IV*. Lakini pia hata Skuli ya *Glorious* kwa skuli binafsi ninakusudia, pia na wao elimu yao ya maandalizi katika kuwaandaa watoto wanafanya vizuri mpaka matokeo yake skuli ya msingi, sekondari na kufanya mtihani wa *Form IV* wanafanya vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo hii inamaanisha kwamba wenzetu wa skuli binafsi ilipotangazwa hii Sera ya Elimu ya Maandalizi wameitikia wito, na mimi nichukue nafasi hii kupitia Baraza hili tukufu kuwapongeza sana skuli za binafsi. Lakini nije kwa upande wa Serikali ambayo Serikali yetu hii ndiyo iliyoanzisha Sera ya Elimu ya Maandalizi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba kwa mtizamo wangu bado hatujawa tayari katika kuimarisha elimu hii ya maandalizi. Ninasema hivi kwa sababu, katika kitabu cha Mhe. Waziri ametuonesha hapa pesa ambazo zimetengewa ni jumla ya bilioni moja nukta tatu lakini pesa za Serikali ambazo zimepangiwa ni milioni mia moja. Na Mhe. Waziri katika kitabu chake ametwambia kwamba pesa ambazo zimetakiwa kutolewa na Serikali hadi leo hazijatolewa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi niseme ni kweli tupo *serious* katika kuimarisha elimu hii ya maandalizi ya watoto wetu. Kwa sababu hapa ndiyo kitovu cha watoto wetu, hapa ni msingi na maandalizi mazuri ya watoto wetu. Sasa tutakapoona katika kitabu hichi kwamba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, pesa ambazo zilitakiwa zitolewe ni milioni mia moja, lakini tunaambiwa kwamba pesa hizi hazijatolewa. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana na pesa ambazo zimetakiwa kutolewa na wafadhili wametoa asilimia 4.7.

Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba hawa wafadhili wetu ambao tunawategemea, kwa hali kama hii ni kuwa kwa kweli tunawavunja moyo sana. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, abwebwae hujikaza. Sasa kama sisi wenyeji ambao wenye uchungu mzazi kwamba pesa ambayo umetakiwa utoe hukutoa hata shilingi, kwa kweli hata wafadhili hawawezi wakatusaidia. Kwa hivyo, mimi nimuomba Mhe. Waziri kwa kweli tujidhatiti katika hili na sera hii tumeiangalia wenyewe Serikali, Wizara ya Elimu ni aibu kwamba pesa ambazo zimetakiwa kutengewa katika mradi huu wa elimu ya maandalizi kwamba Serikali haijatoa kitu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika mchango wangu nije katika ukurasa wa 25, "Vituo vya Kujiendeleza". Mhe. Mwenyekiti, mimi nipongeze sana Wizara kwa kuona kwamba ipo haja ya kuvitayarisha na kuviandaa vituo hivi vya kujiendeleza, ili watoto wetu wale ambao hawakubahatika kufaulu basi wasikae nyumbani tu au

kudhurura ovyo, basi wawatafutie elimu mbadala, ili waweze kujiendeleza. Mimi nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kuipongeza Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho kimenishitua sana kuona kwamba hii idadi ambayo ya wanafunzi waliokuwa wamejikusanya wamesajiliwa katika vituo mbali mbali Unguja na Pemba ni 4,658 na wale ambao wamefanya mitihani ya faragha ya Kidato cha Nne ambao wanafunzi 1,391 ni sawa na asilimia 40.6 ndiyo waliotahiniwa na wote wamefaulu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nikiingia katika wanafunzi ambao wamefanya Kidato cha Sita; wanawake ni 403 na wanaume 342, watahiniwa 217 ambao ni sawa asilimia 29 tu ndiyo waliofaulu. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninadhani ipo haja maalum ya kukiangalia kituo hichi ili hawa wanafunzi wetu waweze kufanya vizuri sana. Kwa sababu mimi ninaamini kwamba lengo ya vituo hivi siyo kuwa mwanafunzi tu apate cheti, lengo kuu ni mwanafunzi ambaye yupo *Form VI* aweze kufanya vizuri na aweze kuchaguliwa kuendelea na Chuo. Lakini na huyu mwanafunzi ambaye wa *Form IV*, lengo kuu siyo kupata cheti tu bali ni kufaulu na kuendelea *Form V*.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, si hilo tu na ukiangalia hawa wanafunzi wetu wameshasoma mwanzo, wamesoma mwanzo wanafunzi hawa na wamefanya mitihani na kwa bahati mbaya walishindwa kufaulu. Kwa hivyo vilivyoanzishwa vituo hivi, mara ya pili wakasomeshwa na wakaweza kufanya mtihani. Sasa cha kusikitisha kwamba wamesoma mara mbili na wamefanya mitihani mara mbili lakini haya matokeo ambayo tunayaona hapa, kwa kweli si mazuri sana. Kwa hivyo mimi nimuomba Mhe. Waziri bado ipo haja ya kuchukua bidii za makusudi kuhakikisha kwamba hivi vituo vyetu vya kujiendeleza, basi wanafunzi wetu angalau wapasi kwa asilimia kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa wa 21.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Nitazungumza haraka haraka.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kushirikiana na mashirika mbali mbali katika kuendeleza mafunzo kazini kwa walimu wa ngazi tofauti ili kuinua uwezo wao wa kufundisha masomo ya hesabati na masomo ya sayansi. Mhe. Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba tulikuwa tuna kilio kikubwa kwa hapa kwetu Zanzibar cha upungufu wa walimu wa hesabu na sayansi. Kwa hivyo ninaamini kuanzishwa kwa mashirika haya tofauti, nina hakika kwamba

walimu wetu watakuza kiwango chao cha elimu katika masomo haya ya sayansi na hesabati.

Kwa hivyo mimi nimuombe Mhe. Waziri wazo hili lisiwe katika vitabu tu, basi ufuatiliaji ni jambo la msingi katika kuhakikisha kwamba hawa walimu wetu wanapata elimu ambayo imekusudiwa, ili na watoto wetu waweze kupata hiyo elimu bora ya masomo ya sayansi na hesabati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa umenipa dakika chache tu basi niseme kwamba ninaipongeza sana Wizara kwa namna ya maelezo yao katika kitabu hichi na ninaamini kwamba kama yatafuatiliwa haya yaliyokuweo kwenye kitabu hiki, basi ninaamini kwamba watoto wetu watapata elimu bora ambayo iliyokusudiwa.

Baada ya hapo nichukue nafasi hii kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kuwashukuru wale wote ambao wameandaa kitabu hichi, naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa anayefuata Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana ninakushukuru. Mimi kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kufika hapa jioni hii sote tukiwa katika hali ya uzima na afya njema. Pia nikushukuru Mhe. Mwenyekit, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusu Makadiro ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2015/2016.

Kwanza nimpongeze kwa dhati kabisa Kamati hii imefanya kazi nzuri na hasa nimpongeze Mwenyekiti na Wajumbe kwa kuwasilisha hotuba yao nzuri kabisa, hasa msomaji wetu wa leo alikuwa; msomaji Mhe. Hassan kaisoma kwa aina yake. Kwa kweli ninawapongeza sana Mhe. Mwenyekiti, kwa juhudi zao walizotuonesha Wajumbe hawa wa Kamati. Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua sekta hii ni muhimu sana kwa wananchi wetu hasa kwa sababu elimu ni ufunguo wa maisha wa binadamu kwa kweli. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze katika ukurasa wa 4 kwenye Kifungu nambari 10, "Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano (2010-2015)". Mhe. Mwenyekiti, mimi ninampongeza sana Rais wa Zanzibar kwa dhati kabisa, wala sibabaishi. Mafanikio yaliyopatikana katika miaka mitano hii na Mhe. Waziri katwambia kwenye kitabu chake hichi. Maana yake nikiyazungumza hapa siyamalizi Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, ninampongeza sana Mhe. Waziri kwa kutuandikia yote yale ambayo yaliyofanyika na mimi nimeyafanyia utafiti, kweli yote yamefanyika katika kipindi cha miaka mitano mpaka kumi Rais wetu wa Zanzibar kwa Awamu yake hii ya kwanza kafanya mambo haya kweli. Mimi ninampongeza sana Mhe. Mwenyekiti, na hasa sekta hii ilivyokuwa muhimu na uzito wake kwenye jamii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niseme pia ongezeko la uandikishwaji wa wanafunzi katika elimu ya lazima ya maandalizi ya msingi na sekondari, kutoka wanafunzi laki tatu, kumi na saba na kidogo kwa mwaka 2010 na kufikia laki tatu karibu na tisini kwa mwaka 2012. Hili ni ongezeko kubwa sana kwa wanafunzi Mhe. Mwenyekiti, kwa kila mwaka na ninaamini yanaongezeka kwa kuhamasika kujua umuhimu wa elimu kwenye jamii yetu na watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme hasa hili suala la elimu ya lazima ya msingi. Hii ni elimu ya lazima na lazima kweli. Mimi nimefanya utafiti kweli kweli Mhe. Mwenyekiti, na ukiangalia elimu ya lazima ya msingi hasa kwa mtoto; mtoto kuanzia miaka minne na kuendelea ndiyo akili inafunguka kujua maeneo husika, kujua kuzungumza na kujua uelewa mzima wa maisha yake.

Mimi niseme Mhe. Mwenyekiti, bila ya kujenga msingi huwezi kujenga nyumba nzuri. Kama msingi utakuwa mbaya basi hata hiyo nyumba itakuwa haina umadhubuti huo. Kwa hivyo elimu ya msingi ni muhimu sana kwa mtoto, akianza vizuri chini na huko juu anamalizikia anakwenda kuwa vizuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na niipongeze sana Serikali kwa kufunguliwa Chuo Kikuu Cha Taifa cha Zanzibar huko Tunguu, kumepelekea kuongezeka kwa wanafunzi, 1205, mwaka 2010 hadi wanafunzi 2538, kufikia 2015, na nimesema utawala Dkt. Shein umefanya kazi kubwa kweli kweli Mhe. Mwenyekiti. Waswahili wanasema, "Mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni".

Kwa hivyo mimi ninasema ninampongeza sana, kwa sababu utafiti niliofanya ni kweli na nimechunguza na nimeangalia, nimesoma kitabu vizuri, nikisema uzuri wa kitabu hichi simalizi mpaka kesho. Kwa hivyo, mimi ninampongeza sana Mhe. Rais kwa juhudi zake na ninaamini miaka mitano mengine inayokuja anayoendelea Dkt. Shein, namuomba aendelee basi tutafika mbali kwa mafanikio ambayo anatarajia yeye mwenyewe na sisi tunamtegemea yeye. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niendelee pia kuangalia kitabu hiki na kuipongeza Serikali kwa kukamilika kwa ujenzi kwa skuli mpya 19 za sekondari za kisasa kwenye maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Ninasema maskuli 19 kwa majimbo mbali mbali lakini Mhe. Mwenyekiti, nipongeze sana maeneo ambayo skuli zenyewe zilizojengwa hizo 19 zimeshaanza kazi, siyo kama kuna maneno tu lakini kazi

imeshaanza. Ukiangalia skuli moja wapo ambayo ipo hapa Kiembesamaki hapo barabarani. Kwa kweli ni skuli nzuri na imeshaanza kufundisha wanafunzi vizuri. Kwa kweli ni jambo la kujipongeza na kupigiwa mfano kwa Serikali yetu hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika ukurasa wa 7; hapa nimesema kwamba skuli 19 zimejengwa kwa Serikali na kwa kweli ni jambo la kupigiwa mfano na zuri na mimi sina mashaka nalo, wala sina la kusema ni kupongeza tu. Ninajua jitihada zitaongezeka za kuongeza skuli nyengine pia. Lakini pia jumla ya madarasa 125 yamekamilika, kati ya hayo 79 yapo Unguja na 46 yapo Pemba, na ukarabati wa madarasa 35 ya skuli 7 za Unguja na madarasa 24 kati ya skuli 3 za Pemba umekamilika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninapongeza na ninashukuru sana na nimesema mwanzo, mimi kitabu hiki sina mashaka nacho kusema kweli. Mhe. Waziri mimi ninakupongeza kazi yako ni nzuri, tena ni nzuri sana na siyo kama nzuri ya kubahatisha. Ukitazama miaka mitano ya nyuma na hivi sasa tupo mbali.

Mimi niseme Mhe. Mwenyekiti, mimi miaka miwili na nusu niliwahi kufika Pemba katika Kamati yetu ya Mawasiliano na Ujenzi, kipindi kile nilikuwa na Mwenyekiti wangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk tulibahatika kwenda Pemba sisi kwenye kazi ya Kamati. Nikafika skuli moja ya Kengeja pale Mtambile. Mhe. Mwenyekiti, miaka miwili na nusu ninasema au mitatu, basi skuli ile mimi nilivyoiona machozi yalinitoka. Watoto kwanza wanakaa chini Mhe. Mwenyekiti, ile *floor* ukiona huwezi kuamini, kama wamekaa juu ya mawe wale watoto. Yale madarasa yote ukitazama mabati matupu, siyo kama kuna makuti pembeni, juu mabati, pembeni pia ni mabati. Kwa hivyo, ni joto la kweli kweli Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mimi nimesema mwanzo mafanikio haya, kwa kuliona hili ninaipongeza tena Serikali kwa sababu jambo lililopo lakini Serikali ijitahidi, matatizo ya skuli na hatua nimeziona skuli zilizojengwa tisa mpya, madarasa nimesema hapa ni sabini na tisa, moja ishirini na tano. Kwa kweli ni wa kupigiwa mfano kweli kweli kwa kuondosha zile kero za wananchi wetu na kuwaondoshea usumbufu na mifano tunaiona na mimi mwenyewe nimeona na hali iliyokuwa nayo sasa hivi, tofauti inazidi kuendelea kila siku. Kwa hivyo, ninaipongeza Serikali kwa jitihada zake hizo kubwa za kuwaondoshea wananchi usumbufu na kuwapa maisha mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee tena katika suala hili la Skuli ya Kengeja, tuone hali ya wanafunzi wanavyokaa, mbali ya skuli nyengine lakini mfano huu nilikwenda Pemba, wacha hapa, lakini Pemba nilikwenda nikaona. Lakini sasa serikali imesema hapa kwamba Pemba skuli 46, Unguja 79, 37, 7 za Unguja na Pemba.

Kusema kweli ni jambo la kupigiwa mfano, serikali yetu inaangalia sana hasa hali za watoto wetu wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na suala jengine, hili pia ni la kupigia mfano kwa serikali yetu imejitahidi, jumla ya seti 3,187, viti na meza imeweza kutekeleza katika skuli zetu ili wanafunzi wetu waweze kukaa. Pia, madawa 3,490 yamechongwa na kusambazwa katika skuli za msingi za Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba serikali inajitahidi kwa maana yangu, sio kama nasema tu. Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni nilikwenda katika Skuli ya Kibweni kama miaka miwili na nusu hivi. Skuli ya Kibweni maandalizi ya wanafunzi wadogo, wanakaa darasani wanafunzi 130, Mhe. Mwenyekiti, darasa dogo wanafunzi wengi, hata yule mwalimu pale mbele hana nafasi, inatia huruma kwa wanafunzi wetu. Lakini serikali kwa jitihada zake na juhudi zake, mimi naipongeza kwa kuona suala hili umuhimu wake wa kujenga majengo na watoto wetu hawa wakaweza kukaa vizuri.

Pia, Mhe. Spika, nataka niseme hapa katika jimbo langu kwenye Skuli ya Bububu, kuna matatizo sana kwa wanafunzi wetu. Kwa kweli kila siku zikienda mbele wanafunzi wanakuwa wengi, lakini serikali inajitahidi hatuwezi kuitoa shukrani. Nilisema mwanzo kwamba "Mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni". Serikali inajitahidi, Rais wetu anajitahidi sana. Ukitizama juzi juzi kuna madarasa kama matatu yanakaa chini ya mwembe wa Jimbo langu la Bububu, wanasoma darasa la kwanza hapa na la pili hapa, madarasa matatu yanakaa chini ya mwembe. Yote hayo ni kwa sababu ya udogo wa eneo la maskuli yetu, lakini serikali inajitahidi sana.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri, kama huu mradi umebakia basi namuomba anijengee skuli moja Kisasa pale Bububu kwenye jimbo langu, Bububu skuli kuna eneo kubwa sana kule nyuma, lakini skuli iliyopo pale ni ndogo, yaani madarasa kidogo. Kwa hivyo, naomba lile eneo Mhe. Waziri hebu nisaidie nakuomba kwa heshima zote, unijengee skuli moja ya kisasa kama ile ya Kiembe Samaki hapa. Nasema hivi Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu skuli ile ya Bububu wanasoma wanafunzi kutoka Mtoni, Mfenesini, Dole na kutoka Bububu yenyewe wote wanakuja pale na wamejaa wengine wanakuja mjini na wanaokuja mjini ni wengi sana Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, naomba sana tuangalie kwa jicho la huruma skuli moja hii ya kisasa, Mhe. Waziri, naomba tuijenge pale katika Jimbo la Bububu, pale Skuli ya Bububu niongezee skuli ya kisasa.

Mhe. Mwenyekiti, nianze katika ukurasa wa kwanza wa kitabu hiki cha waziri wetu kwa hotuba yake hii nzuri sana, kifungu cha 28. Jumla ya walimu wetu 1,372 Unguja peke yake 778 na Pemba 594, kwenye vyeti na uzoefu mkubwa wanao

hawa walimu wetu, uzoefu wa kazi pia wanao usiopungua wa zaidi ya miaka 30 na hawa hasa ni walimu wenye uzoefu huo, miaka 30 sio kidogo. Katika miaka hiyo unaweza ukazaliwa ukazaa na ukasahau kama uliowa na una mtoto keshakuwa mkubwa, miaka 30 ni mingi Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, hawa walimu wetu wana uzoefu kweli kweli. Lakini pia niipongeze serikali kwa kuwafanyia marekebisho mishahara yao, zilitumika karibu jumla milioni 513 zilitumika katika kuirekebisha mishahara yao na shilingi milioni 156 ilitumika kwa kuwalipa posho zao.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niseme mimi naipongeza serikali, wala sitowi makosa, najua inajipanga kila siku ukitokea uwezo inajipanga serikali yetu. Juzi hapa tulisikia bajeti ya Wizara ya Fedha ilijipanga kuwalipa wazee wanaotimia miaka 70, hiyo ni hatua nzuri sana naipongeza. Lakini mimi namwambia Mhe. Waziri, kwamba pamoja na kujitahidi kuwaongezea mishahara na fedha zimetumika nyingi, lakini bado hali za walimu wetu ziko dumu, niseme ukweli, ziko duni Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, hata juzi nilisema hawa walimu wetu hata usafiri hawana, nyumba zao wanazokaa zina mashaka, huu mshahara kwa kweli haukidhi hasa mahitajio yao yote wanakuwa na hali ngumu ya kimaisha. Lakini mimi nilisema juzi hapa katika Wizara ya Afya, na leo narudia tena leo hapa. Hawa walimu na madaktari tuwaangalie sana Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema hapa kwa kupitia benki yetu ya *PBZ*, iwaangalie walimu iwakopeshe, iwajengee nyumba, iwakopeshe kwa mkopo nafuu walimu wetu hawa, iwakopeshe gari au vespa. Lakini vespa sitaki kusema tena leo kwa sababu nimeona kitu kimoja, Mhe. Makame Mshimba, leo kasema asubuhi hapa, walimu wetu wakipanda vespa itakuwa sasa hivi hatari, wale waendesha vespa wa tako moja wana hatari. Mimi sipendelei tena sasa hivi hawa walimu wetu wapande vespa, kweli vespa inatisha sasa hivi. Kwa hivyo, mimi naomba sana serikali iangalie kuwapatia usafiri wa gari kwa mkopo nafuu walimu na madaktari, suala la nyumba na kipando kwa usafiri ni muhimu sana kwa walimu na madaktari wetu wakopeshwe mkopo nafuu kwa kupitia benki, halafu ule mshahara wao ukatwe kidogo kidogo ili wawezeshwe hawa.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa nini, kwa sababu ukiangalia, nilisema juzi mfano madaktari wanasomeshwa katika serikali hii hii wanapelekwa nje kusoma, wakirudi hapa na wakipata maslahi makubwa zaidi Bara, basi wanakwenda kufanyakazi Tanzania Bara. Ukiangalia walimu pia wana uzoefu mzuri walimu wetu, tena wana vipaji kabisa walimu. Naweza kutoa mfano mimi Mhe. Mwenyekiti, lakini wanawacha kazi ya ualimu, wanakwenda kufanyabiashara, wanakwenda kufanyakazi nyengine ambayo sio taaluma yao inavyoielekeza.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nitowe mfano mzuri. Mimi nilikuwa na mwalimu wangu kanisomesha Mwalimu Sanya Mbunge wa Mji Mkongwe aliyekuwa, ni mwalimu mzuri sana wa *Geography*, namshukuru sana mwalimu yule alinisaidia sana kwa upande wa *Geography* sana nilipokuwa *Form Two* katika Skuli ya Haile Selassie, alikuwa hodari na anakipaji kwa *Geography* Mwalimu Sanya. Lakini alipoona maslahi madogo akenda katika vyama vya siasa akagombania Ubunge.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana hii hali tuiangalie kwa walimu wetu wasitoke kwenye fani. Wapo walimu wengi wazuri wametusomesha na wametusaidia mpaka tumefikia hapa leo hii tunawashukuru, bila wao leo tusingefikia hapa, haya maendeleo tusingeyapata bila ya wao. Lakini wamejituma, wametusomesha vizuri kwa moyo wao wa dhati kabisa, kwa imani yao wakijua sisi tutakuja kuitumikia nchi hii. Kwa hivyo, mimi naamini kabisa kwa kazi waliyoifanya hata Mwenyezi Mungu atawalipa. Lakini tuangalie maslahi yao, kwa sababu wasije na wao walimu waliokuwa na uzoefu wa miaka 30 wakajakuondoka wakenda kwenye fani nyengine ya siasa au ya biashara au mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tatu za ziada.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Kwa hivyo, naomba sana tuangalie maslahi yao tuwapandishie siku baada ya siku, basi mishahara yao na posho zao zizidi, hasa hawa walimu na madaktari tuwatizame sana kwa jicho la huruma sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika ukurasa wangu wa 15 wa kitabu hiki, kifungu cha 14. Kwa kweli mimi nampongeza Mhe. Waziri na namshukuru sana katika kitabu hiki na kwa juhudi zako. Kwa nini nasema hivi, katika ukurasa wa 15, ninukuu kidogo hapa;

Kifungu cha 14;

"Elimu ya madrasa ya vyuo vya *Qur-an*, idara imeshughulikia jumla ya vyuo vya *Qur-an* 2,296".

Kwa kweli Mhe. Waziri, nakushukuru kwa kuwaaangalia hawa na kuwaona hawa vyuo vya *Qur-an* na kwa umuhimu wao mkubwa hawa walimu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuhusu hawa walimu wa madrasa ni muhimu wana na wanafanyakazi kubwa ni lazima tuwaangalie vizuri. Lakini yeye Mhe. Waziri, kasema anawashughulikia, lakini anawashughulikia kwa kuwapa mafunzo. Mafunzo walipewa sawa, lakini naomba sana uwaangalie japo kwa pesa kidogo ya sabuni, kwa sababu unasema kuna vyuo 2,296. Sasa sijui kuna walimu wangapi,

hawapungui walimu 4,000 wanaweza kufika. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri, uwaangalie kuwalipa walimu hawa, kwa sababu kazi wanayoifanya walimu hawa ni kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwenye jimbo langu ukitembelea kuna vyuo, madrasa zile hazipungui 58 au zaidi. Lakini ukiwatizama watoto wanaosoma Mhe. Mwenyekiti, ni mpaka nje. Maana yake ukenda wakati wa mchana kwa kweli wanatia huruma, wengine wanasoma ndani na wengine wanasoma juani wanapigwa na jua. Lakini kwa sababu uwezo na fedha inakuwa tabu kuweza kuwajengea, kwa hivyo, tunawacha hali iende hivyo, lakini kwa kweli inauma sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona na hawa walimu wanafanyakazi kubwa sana ya kuwasomesha watoto wale wadogo wa si chini ya miaka 4 kwenda juu, wana kazi kubwa. Mhe. Mwenyekiti, tuseme ukweli. Mimi nikipewa mtoto mdogo wa miaka 2 nikae naye kwa siku moja tu au masaa tu nitashindwa siwezi kumshughulikia yule mtoto, kuanzia miaka 3 au mpaka 4 kukaa naye tu basi yale mashughulikiaji yake ili niweze kumuelekeza basi itakuwa tabu. Sasa sikwambii hawa walimu wana wasomesha watoto zaidi ya 100, hawa walimu wetu wa madrasa tuwapongeze sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, akija aniambie kawafikiria vipi hawa walimu wa madrasa kuwalipa japo pesa ya sabuni kidogo wapate kwa siku zinavyokwenda na alivyojipanga kuwaangalia, kwa sababu ukiangalie ana vyuo karibu 2,296, sasa kajipanga vipi ili japo pesa ya sabuni kwa walimu wetu wapate hasa kwenye vyuo vya madrasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la michezo. Zamani ukiangalia michezo ilikuwa muhimu sana kwenye skuli zetu. Mimi nakumbuka nilikuwa nasoma Skuli ya Haile Selassie pale, tulikuwa tuna michezo ya kila aina pale; michezo ya mpira wa *football, basket ball, netball* na michezo mingine tofauti ya riadha na kadhalika. Lakini kwa kipindi hiki Mhe. Mwenyekiti, imeshuka sana, wala husikii na ukitizama sasa hivi mpira wa *basket ball, football ball* na mingineyo ni ajira kwa kifupi kwa vijana wetu. Sasa sijui Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili-*drop* kwa kiasi fulani na kwa fulani ikawa sekta hii imetupwa.

Lakini katika kitabu hiki niliposoma vizuri Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze Rais wa Zanzibar tena kweli kweli, maana yake umpongeze mtu kwa vitendo na sio kwa maneno, lakini nampongeza kwa vitendo kwa kazi aliyoifanya. Kwanza ukitizama hapa kaunda hii Idara ya Michezo, Utamaduni ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, inaitwa UMISETA hii. Ukitizama sasa hivi wako Mwanza wanashindana kwa ngazi ya sekondari. Kwa kweli Mhe. Rais, kafanya kazi kubwa kwa kuiona sekta hii muhimu.

Mimi nasema hivyo, kwa sababu nilipokuwa *Form Two* nakumbuka pale Haile Selassie tulikuwa tunacheza mpira. Alikuwepo mchezaji mmoja anaitwa Dua Said alikuwa Small Simba alitokea pale Skuli ya Haile Selassie. Lakini mwanzo tulipokuwa tunacheza timu za skuli, kwa bahati kipaji kilikuwa kikubwa mchezaji yule akenda mpaka sehemu kubwa kubwa za kimataifa. Kwa hivyo, huu uwezo wa vipaji vipo kwa wanafunzi wetu, lakini tukiwaanzisha tangu chini. Mhe. Rais, kaliona hili na keshaanza na nimpongeze kabisa kwa kutilia muhimu wake katika suala hili.

Vile vile, kamchagua Mkurugenzi makini kabisa wa Idara hii ya Michezo ndugu yangu Hairala, huyu ni mtu makini na hii kazi anaiweza na anaijua. Kwa hivyo, mimi nampongeza kwa uteuzi wake Mhe. Rais, kwa sababu kafanyakazi nzuri kwa kujua huyu mtu wa makini kufikisha yale malengo ya mashindano yetu, ili aweze kwenda kuzuru kwa watoto wetu na hivi sasa mashindano haya wanafunzi wetu wako Mwanza, wanafunzi wetu 120 kwa timu zetu 8 wanashindana kule kwa ngazi ya Sekondari.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie mwisho kuhusu hili suala la usafiri wa wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda wako umemalizika.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Hili suala la usafiri Mhe. Mwenyekiti, linaumiza kweli kweli wanafunzi wetu wanapata tabu sana kwa usafiri. Kuna baadhi ya watu naomba sana, wanajaribu kupotosha watu au kuharibu *mind set* za watu, hili suala la usafiri. Mimi mfano mmoja nawachukua wanafunzi wangu kila siku asubuhi, mchana na jioni. Lakini changamoto kubwa napata, lakini kuna watu wanasema, kwa sababu sijui ni kwa siasa au vipi. Hoo! utafanyakazi hii kwa muda wa wiki 2, 3, mwezi utachoka. Mhe. Mwenyekiti, mimi sichoki kwa kazi ile. Kwa nini nasema sichoki, kwa sababu ile kazi ni kubwa na ile kazi Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanyakazi kubwa ya kujenga maskuli haya.

Kwa hivyo, mimi naona uchungu sana wanafunzi wangu hawawezi kufika skuli na wanafunzi hawa Mhe. Mwenyekiti, ni wa Taifa, wakisoma leo kama nilivyosoma mimi kwa serikali hii bure sijalipa pesa, sijalipa pesa za *uniform*, sijalipa mabuku. Mhe. Mwenyekiti, mabuku tulikuwa tunapewa bure skuli. Lakini hawa wanafunzi mimi nawachukua kwenda skuli na kuwarejesha ile ni fadhila ya serikali yangu iliyonisomesha mimi na mimi kuwasomesha wale nalipa fadhila ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hawa wanafunzi nataka wasome wawe wanafunzi wa Taifa la kesho. Kwa hivyo, suala hili sio langu mimi binafsi, hili suala ni letu sote, wanafunzi hawa wakisoma watakuja kutusaidia sisi wenyewe. *(Makofi)*

Kwa hvyo, naomba haya mambo wasipige vita, nawaomba tushirikiane haya masuala ya usafiri yaende vizuri na hawa wanafunzi wetu wafike skuli kwenda nakurudi. Mimi inaniuma sana mtu kupiga vita suala kama lile, atizame mtu katoka wapi yeye. Mimi naishukuru serikali yetu sana ilinipa mabuku bure kusoma, elimu bila malipo. Mimi nimesoma Skuli ya Rahaleo, nimesoma Skuli ya Migombani pale, nimesoma Skuli ya Tumekuja, nimesoma Skuliya Haile Selassie bila ya malipo yoyote Mhe. Mwenyekiti, sikumbuki mimi kulipishwa hata shilingi 10,000 ya skuli, *uniform* sikumbuki kununua mimi skuli, napewa kitambaa cha suruali, cha shati na mabuku. *(Makofi)*

Sasa leo serikali yetu inajitahidi kama hivi, kwa kweli tuiopongeze na sisi tutowe michango yetu kwa watoto wetu hawa wadogo wasa, tuwasaidie ili wafike skuli salama waende na warudi, tusitie utashi mambo mengine ili kuweza kuwasaidia watoto hawa waweze kuwa viongozi wa Taifa letu na kuweza kuongoza nchi hii. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mimi nakushukuru sana na naipongeza sana wizara kwa kitabu chake hiki. Mhe. Waziri, hotuba yake hii, naionga mkono mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Bububu kwa asilimia mia kwa mia hii bajeti. Kwa hivyo, nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Elimu. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa kuendelea na shughuli zetu kwa amani na utulivu, pamoja na kumshukuru Mhe. Waziri, kwa mipangilio mizuri ya shughuli za elimu ambazo anaziendeleza, pamoja na wafanyakazi wa chini yake ambao wanamsaidia shughuli zake za kazi.

Kwanza, Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu nianze katika ukurasa namba 15 kuhusu Idara ya Elimu ya Maandalizi ya Msingi. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ndio yenye jukumu kubwa kuhusu kuwashughulikia vijana wetu, hasa kuhakikisha kwamba vijana wote wanakwenda skuli kwa wakati na wanapata mambo yote yanayohitajika katika wizara ile.

Mhe. Mwenyekiti, namkumbusha Mhe. Waziri, kwamba hivi sasa katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, vijijini kuna matatizo makubwa sana kuhusu vikalio kwa Skuli zetu za *Primary*, pamoja na vyuo vya *Qur-an*. Kwa kweli Mhe. Waziri, juhudi hizi angejitahidi sana ili kuhakikisha kwamba Skuli za *Primary* zinapatiwa vikalio kwa wakati. Hivi sasa ukienda katika madarasa ya *Primary,* wengi wao wanafunzi wanakaa chini, wanapokaa chini basi wengi wao utawakuta nguo zao zimechafuka pamoja na wao wenyewe, hivyo hawapendezi kama ilivyotegemea serikali.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, afanye juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba vikalio vinapatikana, hasa katika skuli zetu za *Qur-an*, huko ndio kabisa wanapata matatizo makubwa. Mhe. Mwenyekiti, ningemshauri angalau mazulia yangepatikana katika hizo skuli za Kurani zikasaidia hasa vijijini. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, akija atuhakikishie ni lini ataweza kufanya juhudi hizi ili akahakikisha kwamba skuli zetu zinapata vikalio kwa wakati na vya kutosheleza katika skuli zetu. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa sana ambalo linaendelea na hatuelewi litakwisha lini.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nichangie katika ukurasa wa 36 kuhusu Vyuo Vikuu. Vyuo Vikuu hivi sasa viko nje ya mji na utakuta sehemu kubwa ambazo hazina madakhalia ya kukalia wanafunzi, ambayo ya kuweza kulala dakhalia hazipo. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri, atowe juhudi za makusudi ili vyuo vyetu viweze kupata madakhalia mengi ya kutosha ili vijana wetu wapate kulala mule mashuleni, ili waweze wakati mzuri wa kuweza kujisomea.

Hata hivyo, kama madakhalia bado yana matatizo, basi ahakikishe kwamba usafiri unapatikana kwenye Vyuo Vikuu. Utakuta hivi sasa tuna miaka mingi ambayo tumejitawala, lakini utaona mwanafunzi wa Chuo Kikuu utamkuta Mwanakwerekwe anasubiri gari kwa masaa matatu hajafika katika skuli ambayo amepangiwa. Skuli nyingi ziko nje ya mji, utakuta Tunguu Kibele, utamuona mwanafunzi yule anapapatua mwisho anapata gari la mchanga ama gari la mawe ndio anakwenda skuli Chuo Kikuu. Hii ni aibu sana. Kwa hivyo, iko haja Mhe. Waziri, akafanya juhudi ya makusudi kuhakikisha kwamba vijana wetu wanakwenda skuli kwa wakati, badala ya kukosa dakhalia za kulala katika mabweni yao ili wahakikikishe kwamba tunakwenda katika Chuo Kikuu kuhakikisha kwamba ndio maendeleo ya nchi yoyote kwamba wanafunzi wa Chuo Kikuu wanahakiksha wanatunzwa na mtunzaji sio sisi tulioko nje isipokuwa mwenyewe Mhe. Waziri na viongizo wake wahakikishe wanapanga mipango mizuri kuhakikisha kwamba gari zipo za kutosha ili wanafunzi kufika Chuo Kikuu kwa wakati.

Hiyo itasaidia sio kwamba wanafunzi wale wanakwenda chuo sio kwamba wanajitolea bure hata kujitolea kwamba walipie, lakini ziweko gari makusudi tena za kisasa ambazo zinaweza kuwachukua wanafunzi kwenda na kurudi ingawa kwa malipo, lakini utakuta kwamba mwanafunzi anafika saa nne hajapata usafiri na kule masomo yameshakwenda kwa wakati unakuta anafika Chuoni masomo ambayo amepangiwa yeye hayapati tena. Hivyo, namshauri Mhe. Waziri, ahakikishe anapokuja kututolea maelezo atueleze ni lini ataweza kuhakikisha

kwamba Wizara yake imeweza kuhakikisha kupata usafiri kwa wakati kwa wanafunzi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu naingia ukurasa wa 35 kuhusu taasisi za Elimu ya Juu. Kwa kweli vijana wetu wengi wana bidii ya kusoma, lakini wanapofika Elimu ya Juu ili wahakikishe masomo yao yanakwenda kwa wakati ndio mwanzo wa kushindwa kusoma, kama ndio mwanzo wa kushindwa masomo, kwa kweli Mhe. Waziri, atueleze kwa nini wanafunzi wengi wanashindwa kupata mkopo ambao ni juhudi ya Waziri mwenyewe ahakikishe kwamba mkopo unapatikana kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu ili tuhakikishe tuwe na wataalam wengi ambao ni wasomi.

Sasa utakuta wanafunzi wengi wanakosa kupatiwa mkopo kwa wakati, hii inasababisha kuacha masomo bila ya kutaka kwa sababu ukitizama wanafunzi wengi ni watoto wa masikini, wanategemea sana Serikali yao baada ya juhudi zao za kusoma wapate na mikopo ili iwaendeleze kwa wakati ndivyo tutapopata mabingwa wazuri ambao ni wasomi, lakini utakuta kwamba wanafunzi wanaacha masomo bila ya kutaka kwa sababu mkopo ameukosa au hakupata kwa wakati. Ukienda kwenye familia hata wakichangishana lakini katika Elimu ya Juu kama hukufikisha pesa iliyotakiwa ndivyo utakavyozuiliwa masomo.

Kwa hivyo, mimi namshauri Mhe. Waziri, akija atujulishe kwa nini na kuna sababu gani za wanafunzi kwamba wasipate mikopo kwa wakati, hili linatakiwa kwamba Mhe. Waziri, ahakikishe kwamba kwa vile vuna Serikali zetu mbili zote zinatoa mikopo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zote zinatoa mikopo, iweje wanafunzi kidogo kama hawa usiweze kuhakikishiwa kwamba wanapata juhudi ya kuweza kupata masomo kwa wakati na kuweza kujiendeleza ili tukahakikisha kwamba tunaondokana na matatizo ya wataalam ambao tuna shida nao sana katika nchi yetu, hivi sasa tunategemea kufanya mambo mengi. Kama hivi sasa tunataka kuchimba gesi, tunataka kuchimba mafuta, hiyo yote inatakiwa tuwe na wataalam isiwe kwamba mchimba mawe ndio ataweza kuchimba mafuta au kuchimba gesi, gesi na mafuta yanachimbwa kwa utaalam.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri, ahakikishe kwamba anafanya bidii zote ili kuhakikisha vijana wetu wanapata elimu na kuweza kuhakisha kwamba wanakwenda katika teknolojia ya kisasa katika mambo ya masomo. Kwa kweli Mhe.Mwenyekiti, kutokana na wakati na kwa kuwa muda uliotoa ni dakika kumi, mimi sitaki kuula

muda wako naweza kusema kwamba huo ndio mchango wangu kwa leo kuhakikisha Wizara hii inafanya juhudi kwa ajili ya kupata wanafunzi bora na elimu bora. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti,...

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, juzi tulizungumza hapa kwamba hii ni Wizara muhimu sana na tukaomba kwamba tupewe muda wa kuweza kui-*digest* hii hotuba kusudi Waheshimiwa waweze kulisaidia Taifa katika Wizara nyeti kama hii, na kwa kuwa wachangiaji bado wapo leo unampa Mhe. Nassor dakika tano na kuna wengine bado wako huku, huoni kwamba ni kumkosesha na wigo wa mawazo Waziri wetu wa mambo ya taalim na mambo mengine ili akaweza kuisaidia Serikali kuweza kufanya vizuri katika mambo ya elimu. Isengekuwa vyema kwa sababu muda upo na siku ilikuwa tumalize tarehe 30 mmekata mpaka tarehe 26, nadhani mnataka kukata mpaka tarehe 14 sasa, kwa nini msiwape muda hawa Waheshimiwa wakachangia wakatoa mawazo ambayo yatamsaidia sana Mhe. Waziri, katika kuleta ufanisi katika Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti: Imenibidi nisimame Mhe. Mjumbe, chombo hichi kinaendeshwa kwa mujibu wa taratibu, sasa aliyeomba dakika tano sio mimi, ni yeye mwenyewe kwa taarifa hii na hatukumkatalia mtu kuchangia pamoja na umuhimu wa Wizara hii, lakini majina yenyewe sina ya wale watu ambao walipaswa kuniletea huku kwa ajili ya maombi ikesha niendelee kuwapa nafasi ili wachangie. Baada ya kwisha kuona utaratibu huo, ndio maana nimempa dakika ambazo ameziomba na baadae nimemuomba Mhe. Naibu Waziri, ili aanze kujibu, kwa hivyo, hakuna tatizo katika hilo naomba tuheshimu hilo tuendelee na taratibu. Ahsante.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Sitaki kubishana na kiti Mheshimiwa, mimi ni mzoefu katika mambo ya Mabunge haya na wala sio hili Bunge la Zanzibar tumeshafanya kazi katika jengine kubwa la nchi, kwa maana ya Bunge la Jamhuri ya Muungano, ni mzoefu katika mambo ya mijadala kwa sababu Mhe. Spika, anapokuwa hana watu huangalia katika *audience* ya Baraza au Bunge akauliza majadiliano yanaendelea, mabunge yote ya *Commonwealth* yanafanya hivi na Maspika wote wa *Commonwealth* wanafanya kitu kama hichi, kwa nini Mheshimiwa, leo hutufanyii hilo kuhusu majadiliano yanaendelea.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nilikwisha kuwasiliana na Mhe. Spika, tumekubaliana hivyo, naomba Mhe. Nassor Salim Ali, tuendelee.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa na kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii japo ndogo, aidha, pia nichukue nafasi hii ya kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuleta maendeleo ya elimu katika Wizara yetu na nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kuungana na kumpongeza sana Mhe. Ibrahim Hussein Mkungu, kwa mchango wake mzuri alioutoa hivi punde na kuweza kusema maneno ambayo yana ukweli ndani yake, katika kipindi cha miaka miwili na nusu kilichopita cha mwanzo mimi nilikuwa katika kamati ya Wizara hii Kamati ya Ustawi wa Jamii ambayo inasimamia Wizara ya Elimu, na katika kipindi hicho niliwahi kutembelea pia katika skuli hiyo ya Kengeja ikiongozwa wakati ule kamati yangu ikiongozwa na Mhe. Amina Iddi Mabrouk ambae ndio alikuwa Mwenyekiti wetu.

Kwa kweli tulipotembelea skuli ile tulipata masikitiko makubwa kama alivyosema Mhe. Ibrahim Hussein Mkungu, skuli ile ni skuli kongwe, skuli ya zamani kweli kweli, lakini hali halisi ya mandhari ya elimu katika skuli ni mbaya, ni mbaya na inasikitisha sana na tulipofika pale tukaona jengo moja ambalo haliko katika hali nzuri ambayo imeshaanza kujengwa, lakini kamati yetu kipindi kile ilifanyia kazi ili kuwasiliana na Waziri husika wakati ule Mhe. Ramadhani Abdalla Shaaban, lakini kwa kazi nzuri aliyoifanya kipindi kile baada ya muda mchache banda lile liliweza kumalizika na leo hii banda lile lina wanafunzi ambao wanaendelea na masomo.

Lakini pia kuna eneo ambalo tayari wananchi wameanza kujenga banda jengine ambalo lilikuwepo pale zamani, hebu niiombe Wizara kupitia Mhe. Waziri, aweze kulifanyia kazi ili angalau banda lile ambalo wananchi tayari wameanza kulijenga basi kumalizika ili iweze kuwa na majengo ya kisasa kama vile ambavyo Serikali yetu imeanza kujenga majengo mbali mbali, katika skuli mbali mbali katika kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema haya, pia, nizungumzie suala zima la skuli ya msingi ya Rahaleo, Skuli ya msingi ya Rahaleo iko katika hali ambayo ya kusikitisha sana hata katika maeneo ya mabanda kuna maeneo mengi pale mabanda yote yanavuja, na mimi nimeshafanya ziara pale ya kutembelea skuli ile na tayari nimefanya mipango ya kuweza kufanyiwa ukarabati lakini hata hivyo ukarabati ambao nimepanga hautotosheleza ili kuweza wanafunzi wetu kusoma katika mazingira mazuri.

Kwa hivyo, niiombe Wizara kuweza kufanya juhudi ili kuweza kufanyajia ukarabati skuli ile na angalau kupata madawati japo ya waalim kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, skuli ile ina mabanda takriban 16, lakini hakuna banda hata moja lenye vikalio, nakusudia madawati humu, wanafunzi wanakaa chini angalau kupitia Mbunge na Muwakilishi waliweza kufanya angalau marekebisho ya *floor* kwa kuondoa yale mavumbi vumbi. Lakini ningeiomba Wizara kuhakikisha kwamba angalau kusaidia madawati kwa kuweza kukalia wanafunzi wetu katika skuli ya Rahaleo.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kuipongeza sana sana benki ya *NMB,* imeweza kusaidia kompyuta kwa ajili ya skuli za msingi katika skuli ya Makadara, hali kadhalika skuli ya msingi ya Kwamtipura, lakini kwa kuweza kutoa ahadi ya kusaidia kompyuta pamoja na madawati kwa Skuli ya Rahaleo pamoja na skuli ya Kengeja, haya yote yametokana kutokana na juhudi ya viongozi ambao wa majimbo yetu Jimbo la Rahaleo na Jimbo la Kwamtipura. Kwa hivyo, niiombe Wizara kukaa karibu na wahisani hawa ambao huwa wanasaidia sana katika kuleta maendeleo katika skuli zetu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima katika hotuba ya Mhe. Waziri, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, mimi niipongeze sana Serikali kwa juhudi zake kubwa ambazo imezichukua katika kuinua elimu Zanzibar. Mheshimiwa, kuanzisha programu mpya sita ambazo Shahada ya Elimu ya Mjumuisho, Mahitaji Maalum, Shahada ya Elimu ya Michezo na Shahada nyengine, kwe kweli ni kitu kikubwa na kitu cha kupongeza sana. Niipongeze sana Serikali kwa kuweza kufanya masuala kama haya kwa sababu haya ndio maendeleo, lakini kama hayatoshi Chuo Kikuu cha Zanzibar leo wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu takriban 3,295, ni kiwango kikubwa na kiwango ambacho sisi tunahitajika kuipa pongezi sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Lakini kama hayo hayatoshi Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, leo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu katika bajeti ya 2014/2015 ilikuwa na kutoa mikopo ya wanafunzi 1,200, lakini imeweza kutoa mikopo kwa 1,611, haya yote ni matunda mazuri sana ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ni matunda ya Rais wetu kipenzi DK. Ali Mohammed Shein na ni kazi nzuri ya Mhe. Waziri pamoja na Naibu na Makatibu Wakuu.

Kwa kweli sote watu wazima, sote ni viongozi, lile zuri tunaloliona lazima tuliseme na tulipongeze, kazi inayofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kazi nzuri na haya yote ni katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa hivyo, ni wajibu wetu sisi kama viongozi tunaosimamia Serikali tuyaseme yale mabaya na mazuri ambayo tunayoyaona, ni wajibu wetu huo.

Wale ambao wanaolaumu kila kitu hata kikiwa kizuri sisi tunalaumu, haifai, inafika wakati inapofanya mambo mazuri Serikali yetu tuiseme kwa uzuri, kwa hivyo, haya yote ni kazi nzuri ya Dk. Ali Mohammed Shein na mimi nina imani kwamba niungane na mwenzangu Mhe. Baa, kumuomba Dk. Ali Mohammed Shein agombee tena 2015 ili awe Rais wetu amalizie kipindi cha 2015/2020 ili kumalizia ile mipango aliyoiweka katika kuleta maendeleo kwa Zanzibar.

Baada ya kusema hayo machache kwa dakika zako tano Mhe. Mwenyekiti, ulizonipa namalizia kwa kuiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rahaleo naunga mkono asilimia mia moja nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia kwanza kutokana na hali ya wajumbe *quorum* kwanza haijatimia na akitoka Mhe. Naibu Waziri, anaingia Mhe. Waziri, Mheshimiwa na kwa kuwa kutokana na hali ilivyo hii Wizara tuliseme muhimili mkubwa sana ili sasa Mheshimiwa, kumpa Waziri papo kwa papo ili kuweza kujibu hoja, huoni kama tutakuwa sisi Wajumbe hatutapata hoja ambazo zilizokuwa za msingi na wananchi watatuelewa vipi, naomba kiti Mheshimiwa nilisikia unasema kuwa wewe ndio kiti, ndio mwenye maamuzi, ushauri utoe weye, maarifa utoe wewe, ndio tunavyotaka sisi Mheshimiwa, naomba kiti chako kinieleze.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba tufahamiane, muwache Mhe. Waziri, aendelee kujibu hoja, hayo ambayo unayazungumza ya *quorum* tutaangalia wakati wa kupitisha vifungu, kwa sasa tumpe nafasi Mhe. Waziri, ajibu hoja na hayo mengine yatafuata baadae.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushkuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwanza Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti, pili, nawashukuru wote Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ambao wamechangia hotuba yetu hii na michango yao tunaipokea na tunaithamini na michango yao kwa kweli ilikuwa imeelekeza zaidi katika kujenga Wizara hii, ili kuhakikisha tunafanya vizuri zaidi. Mhe. Mwenyekiti, utambuzi wa nani kachangia, mwenyewe Mhe. Waziri, atakuja kumtaja mmoja baada ya mwengine mimi naomba moja kwa moja niende katika hoja ambazo zilijitokeza.

Hoja ya kwanza ambayo nilitaka kuchangia ni ile hoja ya Mhe. Mohammed Haji Khalid wa Jimbo la Mtambile na Mhe. Fatma Mbarouk wa Jimbo la Amani, wao walitaka kujua sababu zilizopelekea pesa za miradi ya maendelea kutoka katika michango ya serikali kutopatikana. Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwajibu Waheshimiwa Wajumbe, kuwa sababu za kutopatika fedha za miradi kama ilivyopangwa, zaidi wanaweza kulijibu suala hili ni Wizara ya Fedha. Hata hivyo, wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Fedha tumekuwa tukifuatilia kwa karibu zaidi ili kuhakikisha zinapatikana fedha hizi kwa kadiri uwezo unavyoruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohammed Haji Khalid na Mhe. Hamad Masoud, walionesha wasiwasi wao kwa kuondoshwa michango ya wazee katika ngazi ya Elimu ya Msingi na walitaka kujua wizara imejipanga vipi katika kukabiliana na suala hili. Napenda kulijibu suala hili kama hivi ifuatavyo.

Suala la serikali kuondoa michango ya wazee lilianzia na ripoti ya tathmini ya utekelezaji malengo ya elimu ya lazima kwa wote. Moja ya changamoto ambazo zilijitokeza katika ripoti hii ni kuwa bado shabaha ya kufikia asilimia 100 ya uandikisha ya watoto wote wenye umri sahihi wa elimu ya msingi haijafikiwa. Moja kati ya sababu ya kutofikia ni kuwa baadhi ya wazee wanashindwa kukidhi mahitaji ya watoto wao ya kupata elimu kutokana na hali ya umasikini. Hivyo, serikali imeamua kuwaondoshea wazee michango na hivyo kuifidia gharama hizo. Wizara ilitayarisha kwa gharama ambazo zitakazo hitajika kufidiwa na serikali na

hivyo kukubalika na majadiliano na Wizara ya Fedha. Hivyo, ni imani yetu wizara kuwa kiwango cha fedha kilichowekwa kitatolewa ili kutekeleza azimio haya.

Mhe. Mwenyekiti, katika kufidia michango ya wazee katika ngazi ya elimu ya msingi, Wizara itazipatia skuli vifaa vifuatavyo kwa wanafunzi wote wa skuli za serikali. Vifaa ambavyo tutavipatia Maskulini ni; mabuku, chaki, daftari la mahudhurio, manilla, karatasi za kuandikia, gundi, mkasi, *marker pen*, vifaa vya maabara na vitabu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Marina Joel Thomas, alishauri tenda za kutengeneza madawati wapewe Skuli za Ufundi za Mikunguni au Kengeja. Mhe. Mwenyekiti, suala hili ni zuri na hata Wizara ingependelea hivyo. Hata hivyo, taratibu na Sheria za manunuzi ni lazima zifuatwe na tenda. Tenda hutolewa na wizara na yeyote yule atakaeshinda tenda hiyo kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa hupewa kazi ya kufanya *furnitures* hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Marina Joel, Mhe. Moh'd Haji , Mhe. Panya Ali na Mhe. Hamad Mbwana, walitaka kujua kwa mujibu wa uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi waliopo wanatosha hakuna upungufu kama inavyoonesha katika (ukurasa 82 wa kitabu cha bajeti)

Maelezo ya suala lao, kinachojitokeza ni mapungufu katika upangaji hasa kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha kuwalipa walimu nauli kwenda skuli za vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Moh'd Mbwana, alilizungumzia suala hilo kuhusu upungufu wa madarasa ya maandalizi. Ni kweli upungufu wa madarasa ya maandalizi tunao, lakini wizara inakabiliana na changamoto hii kwa kuanzisha madarasa ya maandalizi katika skuili za msingi, sambamba na hilo walimu wanapatiwa mafunzo ya kufundisha madarasa hayo. Hii itasaidia kupunguza tatizo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamad Masoud, pia, alizungumza suala la walimu kufanya biashara katika skuli. Mheshimiwa, ni kweli kwa baadhi ya walimu wanajihulisha na masuala ya biashara katika skuli. Suala hili lilipigwa marufuku na wizara kwa toleo rasmin. Hata hivyo bado inaonekana suala hili bado linaendelea. Lakini kinakinachojitokeza inaonekana ni baadhi ya walimu wakuu kutosimamia vyema suala hili. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nimuahidi Mhe. Hamad Masoud na Baraza lako tukufu kwamba Wizara itajitahidi kulisimamia suala hili ili liweze kutoweka katika maskuli yetu.

Vile vile, Mhe. Panya Ali Abdulla, alizungumzia suala la walimu wale wamefanya vizuri na alihisi kuwa ni vizuri basi walimu wale tuwaajiri.

Mhe. Mwenyekiti, walimu wanaofundisha TUTU kwa sasa ni walimu wasaidizi tu, ambao hawajapata mafunzo kamili ya ualimu. Kivyo, kwa hivi sasa hawana sifa za kuajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Saleh Nassor Juma, alizungumzia masuala ya migogoro wa ardhi baina ya Baraza la Wawakilishi na taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia**.** Kimsingi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haina taarifa ya migogoro ya ardhi baina ya Taasisi ya Karume na Baraza la Wawakilishi. Wizara haijapokea malalamiko ya maandishi au mdomo kutoka Baraza la Wawakilishi kuhusiana na mipaka ya Baraza na Taasisi.

Wizara inafahamu uwepo wa jengo la Baraza la Wawakilishi ndani ya eneo la Taasisi na limeweka uzio kumaanisha ndio sehemu ambayo wameitumia kwa ujenzi. Wizara haikuwa na pingamizi kubwa na hilo kwa kuwa makubaliano ya awali yalifanyika ingawa sehemu iliyojengwa Baraza haikuwa ile ya makubaliano ya awali wala nafasi iliyotumika iliongezeka kidogo. Wizara iliweka uzio sehemu iliyobakia kwa upanuzi wa Taasisi na mwezi unaokuja ujenzi wa upanuzi wa Chuo hicho utaanza rasmi.

Tunaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuiwezesha Taasisi ya Karume kuongeza majengo ambayo yatawaongeza nafasi vijana wetu kujiongezea elimu ya ufundi ambayo ndio tegemeo kubwa la ukuwaji wa uchumi kwa wa nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya maslahi ya walimu, nawashukuru wajumbe wote waliochangia hoja hii. Hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa wafuatao:

Mhe. Muhamedraza Hassanali Mohamedali
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Moh'd Mbwana Hamadi
Mhe. Marina Joel Thomas
Mhe. Hassan Ibrahim Makungu
Mhe. Hamad Masoud Hamad
Mhe. Panya Ali Abdalla

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe hawa wote wamechangia kwa uchungu juu wa maslahi ya walimu na mimi mwenyewe binafsi na Wizara yangu tungependa sana kuona kuwa posho na malimbikizo ya walimu yanalipwa kwa wakati. Hata hivyo, Wizara yangu imechukua hatua zifuatazo katika kuhakikisha kuwa malimbikizo na posho zote za walimu zinalipwa:

1. Kufanya mkutano maalumu wa kujadili utaratibu wa kulipwa malimbikizo na posho za walimu kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wizara ya Fedha. Kikao kilifanyika tarehe 26/03/2015 na kilihudhuriwa na Waziri wa Fedha na Mhasibu Mkuu wa Serikali.

2. Mhe. Mwenyekiti, Kuendelea kufanya uhakiki taarifa za walimu ili kujua ni walimu wangapi wanastahiki kulipwa malimbilikizo na posho husika.

Ahadi iliyotolewa na Waziri wa Fedha katika kikao hicho ni kuwa walimu wote watalipwa malimbikizo na posho zao kabla ya mwaka wa Fedha wa 2015/2016 kumalizika. Hadi sasa walimu 1344 (594 Pemba na 750 Unguja) ambao ni wa kundi maalumu waliorekebishiwa mishahara yao kuanzia mwezi Novemba na Januari, 2015 bado hawajalipwa malimbikizo yao. Walimu hawa kabla ya marekebisho walikuwa na mishahara ambayo haikuzidi 274,000 na wamefanya kazi zaidi miaka 30.

Pia, wapo walimu wanaodai kulipwa malimbikizo yao baada ya kurudi masomoni ambao ni 677(532 Unguja na 145 Pemba). Pia, walimu 6487(3818 Unguja na 2669 Pemba) bado hawajalipwa posho la likizo.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu itafanya kikao chengine maalumu na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kutafuta njia ya kulipwa kwa malimbikizo na posho za walimu mara tu baada ya kumalizika kwa Kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya walimu wanaosoma katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia kupatiwa ruhusa na wizara. Hoja hii ilichangiwa na Mhe. Moh'd Mbwana wa Jimbo la Chambani. Ni kweli kuna walimu kutoka Skuli za Msingi ambao wanajiendeleza katika taasisi hii. Walimu hawa ni walimu ambao hawana sifa ya kusoma masomo ya diploma na hakuna masomo ya diploma kwa Tanzania hii ambayo mtu atasoma kwa kiwango cha sifa cha pasi ya D tu.

Ndiyo maana Wizara hadi sasa haitambui diploma hii. Wafanyakazi hawa wameomba ruhusa ya kujiendeleza kwa kusoma wakati wa jioni na wizara ikawaruhusu, lakini si kwa masomo ya diploma. Hawa wanajiendeleza kwa masomo ya Hisabati na Kiingereza ili kunyanyua kiwango chao. Hata taasisi hii ilipotakiwa kuwasilisha wizarani sifa za walimu hawa imeshindwa hadi hii leo. Walipewa ruhusa ya kujiendeleza wakati wa jioni na asubuhi waendelee na kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, suali la Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Mtambile Mhe. Moh'd Haji Khalid, kuhusu haki za walimu wanaosimamia mitihani mwaka 2014. Tayari walimu waliosimamia mitihani ya darasa la saba Pemba na waliosimamia

kidato cha pili Unguja wameshalipwa. Juhudi za kuwalipa wasimamizi waliobaki wa kidato cha pili Pemba na darasa la saba Unguja zinaendelea kufanyika na walimu hao wanatarajiwa kulipwa karibuni kabla ya kumaliza bajeti ya mwaka huu wa fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili asubuhi nililijibu uzuri katika swali Nam. 27 kwa urefu sana. Naomba Mheshimiwa Mwakilishi aamini hivyo kwamba pesa hizi zitalipwa kabla ya bajeti hii kumalizika ya 2014/2015.

Idadi ya Wasahihishaji wa mitihani kutoka Pemba. Hakuna kiwango maalumu cha wasahihishaji kilichowekwa kutoka Pemba. Isipokuwa idadi ya wasahihishaji huongezwa kadiri hali ya kifedha na haja inavyoruhusu. Mfano, mwaka 2013 walikuwa 80. Mwaka 2014 walifikia 108.

Mhe. Marina Joel Thomas, pia aliishauri wizara kufanya utafiti wa matokeo ya mitihani ili kubaini sababu za kutofanya vizuri kwa skuli za vijijini.

Mheshimiwa Mwakilishi, utafiti wa kubaini sababu zinazopelekea matokeo ya wanafunzi wa vijijini kuwa chini ukilinganisha na wanafunzi wa maeneo ya mjini. Ni kuwa utafiti umeanza kufanywa na miongoni mwa changamoto zilizojitokeza ni pamoja na utoro na muamko mdogo wa wanafunzi katika kufuatilia masomo yao.

Mhe. Muhammed Haji Khalid, pia alitaka kujua juu ya mitihani ya darasa la sita na saba kama mitihani hiyo itafanyika kwa pamoja au vipi. Mtihani wa darasa la sita na saba itakuwa tofauti kwa idadi ya masomo, aina ya masuala ya mitihani, pia mitihani hiyo itafanywa kwa siku tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, pia, palikuwa na suala ambalo lilijitokeza katika Kamati ya Ustawi wa Jamii Wanawake na Watoto. Hoja ambayo ilijitokeza moja ilikuwa ni wizara imeanza kutekeleza Mtaala wa Elimu ya Msingi wakati haikujipanga kwa vitabu vya kufundishia.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa wizara iko katika utaratibu wa kuandika vitabu ni mategemeo yetu mnamo mwezi wa kumi wa mwaka huu vitabu vya madarasa ya tano na sita vitakuwa tayari.

Mhe. Marina Joel Thomas, alishauri kwamba masomo ya Sayansiskim na Ujasiriamali yafundishwe katika skuli kuanzia kidato cha kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri huo tunauchuwa na tumeanza kuufanyia kazi. Hata hivyo, kwa hivi sasa tumeanza kwa Skuli ya Sekondari ya Ben Bella tayari inafundisha masomo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Saleh Nassor Juma Mwakilishi wa Jimbo la Wawi, aliuliza kuhusu mzozo wa ardhi skuli ya Ndagoni Pemba. Namuomba Mheshimiwa Mwakilishi alisema bila ya kupata jawabu basi hatutopitisha bajeti yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ukumbuke kama ni wewe ambae ulinijuilisha suala hili mtu wa mwanzo na mimi sikudharau nilichukua hatua moja kwa moja ya kwenda Ndagoni na kuonana na wahusika na kukagua shamba lote lile pamoja na wahusika na watu wa Wizara na Masheha. Lakini mpaka hivi sasa hatua zifuatazo zimechukuliwa.

Tayari limefikiwa makubaliano baina ya wadai (warithi) wa ardhi hiyo na uongozi wa Wizara ya Elimu, Pemba tangu tarehe 31/12/2014 kwa barua ya makubaliao yenye kumbukumbu PSC/77/14 nakla imeletwa kwangu Naibu Waziri wa Elimu na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba na Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake Pemba na makubaliano yafuatayo yalifikiwa:-

a) Kutayarisha mipaka mipya,
b) Kuchapa hatimiliki mpya, na
c) Madai yakufikiriwa kulipwa chochote kama fidia kwa ardhi hiyo ambayo kwa eneo la kujengea Skuli.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kauli moja warithi wa ardhi hiyo wamekubaliana na kuweka saini zao. Kwa hivyo, Mheshimiwa ninakuomba utupitishie bajeti yetu hii ili basi tupate hizo nguvu za kuweza kuwalipa warithi hao kile kiasi kidogo cha fidia ambacho walikitika kwa wizara iwafidie.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi walichangia hoja hii kwa nguvu kubwa sana na walichangia wajumbe wengi.

Mhe.Moh'd Haji Khalid, Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Moh'd Mbwana, Mhe. Hamad Masoud, Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Saleh Nassor Juma, wote hawa walichangia hoja ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa wote hawa waliguswa na tatizo la wanafunzi kuchelewa kuingiziwa fedha zao za ada na posho ya kujikimu, hali ambayo inazorotesha usomaji wao wakiwa vyuoni na kusababisha kufanya vitendo visivyofaa kinyume na maadili yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha tunaomalizia, Bodi ilipangiwa kutumia shs. 9.3 bilioni na kati ya fedha hizo hadi Mei 2015 Bodi imeingiziwa shs 4.9 Bilioni sawa na 52% ya bajeti yetu ambayo ilitengwa. Fedha hizo zilianza kupokelewa katika mwezi wa Septemba 2014 na kutumika kwa kulipia ada ya

vyuo vya nje na kumalizia katika vyuo vya ndani. Aidha, Bodi imetumia fedha za ndani shs. 750 milioni zilizokusanywa kutoka kwa wakopaji walio hitimu mafunzo yao.

Juhudi ya kuihimiza Serikali kupatikana kwa fedha kwa wakati inazidi kuchukuliwa. Katika suala la Wanafunzi wa Zanzibar walioko Algeria lililoulizwa na Mhe. Hamad Masoud, ni kwamba wanafunzi hao wamepata *scholarship* na hiyo kupitia Bodi ya Mikopo ya SMT. Jadweli liliomo katika kitabu linaonyesha wanafunzi walioko vyuo vya nje wanaodhaminiwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar. Hata hivyo, wanafunzi wa Zanzibar waliopata *scholarship* za nje kupitia SMT wameelezwa katika kitabu cha bajeti katika ukurasa 48, kifungu 123 sambamba na wanafunzi wa nchi nyengine wanaosoma. Kuhusu ongezeko la wanafunzi 411 wa ziada waliodhaminiwa kutokana na kupatikana kwa *scholarship* za ziada kutoka China, Sudan na Oman na pia kutumia fedha za marejesho kwa kudhamini wanafunzi wa ziada.

Aidha, itakumbukwa kuwa mwaka jana katika kupitisha bajeti shs. milioni 500 zilihamishwa kutoka mafungu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kupelekwa Bodi ya Mikopo kwa idhini ya Baraza hili kwa ajili ya kuongeza idadi ya wanafunzi kupata mikopo hiyo.

Kuhusu suala la Mhe, Moh'd Haji Khalid, utaratibu wa kurejesha mikopo ulianza mwaka 2013 na hadi sasa jumla ya wanafunzi waliohitimu na kurejesha fedha ni 811 kati ya wanaodaiwa 3,400 waliomaliza kusoma. Aidha, wanafunzi 12 waliomaliza kulipa, madeni yao walikuwa si zaidi ya shs 5,000,000 kwa kila mmoja na wengi walilipa kwa mkupuo.

Mhe. Mwenyekiti, pia, kuna hoja ya ajira ya walimu ambayo hoja ilizungumzwa na Mhe. Panya Ali Abdalla wa Viti Maalum. Naomba kumjulisha Mhe. Panya kuwa wizara yangu tayari imewasilisha maombi mapya ya ajira kwa walimu wa Historia, Kiswahili na English kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza. Wizara pia imewasilisha maombi ya walimu wapya wa Sayansi, Hesabu kwa ngazi ya Diploma. Hivi sasa wizara yangu imekamilisha mchanganuo wa mahitaji ya walimu wa ngazi ya cheti nayo ikikamilika itawasilisha katika Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa hatua. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 wizara yangu imepatiwa nafasi 942 kwa ajira kwa ngazi tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, pia, kuna hoja ambayo ililenga katika Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima. Mhe. Fatma Said Mbarouk wa Jimbo la Amani alizungumza hoja hii. Wanafunzi wa Elimu Mbadala walio umri wa miaka 10 mpaka 15 hupelekwa katika madarasa ya kawaida ya msingi. Utaratibu ulioko ni kuwa wanafunzi hao wenye mika 10 mpaka 15 huwekwa kwa muda tu katika madarasa

hayo na baadae hupelekwa madarasa ya msingi kuendelea na masomo ya msingi. Na wale wenye umri wa miaka 16 mpaka 21 hupelekwa Kituoni Rahaleo kupata masomo ya msingi na fani ili waweze kujiendeleza.

Kuhusu changamoto zilizopo katika kituo cha Rahaleo, suala hili pia lilizungumzwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa zipo changamoto hizi na wizara zimeshaanza kuchukua hatua. Suala la walimu wa fani, Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima kwa kushirikiana na Idara ya Uwezeshaji Utumishi, imeanza kufanya utaratibu wa kuwahamisha walimu wenye fani walioajiriwa kutoka maskulini na kuhamishiwa vituoni. Hadi sasa walimu watatu wamehamishiwa vituoni.

Kuhusu suala la pahala pa kusomeshea fani kituo kinaendelea na utaratibu wa kutafuta wafadhili kwa kujenga *workshop* Kituo cha Rahaleo ili wanafunzi waweze kusoma kwa vitendo. Mhe. Mwenyekiti, pia, suala la vifaa wizara inajitahidi kulipa kipaumbele suala hili ili vifaa vipatikane na vya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kumalizia kwa kuwaomba wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mara tu baada ya Mhe. Waziri, atakapokuja kumaliza kufanya majumuisho basi kuunga mkono hoja bajeti yetu hii ili waweze kutupa fursa kwa yale ambayo wameyazungumza na mengine ili tuweze kuyakamilisha.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nami kupata nafasi ya kufanya majumuisho. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amani kwa kazi nzuri sana sana aliyoifanya, *almost* amenifilisi yale niliyokuwa nataka niyazungumze ameyachangia na ameshayatolea ufafanuzi, lakini hata hivyo na mimi nitazungumza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nataka niwashukuru wajumbe wote waliochangia kwa kusema, kuna mjumbe mmoja tu ndio amechangia kwa maandishi naye huyu ni Mwenyekiti wa Baraza hili peke yake ndio amechangia kwa maandishi. Wajumbe wengine 15 wote wamechangia kwa kusema.

Napenda kuwapa heshima wajumbe hawa niwataje majina yao:-

1) Mwenyekiti wa Kamati
2) Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali
3) Mhe. Fatma Said Mbarouk

4) Mhe. na sasa nampa jina maalum *General* Makame Mshimba Mbarouk
5) Mhe. Mohammed Haji Khalid
6) Mhe. Marina Joel Thomas
7) Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi
8) Mhe. Hamad Masoud Hamad
9) Mhe. Panya Ali Abdalla
10) Mhe. Saleh Nassor Juma, mkereketwa
11) Mhe. Amina Iddi Mbarouk
12) Mhe. Hussein Ibarahim Makungu
13) Mhe. Mussa Ali Hassan
14) Mhe. Nassor Salim Ali

Mhe.Mwenyekiti, ninawashukuru wajumbe hawa wote na ninawapongeza kwa michango yao. Maelezo ya jumla nasema nimeipokea michango yao yote walionishauri, nimepokea ushauri wao na sio kwamba nimeupokea tu, tumeupokea sote Wakuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa sababu tulikutana hivi mchana tulipovunja Baraza tukajadiliana na tukakubaliana. Kwa hivyo, tumeyapokea yote na nakwambieni ahsanteni sana kwa ushauri wenu.

Mhe.Mwenyekiti, kwa heshimia kubwa nianze sasa kuchangia hoja za wajumbe mmoja mmoja isipokuwa wale hoja zao zimeshajibiwa na Mhe. Naibu Waziri. Kwa heshima kubwa sana naomba nichangie hoja ya Mhe. Raza. Mhe. Raza, ni swahibu yangu sana, lakini ninasikitika sana pamoja na kwamba kuhusu Skuli ya Kiboje tulikutana mimi na yeye tukaizungumza, tukakubaliana na pale tulipokuwepo mimi na yeye alionesha amefurahishwa sana sana sana. Lakini leo ninasikitika sana Mhe. Raza, huyu huyu amelifufua tena suala hili la Skuli ya Kiboje kama kwamba hatukulizungumza wala hatukukubaliana.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikupe taarifa tumezungumza nini. Skuli ya Kiboje alinambia skuli ile haifai hata kulala ng'ombe wala punda jinsi ilivyochakaa na ile skuli ina jina la Rais mstaafu Kamandoo, alizungumza hivyo. Mimi nilistaajabu sana kwamba kuna skuli haifai kulala hata ng'ombe wala punda nikenda haraka Kiboje kuitizama skuli hiyo. Kwanza hao punda na ng'ombe, sikuwakuta na mimi nilistaajabu sana, lakini mimi niliporudi Kiboje nikamwambia mimi punda na ng'ombe katika ile skuli uliyonambia wanalala punda na ng'ombe hawapo, lakini ile skuli jinsi ilivyochakaa, mimi natafuta wafadhili waijenge upya ile skuli, kuikarabati sisi tu peke yake haitoshi na gharama zitakuwa kubwa sana, hilo nilimwambia Mhe. Raza.

Kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu ametuletea Diaspora anaitwa *Milele Foundation Zanzibar*. Diaspora huyu ameamua kutusaidia na akataka tumkaguze skuli zote zetu za Unguja na Pemba ambazo bado hatujazikamilisha tukamkaguza.

Tukatiliana *MOU* mkataba mdogo kwamba atazijenga Skuli 20, atazijenga upya na kila skuli atajenga nyumba ya mwalimu, tumekubaliana hilo na hilo ndilo nililomwambia Mhe. Raza.

Katika uteuzi wake huyu bwana au hawa Diaspora skuli ya Mhe. Raza, ilikuwa ni skuli 4 za mwanzo za Unguja. Alisema nitajenga Skuli 4 za mwanzo za Unguja na skuli 3 za mwanzo za Pemba, anakaribia kuzimaliza hizo skuli 4 ukiacha hii skuli ya tano ya Mhe. Raza. Alituahidi ataijenga Skuli hii kabla ya kumalizika mwaka huu wa Serikali yetu, yaani kabla ya uchaguzi.

Na kwa ujenzi wa skuli hizi mwenye kutaka kuziona anavyozijenga na anavyozikarabati kwa Unguja aende Mbuyutende, kwa Kaskazini "B" ende Kaskazini "B" mwisho kule pwani kule akaione skuli ilivyojengwa na nyumba ya mwalimu ilivyojengwa upya. Sasa hayo yote nilimuelezea Mhe. Raza, leo nastaajabu kwamba Mhe. Raza, amekuja na picha, amekuja na maneno mazito na makali. Kweli ni wajibu wake kuzungumza ili wawakilishi wenzake wamsikie, lakini kubwa alilolizungumza Mhe. Raza, ni kujenga skuli mbili na kutia madawati, Wizara ya Elimu tumemjengea skuli nne katika eneo hilo hilo lake na tumetia madawati na kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti, kama hayo hayatoshi kama yeye amejenga skuli mbili za madarasa mawili mawili, sisi tumejenga skuli moja kubwa ya ghorofa. Tumemjengea katika jimbo lake; skuli moja kubwa ya ghorofa katika hizo skuli 19 tunazosema moja iko kwake. Huyu bwana mimi rafiki yangu sana huyu sijui kwa nini kaja hivi leo, lakini ni wajibu wake asikike na mimi ni wajibu wangu niseme sasa hivi watu wanisikie, Mhe. Raza, tumemjengea skuli na hii skuli hiyo anayoonesha picha tutaivunja yote na tutaijenga upya, kabla ya uchaguzi.

Sasa kama anazungumza amepewa ahadi lakini hajui ahadi hii itatekelezwa lini, sasa namwambia na huyu *Diaspora* huyu amesema haendi kujenga skuli nyengine zilizobakia hizo 15 Unguja na 3 Pemba zilizobakia hajengi mpaka hizi azimalize. Sasa ah, haya, sisi tutatekeleza wajibu wetu si kwa sababu skuli na jina la Rais hapana, kwa sababu skuli wataitumia wananchi na sasa hivi haiwezi kutumika. Sasa hivi suala la kwamba haifai kulala punda, haifai kulala ng'ombe mimi naachilia mbalini, skuli tutaijenga. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mchangiaji wa pili alikuwa Mhe. Fatma Said Mbarouk, lakini Mhe. Naibu Waziri, ameshajibu.

Mchangiaji wa tatu alikuwa Mhe. Makame Mshimba, huyu namwita generali kwa michango yake ya leo ningekuwa na cheo cha kumvisha cha ujenerali ningemvisha leo, lakini nakupigia saluti. Nasemaa "mbaya msemeni lakini wajibu wake mpeni",

ndio aliyoyafanya yeye Mheshimiwa, "mbaya msemeni lakini wajibu wake mpeni". Mhe. Mshimba, nakushukuru sana, sana, sana kwa michango yako na imenipa zaidi ya moyo niliyokuwa nao, imenipa moyo mkubwa zaidi wa kushirikiana na wewe, kufanya kazi pamoja na wewe na kukutekelezea mambo yako. (*Makofi*)

Mhe. Mohammed Haji Khalid, keshajibiwa na Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Marina Joel Thomas, ameshajibiwa na Mhe. Naibu Waziri, tena kwa urefu sana na nakushukuru sana kwa muono wako.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, ameshukuru sana kwa hatua tuliyochukua ya kujenga chuo cha maadili ya Kiislamu. Alizungumza kwamba Waislamu wetu wa Unguja hii wamepoteza maadili yao na kadhalika na kadhalika, lakini akapongeza kujengwa chuo hiki cha maadili ya Kiislamu. Na kwa heshima na taadhima namualika kila Mjumbe wa Baraza hili atakayepata nafasi tushatoa pale salamu, Mjumbe akakague akauone ujenzi unavyoendelea. Tunawashukuru sana ma-*contractors* wanaofanya kazi ile na sio tu kwa sababu wanapewa fedha na malipo wanafanya na kadhalika, lakini jitihada yao ya ujenzi inatosha kwamba niwapongeze sana, sana.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tuna ukosefu wa walimu wa msingi kama tulivyo na ukosefu na walimu wa Sayansi katika skuli nyengine, lakini tumo mbioni katika jitihada zetu. Kwa upande wa skuli zetu za Sekondari *Alhamdulillah* Benki ya Dunia imetukopesha pesa tumejenga skuli kubwa sana 19, tumekarabati skuli zilizoharibika 6 Unguja na Pemba, tumejenga skuli nyengine 3 ikiwemo Skuli ya Kiembe Samaki na hivi sasa tuko mbioni kuzijenga skuli nyengine 10 kwa mfano ule ule wa skuli ya Mpendae ya ghorofa moja. Panapo uhai na uzima tutaanza kazi hiyo mapema tukishamaliza ule mchakato wa maabara tulioambiwa tuufanye, tukishamaliza ule tunakuja kujenga hizi skuli.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimjibu Mhe. Nassor Jazira, kabisa ile skuli unayoizungumza ya Rahaleo, tunaijenga mfano ule ule wa Skuli ya Kiembe Samaki, kwa sababu tunajua Skuli ya Rahaleo itachukua watoto wa Darajani Skuli na watoto wa Vikokotoni Skuli na watoto wengine zaidi. Kwa hivyo, tunahitaji tujenge skuli kubwa zaidi ili tuhakikishe kwamba watoto hao wanapata pahala pakusomea.

Mheshimiwa, alizungumzia Bodi ya Mikopo lakini suala hili limeshajibiwa na Naibu Waziri wangu. Alizungumzia Bodi ya Maktaba akatwambia maktaba ndio roho ya elimu yetu, ni kweli kabisa. Nataka nimuhakikishie kwamba kazi nzuri sana inafanywa na Mkurugenzi wa Maktaba na alipoondoka kwenda kuongeza

taaluma yake aliyemuachia alifanya kazi kubwa sana pamoja na kuimaliza maktaba mpya ya Pemba. Kwa hivyo, nampongeza Mkurugenzi wa Maktaba na nampongeza Mkurugenzi aliyeachiwa wakati ule dhamana ya kuendesha maktaba kwa kazi nzuri sana aliyoifanya. (*Makofi*)

Labda niongezee kidogo suala la mikopo, nasema mwaka jana tulipatiwa shilingi bilioni tisa na ushei, tukajitahidi kuwakopesha walimu wetu, wanafunzi wetu. Mwaka huu nilitegemea pesa zile nitaongezewa kidogo kwa sababu ada ya masomo imepanda, maisha yamepanda ya wanafunzi wetu wanaokwenda kusoma na kadhalika badala yake bahati mbaya sana nimepunguziwa kidogo.

Sisikitiki kupunguziwa, lakini kutoka bilioni tisa imekuja bilioni nane, sio tatizo, lakini kutoka bilioni tisa nimepewa bilioni nne, kutoka tisa niliyokisiwa nimepewa bilioni nne. Sasa sijui hizi bilioni nane nilokisiwa sasa nitapewa bilioni ngapi? Lakini namshukuru sana sana Waziri wa Fedha, wala sitaki nimlaumu hata kidogo, matumizi ya serikali ni makubwa sana, sana na matumizi kila yanayokuja mwenye kuyajibu ni yeye, matumizi ukiyatizama tunayafanya ghafla ghafla hata bila ya makisio ni makubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, tuna meli ivo tumenunua, haikuwemo kwenye makisio na imekuja hapa hiyo, lakini tukadhamiria tuchangeni, tuchangeni mfuko wetu tufanye nini, lakini meli lazima inunuliwe na imenunuliwa.

Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hivi karibuni alikuja na wazo ambalo sisi Wizara ya Elimu na serikali nzima tunaiunga mkono *hundred percent* wazo hilo, kwamba wanafunzi au wazee wao wasichangishwe tena. Wanafunzi hao wasisome sasa kwa michango yao, fedha hizi tukazifanyia tukaambiwa sasa leteni makisio, serikali ichangie kiasi gani kugharimia pesa hizi. Tukakaa tukaumiza vichwa mpaka tukapata idadi ya shilingi bilioni sita tukampelekea Rais, tukadhani Rais labda angesema aah, ngojeni kwanza nisitangaze hili, ngojeni kwanza.

Lakini Rais wetu mpendwa alisema bilioni sita si pesa nyingi serikali inaziweza na tutachanga mpaka tutafika, lakini wanafunzi wetu wasitoe tena michango yakujisomea. Rais wetu wa mwanzo Mhe. Mtukufu Rais Abeid Amani Karume alitangaza elimu bila ya malipo. Sasa kama tunamwambia mwanafunzi na mwalimu achange, sasa hiyo ni kinyume chake bila ya malipo lakini changa, ndio hayo hayo. Kwa hivyo, sisi hili hatukulilalia wala hatukuliamkia lakini kwa sababu Rais kasema, tumelifanyia kazi na tumepanga bilioni sita, tumeshampelekea na ameshalitangaza na tumeshalitia katika bajeti mwaka huu.

Kuanzia Julai mwaka huu wanafunzi wanaofanya mitihani hawatolipa gharama za mitihani wala wanafunzi wa *Primary* wanaosoma katika *Primary School*

hawatolipa. Kuna mjumbe mmoja amesema tufanye kazi kubwa yakuwaelimisha wazee wa wanafunzi ili hili walifahamu, kazi hiyo ilianza siku ile ile aliyoitangaza suala hili Rais, siku ya pili sisi tumeanza kufanya kazi hiyo na kazi inaendelea.

Mhe. Bi. Panya, ameshajibiwa, Mhe. Saleh Nassor Juma, ameshajibiwa, limetoka shauri hapa kwamba tuanzishe Chuo cha Masomo ya Uhandisi wa Mafuta na Gesi ili katika huu msako tunaofanya wa kutafuta gesi asilia na mafuta basi na sisi tujitayarishe kwa kujenga wataalamu, ili kwamba huku tunatafuta lakini huku tunatafuta wataalamu.

Nataka nitoe taarifa hii yule aliyemsifu hapa Dkt. wetu Profesa wa Chuo Kikuu cha *SUZA* kamsifu hapa, kajenga hoja kweli kweli ya kumsifu alifanya haki, alifanya vizuri, ndio yale niliyoyasema anayefata vizuri asifiwe. Watoto tumeshawapeleka nchi za nje kwenda kusoma na kozi mchakato uko njiani wa kuanzisha hizo kozi, Mungu akipenda tukianza tu mwakani *Faculty* itakuwepo tayari kufunguliwa na somo la gesi asilia na mafuta litaanzishwa. Lakini hivi sasa wanafunzi wetu zaidi ya 15 wako nje wanasomea suala hili. Kwa hivyo, hatukukaa bure tu kwamba tunatafuta sisi wenyewe tumefunga mikono, hapana na Rais wetu kila siku anatuhimiza yayo kwa yayo hayafai badilikeni na sisi tunabadilika na yeye yuko nyuma nyuma kutuhimiza tubadilike. (*Makofi*)

Mhe. Amina Iddi Mabrouk, tumezipokea pongezi zako umezungumza kwamba tuyatilie mkazo sana masomo ya Sayansi, tutie mkazo sana katika masomo ya elimu ya msingi na ukatoa mfano nyumba iliyokuwa haina msingi mzuri haidumu. Nasema tumeupokea ushauri wako, sio kwamba tutaufanyia kazi ndio katika yale mambo tuliyosema tumeyapa kipaumbele na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia tuyatekeleze.

Tuje kwa Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa), nijibu hoja yako ya mwisho niipeleke mwanzo, uliniomba uliniomba nikujengee skuli Bububu ya kileo, hilo halitaki kuombwa, hilo kwa nini uliombe. Katika *programme* yangu ya kujenga skuli tisa za ghorofa Bububu imo, sio Bububu tu, skuli tisa zote tunazijenga Wilaya ya Mjini Magharibi hatukwenda Donge, hatukwenda Makunduchi, hatukwenda kokote, wala hatukumshauri mwanasiasa yeyote tuzijenge wapi aa, tumeogopa kinyang'anyiro; maana mwanasiasa ndio mwanasiasa, ataseme mimi jimbo langu halina skuli, hapana, tumefanya *survey* sisi wenyewe ya kutosha na tukagundua ni eneo gani wanafunzi ni wengi sana na kigezo kizuri Skuli ya Mtopepo.

Jamani mkipata nafasi tembeleeni Skuli ya Mto Pepo mimi nahimiza kila siku, nimekwenda Skuli ya Mto Pepo darasa moja kuna wanafunzi 200 wanasomeshwa na kuna walimu watatu, mmoja wa kusomesha, wa pili wa kutuliza kelele na wa tatu wa kutunza heshima, tutakwenda namna hii, hatuwezi kusomesha hivi, ndipo

tukaamua safari hii tukatae kwenda vijijini tunakwenda mjini ndio kwenye wanafunzi wengi sana. *(Makofi)*

Mhe. Ibrahim Makungu Ibrahim, huna haja ya kuniomba, katika skuli tisa tutakazozijenga skuli yako imo ya Bububu. Kwa sababu ukitaka kujua Bububu kuna wanafunzi wengi, kaa pale kwenye kuvuka barabara ya wanafunzi mchana wakati wanafunzi wanatoka skuli, ndio utajua pale Bububu pana wanafunzi wengi.

Pia, amenipongeza sana mimi na watendaji wangu wengine, umempongeza Mhe. Rais kwa uadilifu wake na kazi zake anavyozifanya, umepongeza uandikishaji wa wanafunzi wa skuli ya msingi kutoka 317,000 hadi kufikia 390,000 na mimi nazipokea pongezi hizo. Umepongeza serikali kufungua Chuo cha *SUZA*, serikali ndio hii sio awamu hii lakini hii hii ya CCM, wakati ule yuko Kamandoo ndipo chuo kilipofunguliwa na chuo sasa kinaendelea na ukikaa na profesa mwenyewe akikuhadithia hizo *faculties* anazozifungua na kuzianzisha utakamata kichwa. Lakini ni kweli kabisa ana dhamira ya kufanya hivyo, anafanya hivyo na chuo chetu kinakua. Naomba kwa niaba yako Mwenyekiti nami nimpongeze Profesa kwa kazi nzuri sana anayoifanya. *(Makofi)*

Vile vile, amepongeza na wako wengine wametulaumu sana lakini yeye ametupongeza kwa kuchonga madawati, viti na meza na kazi hii ni kubwa sana tuliyoifanya na *Alhamdulillahi* imekwenda vizuri na *Inshaallah* kwa mazungumzo yetu tuliyofanya juzi mimi na Waziri wa Fedha. Mpango tulioubuni hivi karibuni na yeye ndiye muasisi wa mpango huo, kampelekea Rais na Rais kaukubali. Rais kamwambia kazungumze na Wazuri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na Waziri wa Fedha kaja tumezungumza na tumekubaliana, nao ni mpango kama suala la elimu ya masomo ya juu ni suala la Jamhuri ya Muungano, kwa nini na wenzetu wa Muungano hatuwashirikishi katika kuchangia ujenzi wa madawati? Akapanga na tukapanga tukakubaliana tukimaliza bajeti hii tunakwenda Dar es Salaam kwenda kuonana na Waziri Mkuu na wakuu wengine kupanga suala hili. *(Makofi)*

Kwa utaratibu tulioupanga *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitaka tutafanikiwa, lakini wakati ule mpango wetu wa kuchangisha wasafiri wa meli uko pale pale, tukipata mchango huo *fahuwa-lmuradi* tunaendeleza, hatukupata mchango wetu uko pale pale.

Mhe. Mussa Ali Hassan, anampongeza Mhe. Waziri. Mheshimiwa, nazipokea sana pongezi zako, umetaja matatizo ya vikalio ndio hivi nilivyosema, tunaendelea na jitihada ya vikalio kuvitengeneza na sasa tunawashirikisha na wenzetu watusaidie tushirikiane. Lakini tujue tunazaliana sana hata upige kelele vipi uzazi wa mpango. Mhe. Mwakilishi wa Micheweni hataki kusikia suala hilo. *(Makofi)*

Mimi keshanambia simsingizii, tena kanambia vibaya kasema suala la uzazi wa mpango hamfanyi kwenu Donge, unataka utuletee Micheweni, hatufanyi mpango. Sawa tusifanye mpango lakini ilimradi kila tunavyozaa sana mahitaji ya madawati yanaongezeka. Kwa hivyo, sijui lini tutamaliza kutekeleza yale mahitaji yetu ya madawati, lakini tumo katika jitihada.

Suala la Michezo. Hili namjibu Mhe. Fatma Mbarouk Said. Mhe. Fatma, alisema hii wizara nyinyi mnaiita mpya, mbona Wizara ya Michezo iko tokea zamani? Ni kweli kabisa wachezaji wenyewe si ndio sisi, lakini ule mpira wa zama zetu na ile riadha ya zama zetu imetoweka badala yake sasa Mheshimiwa, kalivalia njuga suala hili la michezo, ndio maana akaunda Idara ya Michezo na Utamaduni. Hii ni idara kamili iko katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina Mkurugenzi wake, Mhasibu wake na kadhalika na kadhalika, ni idara kamili.

Mhe. Ibrahim Makungu, alimsifu sana yule Mkurugenzi aliyeteuliwa, akasema yeye anamjua, mtekelezaji mzuri, hodari. Nakubaliana na yeye asilimia mia moja, bwana yule ni mzuri, ni hodari, sijui alishindwa nini kuendeleza michezo katika Idara ya Michezo. Kwa sababu nasikia alikuwa ndio Katibu Mkuu, sijui kilitokea nini. Lakini tumempa nafasi ya kutosha anatuletea mipango mizuri na bajeti yake tumeshamtengenezea, ni hodari sana. Kwa hivyo, hii ni idara mpya kabisa na bahati nzuri iko katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Nassor Salim Ali, pongezi nimezipokea na alimsifu sana rafiki yake Mhe. Ibrahim Makungu (Bhaa), ni wajibu wako. Vile vile, umeitaja skuli yako ya Rahaleo, skuli hiyo ni miongoni mwa hizi skuli tulizozitaja ambazo tunazozitengeneza na tulikuwa tunatengeneza tumefanya *estimate* na kuzitaja na kuzizungumza skuli 10. sasa tunazungumza skuli tisa, kwa nini? Kwa sababu skuli ya Rahaleo itakuwa kubwa zaidi kuliko skuli nyengine hizo tunazozijenga, kwa sababu ni eneo lenye wanafunzi wengi sana. Kwa hivyo, Skuli ya Rahaleo itakuwa ya ghorofa mbili kama ile skuli iliyoko pale Kiembe Samaki, sio kama ya Mpendae kama ile ya Kiembe Samaki.

Kwa hiyo, nimpongeze sana na nimuombe Mhe. Nassor Salim Ali, asichoke kuzungumza na wale jamaa waliovamia lile eneo la pale Rahaleo kujenga duka lao la ulanguzi ili eti watuzuie eneo letu la skuli tusilipate. Sisi ikifika wakati wa kujenga skuli, hatuna mswalie Mtume, hakuna chochote tunakuja kujenga na tunajenga skuli ya kisasa, hatuwezi kuacha watoto wetu hawana skuli, eti kuna mtu kajenga duka kwa uvamizi, hapana.

Tumekipongeza Chuo Kikuu cha Taifa na nimestaajabu sana kwamba ameipongeza Bodi ya Mikopo. Bahati mbaya wengine wameizungumza vibaya lakini mimi nakubaliana na yeye kuipongeza Bodi ya Mikopo.

Kuna Mheshimiwa mmoja hapa alisema jamani mnawalaumu bure hawa Bodi ya Mikopo, mkereketwa wangu yule, alilizungumza hilo. Mnawalaumu bure hawa Bodi ya Mikopo kama hawakupewa pesa watazitoa wapi pesa za kuwakopesha watu? Hilo alilisema Mhe. Nassor, nampongeza sana bwana, ametutetea, kutoka shilingi bilioni tisa tumekuja kiwenye shilingi bilioni nane, hiyo ndio hali na wala simlaumu Waziri wa Fedha, amejikaza kweli kweli.

Mwaka jana hapa tulikuja katika bajeti mpaka tukaamua pesa zetu za *OC*, za safari, tuzikate tuzitie kwenye mikopo. Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alileta wazo hilo na mimi bila ya kuwashauri watendaji wenzangu nikalikubali, tukazitoa shilingi 500 bilioni tukazitia kwenye mikopo, sitaki kusema nini kimetokea, lakini nataka niseme badala ya kuwakopesha watu 1,200 kama tulivyopanga tunakopesha watu 1,422 kwa kukata zile pesa kuzitia huku. Lakini vile vile pesa zetu tunazorejeshewa sasa wanazotulipa, maana hizi pesa zinalipwa ili zizunguke, tumezitia katika mkopo ndio tukapata watu hao 1,422. Mwenyezi Mungu atujaalie tusishuke katika idadi hiyo, lakini iongezeke na *Inshaallah* tutaliweza.

Mwisho, niseme nilitakiwa nizitaje vile vile skuli nne za kisasa tunazojenga Pemba. Skuli moja tunaijenga Wete, Kizimbani; skuli ya pili tunaijenga Micheweni; skuli ya tatu tunaijenga Chake Chake na ya nne tunaijenga Mkoani. Katika zile skuli 10 nilizosema basi hizi nne ndio tunazijenga Pemba na hayo ndio maeneo tutakayojenga na humo mote tumegundua kuna wanafunzi wengi sana, si upendeleo wa Mwakilishi yeyote hapana, lakini ni upendeleo kwamba kuna wanafunzi wengi. Na kule kwa rafiki yangu Mhe. Hija Hassan HIja, ambapo tutajenga skuli moja wanafunzi wa eneo lile wana mikondo mitatu ya kusoma, sisi angalau mikondo miwili miwili, wenzetu wana mikondo mitatu ya kusoma, hakuna sababu kwa nini tusiwajengee skuli yao.

Kwa hivyo, Mhe. Hija Hassan Hija, huko aliko atapata salamu zangu kwamba skuli hii nayo imo katika skuli tisa za ujenzi ambao tutakaojenga hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima sasa naomba kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, amekwisha kutoa hoja, lakini nikiangalia idadi ya Wajumbe hawatoshi kwa kupokea na kuendelea na mambo mengine. Lakini pia tukizingatia na muda nao vile vile haututoshi kwa ajili ya kumalizia kazi iliyokuwepo mbele yetu. Kwa hiyo, basi nahisi niwaombe Wajumbe kazi hii ya majumuisho kwanza kukubali hoja kwa Wajumbe wote na baadae kuja kupitisha vifungu tufanye kesho *Inshaallah* tutakapojaaliwa, tukiamka salama.

Waheshimiwa Wajumbe, nikushukuruni kwa mchango na msaada pamoja na namna tulivyoshirikiana hadi kufikia hapa. Sasa nachukua fursa hii kuahirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 9/6/2015 saa 3:00 barabara za asubuhi. Naomba kuahirisha.

(Saa 2:22 usiku Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 09/06/2015 saa 3:00 asubuhi)